# MAFUNZO YA NYIMBO ZA JANDO NA UNYAGO KWA JAMII YA WAHIYAO WA MASASI, TARAFA YA LULINDI

**HADIJA UTUKULU RASHID**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SHARTI PEKEE LA KUPATIA SHAHADA YA UZAMILI MA-KISWAHILI KATIKA FASIHI SIMULIZI YA KISWAHILI YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2013**

## UTHIBITISHO

Aliyeweka sahihi hapo chini, anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii ya: Mafunzo ya Nyimbo za jando na unyago kwa Jamii ya Wahiyao wa Masasi, Tarafa ya Lulindi kwa ajili ya shahada ya uzamili, katika fasihi simulizi ya Kiswahili, na anaomba ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

…….

Prof. Dr. Sheikh T.S.Y.M Sengo

(Msimamizi)

.....

Tarehe

## HAKIMILIKI

Sehemu yeyote ya tasnifu hii, hairuhusiwi kubadilishwa, kwa njia yoyote iwayo, iwe ya kietroniki, kunakilisha, kurudufu, kaitka hali yoyote, bila ya kupata idhini ya maandishi, kutoka kwa mwandishi wa Tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

## TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi Hadija Utukulu Rashid, nathibitisha kuwa kazi hii nimeifanya mimi mwenyewe na sijaiwasilisha katika Chuo Kikuu Chochote chengine kwa lengo la kupatia Shahada yoyote.

……..

Saini

……...

Tarehe

# TABARUKU

Tasnifu hii ni kwa heshima ya mume wangu Mussa Hassan Minduva, watoto wangu Mitole Hassan, Rahima Hassan na Zakia Hassan wazazi wangu na familia yangu yote, kwani pasipo wao na nguvu za mwenyezi Mungu nisingeweza kuimaliza kazi hii kwa ufanisi mkubwa kama huu.

## SHUKURANI

Nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu (S.W) Kwa kuniwezesha kufanya utafiti na kuiandika Tasnifu hii. Nawashukuru wanafamilia yangu, mume wangu Mussa Hassani Minduva, wanangu, Mitole, Rahma na Zaqia kwa kunivumilia na kunipa utulivu wakati naandika Tasnifu hii. Aidha namshukuru marehemu mama yangu.

Shukrani za pekee ni za Prof. Dr. Sheikh. Mzee Tigiti S.Y. M. Sengo aliyeweza kuisimamia kazi hii. Bila imani yake, uvumilivu na upendo wa dhati na ualimu wake kazi hii isingeweza kufikia mwishoni

Ninaishukuru Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kunifadhili katika masomo. Pia, shukrani maalumu ni za Mkuu wa Chuo Cha Ualimu Mtwara kwa kuniruhusu kukatisha ufundishaji kwa ajili ya kwenda kufanya utafiti wa kazi hii ambayo hitimishi yake ni kwa manufaa ya wanaelimu na wanafasihi wote.

Shukurani zangu za kumalizia ziwaendee walimu wangu wote wa Kitivo cha Fani na Sayansi za Jamii Chuo Kikuu Huria. Pia walimu wote wa kituo cha Mtwara kwa msaada katika kipindi chote cha utafiti. Ninawashukuru wanafunzi wenzangu kwa kunihamasisha kusoma. Mwisho ninawashukuru wote walioshiriki katika kufanikisha kazi hii.

# IKISIRI

Utafiti huu unahusu mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kwa jamii ya wahiyao wa Lulindi Wilaya ya Masasi. Utafiti umechunguza ubora na udhaifu wa mafunzo hayo kwa vijana wa jamii hiyo. Utafiti umelenga kukusanya na kuchanganua data, kuhakiki na kuelezea mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao wa Lulindi wilayani Masasi. Utafiti umeweka msisitizo zaidi juu ya mafunzo ya yapatikanayo kwenye nyimbo za jando na unyago kama tanzu ya fasihi simulizi. Nyimbo za jando na unyago zimekuwa na mjadala mkubwa kwa jamii ya wahiyao. Hii imetokana na mwelekeo hasi wa vijana wa kihiyao. Hali hiyo imechochea kufanyika kwa utafiti huu ili kupata ukweli wa yale yanayosemwa na wasemaje wa tatizo hilo.

## MSAMIATI

Mwenye … kiongozi mkuu katika jamii ya Wahiyao (Kwa asili, Mwenye ni mtu mali, akili, uwezo, hekima, n.k)

Wasyungo … wasichana au wavulana wasiopitia jandoni na unyagoni, msungo, kimosi (Mwanaume), kigori mwari (mwanamke)

Chaamba … ngoma ya kukata viuno wanayochezeshwa vijana wa kike kwa ajili ya mafunzo ya chakula cha ndowa.

Makungwi … walimu wanaotoa elimu ya jando na unyago, mafundi wa kufunda

Ngariba … mwanaume anayefanya kazi ya kutahiri vijana wa kiume, jandoni, si hospitalini.

Masikhara … mizaha

Ndindi … ngoma za nyimbo za unyago

Lupanda … ngoma za nyimbo za jando

UKIMWI…Upungufu wa Kinga Mwilini

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ..... **ii**

**HAKIMILIKI** ..... **iii**

**TAMKO LA MTAHINIWA** ..... **iv**

**TABARUKU** ..... **v**

**SHUKURANI** ..... **vi**

**IKISIRI** ..... **vii**

**MSAMIATI** ..... **viii**

**YALIYOMO** ..... **ix**

**ORODHA YA MAJEDWALI** ..... **xii**

**ORODHA YA VIELELEZO** ..... **xiii**

**UTANGULIZI WA JUMLA** ..... **1**

**1.0 ASILI YA WAHIYAO** ..... **1**

1.1 Utangulizi ..... 1

1.2 Usuli wa Tatizo ..... 3

1.3 Tatizo la Utafiti ..... 7

1.4 Tarjima ..... 8

1.5 Madhumuni ya Utafiti ..... 10

1.6 Umuhimu wa Utafiti ..... 11

**SURA YA PILI** ..... **13**

**2.0 KAZI TANGULIZI** ..... **13**

2.1 Utangulizi ..... 13

2.2 Maana ya Ushairi wa Nyimbo ..... 21

2.4 Jando na Unyago ..... 30

2.5 Chanzo cha Nyimbo za Jando na Unyago ..... 32

2.6 Maudhui ya Nyimbo za Jando na Unyago ..... 35

2.8 Umuhimu wa Unyago ..... 42

**SURA YA TATU ..... 44**

**3.0 NADHARIYA TETE ..... 44**

3.1 Utangulizi ..... 44

3.2 Mkabala wa Kinadharia ..... 47

3.3 Nadharia ya Kijamii ..... 48

3.4 Nadharia ya Kiushumuzi ..... 50

3.5 Nadharia ya Kielimu ..... 51

3.6 Nadharia ya Fasihi ..... 52

3.7 Nadharia ya Kiafrika ..... 55

3.8 Nadharia ya Fasihi Simulizi ..... 56

3.9 Nadharia ya Kitanzania ..... 62

3.10 Nadharia ya Kiulimbe ..... 63

3.11 Nadharia ya Kiafya ..... 65

**SURA YA NNE ..... 68**

**4.0 MBINU NA NJIA ZA UTAFITI ..... 68**

4.1 Muundo wa Utafiti ..... 68

4.2 Mbinu za Utafiti ..... 68

4.2.1 Mbinu ya Usaili ..... 68

4.2.2 Mbinu ya Hojaji ..... 69

4.3 Mbinu ya Ushiriki/Umakinifu ..... 71

4.4 Njia za Utafiti ..... 72

4.5 Uteuzi wa Watafitiwa ..... 72

4.6 Ubora wa Utafiti ..... 74

4.7 Vifaa vya Kukusanyia Data ..... 74

4.7.1 Kirimbo ..... 74

4.7.2 Ngamizi ..... 75

4.7.3 Kamera ..... 75

**SURA YA TANO ..... 76**

**5.0 UCHAMBUZI WA DATA ..... 76**

5.1 Utangulizi ..... 76

5.2 Eneo la Utafiti ..... 76

5.3 Aina ya Nyimbo ..... 76

5.4 Nyimbo za Jando na Unyago Zilizokusanywa ..... 77

5.5 Upungufu wa Ukamilishaji wa Utafiti ..... 89

5.5.1 Watafitiwa Kushindwa Kutoa Maelezo ..... 89

5.5.2 Kutokuyafikia Baadhi Ya Maeneo ..... 90

5.5.3 Baadhi ya Watafitiwa Wameshindwa Kutoa Maelezo Sahihi ..... 90

5.5.4 Kukosekana kwa Vyombo vya Kurekodia Nyimbo ..... 90

5.5.5 Ugumu wa Baadhi ya Maneno ya Kihiyao Ktk Kuyatarijima kwa Kiswahili . 90

5.6 Ukusanyaji wa Data ..... 91

**SURA YA SITA ..... 113**

**6.0 HITIMISHO, MAPENDEKEZO MAREJELEO ..... 113**

6.1 Hitimisho ..... 113

**MAREJELEO ..... 117**

**NYONGEZA ..... 123**

# OORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 5.1: Orodha ya Wahojiwa ..... 94

Jedwali Na. 5.2: Mafunzo Wanayoyapata Vijana Kupitia Nyimbo za Jando na Unyago ..... 94

Jedwali Na. 5.3: Vijana Wanaoona Nyimbo za Jando na Unyago Zina Manufaa ..... 95

Jedwali Na. 5.4: Manufaa ya Nyimbo za Jando na Unyago ..... 96

Jedwali Na. 5.5: Takwimu Zifuatazo Zinaonyesha Umri wa Vijana Walioingizwa Mafunzo ya Jando na Unyago Mwaka 2010 ..... 98

Jedwali Na. 5.6: Takwimu Zifuatazo Zinaonyesha Umri wa Vijana Walioingizwa Mafunzo ya Jando Naunyago Mwaka 2011 ..... 98

Jedwali Na. 5.7: Mchango wa Wazazi Kuhusu Mafunzo ya Jando Na Unyago ..... 99

Jedwali Na. 5.8: Sababu za Wazazi Wanaosema Hakuna Faida ya Nyimbo za Jando na Unyago ..... 101

Jedwali Na. 5.9: Mafunzo ya Jando na Unyago ..... 102

# OORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo Na. 5.1: Mchanganuo kwa Asilimia Kuonyesha Manufaa ya Nyimbo za Jando na Unyago ..... 95

Kielelezo Na. 5.2: Manufaa ya Nyimbo za Jando na Unyago kwa Asilimia ..... 96

Kielelezo Na. 5.3: Mchango wa Wazazi Kuhusu Mafunzo ya Jando na Unyago kwa Asilimia ..... 100

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.0 ASILI YA WAHIYAO

### 1.1 Utangulizi

Neno ‘Yao’’ ni jina la milima ambayo ipo kati ya Mwembe na mto Luchilingo nchini Msumbiji, ambao umeenea hadi Wisulu hadi Lisombe (Yohanna, 1993), ambapo Malingalile wanautumia kwa makazi hadi eneo la Likopolwe na Mkuja nchini Msumbiji. Kwa hiyo Wahiyao asili yao ni kutoka milima ya Yao. Milima ambayo haina miti bali ni mbuga tu.

Wahiyao kama makabila mengine ya hapa Tanzania, wanaishi sehemu zenye mchanganyiko wa makabila mengine ya Wamakonde, Wamwera, Wamakuwa. Makabila haya yanafanana kwa mila na desturi zao. Wahiyao walikuja Tanzani katika makundi mawili. Kundi la kwanza lilipitia mto Ruvuma na kuvuka hadi Tanzania ya kusini sehemu za Newala na Masasi.Wapo waliotoka chini ya utawala wa Kumwembe ambao walipitia Malawi hadi mkoa wa Ruvuma na kuishi Tunduru (Nyagali, 1990) ambako walikuja kutokana na kukimbia vita ya makabila kati yake na Wangoni ,ambao waliweza kuwafukuza Wahiyao katika vita waliyoiita “ Ngondo ja makwangala’’ Vita vya uhasi, (Lucas, 1975) katika *Utani relationship in Tanzania*. Msambao huo umewafanya Wahiyao kuwa na usemaji tafauti wa lugha moja katika matamshi japokuwa kimsingi wanaelewana. Misafara ya Wahiyao kutoka Msumbiji hadi Kusini mwa Tanzania ilisababishwa na vita vya makabila kutoka Afrika ya Kusini vita vya Chaka pamoja na utawala wa Kireno. Pia maeneo yao yalishambuliwa sana na wadudu waitwao “Mbung’o”. (Lucas, 1975) amedokeza

kuwa walishambulia mifugo kama ng’ombe, mbuzi, kondoo pamoja na nguruwe, kiasi cha Wahiyao kushindwa kufuga mifugo hiyo.

Baada ya vita kumalizika, Wahiyao hawakuweza kurudi tena Msumbiji na badala yake walianzisha makazi yao ya kudumu katika Wilaya hizo. Kutokana na kuishi na makabila mengine katika maeneo yao kumejitokeza kuwa na lahaja mbili za Kihiyao.Kabila la Wahiyao wanaoishi wilayani Masasi wanaishi na makabila ya Wamakonde, Wamwera na Wamakuwa kiasi cha kufanya lugha ya Kihiyao iingiliwe na utamaduni wa lugha hizo.Na wale waishio Tunduru wameingiliwa na makabila ya Wamatengo, Wangoni na Wanyasa wote hao wameathiriwa na lugha za makabila hayo. Hali hiyo imefanya kuwe na tafauti za lahaja.

Jamii ya Wahiyao wanajishughulisha na biashara pia. Wanaendesha biashara ya kubadilishana. Kwa vile wao ni mafundi wa kufinyanga vyungu, basi hutumia fursa hiyo kufanya biashara ya vyungu kwa kubadilishana na mazao ambayo wao hawayalimi kama mpunga na mahindi. Pia wanafanya biashara ya kuvuka mipaka ya Tanzania na kwenda Msumbiji.Wakiwa huko wanakusanya nguo, viatu na mbao kwa ajili ya kuuza kwa jamii yao na jamii nyingine hapa Tanzania.

Wahiyao ni maarufu sana kwa ufugaji wa kuku, bata, ng’ombe, kondoo na mbuzi kama sehemu ya shughuli zao za kibiashara. Biashara kubwa inayotegemewa na jamii hiyo ni zao la biashara la korosho. Ni zao linaloisaidia jamii hiyo kupata pesa zinazowawezesha kuendesha maisha yao ya kila siku ukiachia mbali biashara ndogo ndogo za nafaka.

Sehemu kubwa ya Tanzania ikiwemo Wilaya ya Masasi Mkoa wa Mtwara zina mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kwa vijana waliokaribia utu uzima kwa lengo la kuwaandaa na maisha yao ya kiutu uzima na kuzifanya jamii ziishi kwa kuamini mila hiyo inayojenga uchumi wa jamii yenye mwelekeo sawa wa kimaisha. Mafunzo ya nyimbo za jando na unyago, malengo yake yanafanana kwa kila jamii. Ni kumuondoa kijana katika utoto na kumuanda katika maisha ya kiutu uzima. Maisha ambayo ataweza kumudu wajibati zake kwa familia yake na jamii kwa ujumla kutegemeana na mahitaji ya jamii yake anamoishi.

## 1.2 Usuli wa Tatizo

Kazi za fasihi Simulizi zina tanzu zake ambazo ni ushairi, natiki za Kisasa, semi, methali, ngano, na kadhalika. Fasihi simulizi inatumiwa na jamii kulingana na mila, desturi, elimu na ufundi wa jamii husika. Kila jamii ina mahitaji yake. Elimu ya mafunzo ya nyimbo za jando na unyago ni sehemu ya fasihi simulizi. Ilianza tangu zamani za mababu zetu. Mafunzo yaliwaandaa vijana katika maisha ya kiutu uzima.

Kila kijana aliyekaribia au kufikia utu uzima kwa kubalehe au kuvunja ungo, alipewa elimu hii ili aishi na kutenda kama mtu mzima. Jamii ililenga kutoa elimu hii kwa umri maalum hasa wa utu uzima kwa vijana wa kiume na wa kike kwa kuelewa kuwa vijana hao wamepevuka kiakili na wanaweza kumudu mafunzo watakayopewa na watamudu siri watakayofundishwa wakiwa jandoni au unyagoni.

Mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao wa Lulindi ni muhimu, lakini mafunzo hayo yanalalamikiwa sana na wadau wa elimu na taasisi za

kiraia kuwa yanazorotesha utoaji wa elimu nchini. Madai yao ni kwamba, mafunzo ya jando na unyago yanasababisha utoro wa wanafunzi shuleni, mimba za utotoni na ndoa za mapema pamoja na ongezeko la magonjwa yanayotokana na zinaa kama kaswende, kisonono na ukimwi ambyo yanasababisha vifo vya vijana wadogo na kusababisha kupoteza nguvu kazi ya nchi.

Gazeti la Mwananchi (10-Oktoba-2010) lilieleza kuwa, Mkuu wa Wilaya Ruangwa Mkoani Lindi na Hawa Mchopa, walipiga marufuku sherehe za jando na unyago kwa mwaka 2010, ili kutoa nafasi ya kila mwananchi kushiriki katika mikutano ya kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Raisi na Wabunge. Hiyo ilionyesha wazi kuwa viongozi hao wa serikali na ni wadau wa elimu hawakuona umuhimu wa jando na unyago kuwa ni elimu inayomjenga kijana kulingana na mila za jamii hiyo.

Said (2009) anasema kuwa mafunzo ya jando na unyago yanasababisha mporomoko wa maadili. Na hii inatokea sana baada ya vijana kuhitimu mafunzo hayo. Mporomoko huo wa maadili ya vijana unatokana na mababiliko ya tabia na mwenendo wao vijana siku hadi siku. Hapo zamani vijana wakitoka jandoni na unyagoni walikuwa ni msaada kwa jamii. Vijana waliweza kusaidia kazi ndogo ndogo za jamii kama kilimo, kuteka maji mtoni, kukata kuni, kulea watoto wadogo baada ya mama kwenda shambani kwa shughuli za kilimo au kuvuna. Lakini hali hiyo hivi sasa imepotea. Utafiti umebaini kuwa sababu kubwa ni umri wa vijana wanaokwenda jandoni ni mdogo kiasi hawawezi kufanya kazi hizo. Kushindwa kwao huko kunawafanya vijana hao kuona kuwa hayo ndiyo maisha ya kawaida kwao. Na hiyo inatokana kuwa walishindwa kufundishwa tangu umri wao

ulivyoendelea kubadilika. Kwani Waswahili wanasema *"Samaki mkunje angali mbichi"* kuwa mafunzo ya maisha kwa mtu yanaanzia tangu utoto wa mtoto. Kijana anakua akiwa anaelewa mwelekeo wa maisha ni upi. Anapofikia umri wa utu uzima anapewa elimu ya maisha ya kiutu uzima na ambayo sasa vijana wa jamii ya Lulindi hawapati kikamilifu.

Jicho letu Tanzania (11-07-2011) walipata maoni juu ya umuhimu wa kuwepo kwa mafunzo ya jando na unyago kutoka kwa Dr. Mchimbi wa Wilayani Newala na Dr. Ishengoma wa Wilaya ya Tunduru, kuwa mafunzo hayo ni moja ya changamoto zinazokabili sekta ya elimu kwa wanafunzi. Mimba nyingi za watoto zimetajwa kuwa zinatokana na mila na desturi za unyago na jando ambazo zinafundishwa kuanzia wanafunzi wa shule za msingi.

Karugendo (2009) ameeleza kuwa dini zimekuwa zikipiga vita utamaduni wa jando na unyago. Kwa vile dini hizi ni za kigeni, zilileta utamaduni mpya na kuzika utamaduni wa kiafrika bila kufanya utafiti wa kutosha ili kutoa mabaya na kuacha mazuri. Mtazamo huu unashikiliwa na viongozi wengi wa kidini ambapo wanasisitiza zaidi mafundisho ya dini yanayomjenga mwanajamii katika misingi ya dini zaidi.

Misingi ya dini ikienda sambamba na elimu ya jando na unyago jamii itaimarika.Yote ni mafunzo yanayomjenga kijana katika maadili na mwenendo mwema katika maisha yake. Jamii ya Wahiyao wa Lulindi wanatoa mafunzo yote.

Mitazamo ya wadau hawa, imelenga zaidi kuwa mila ya jando na unyago imeshapitwa na wakati. Ni mila iliyofaa kwa wakati wa zamani. Na kuwa hayo

mambo sasa hayawezekani tena. Watoto hawawezi kuwa wanaacha shule kwa sababu ya mila tu zilizopitwa na wakati.

Utafiti wetu, umechunguza mafunzo ya nyimbo za jando na unyago yanavyomjenga kijana katika kupambana na maisha ya kiutu uzima. Pia tumechunguza sababu zinazolalamikiwa na wadau mbalimbali juu ya mafunzo ya jando na unyago yanayosababisha mporomoko wa maadili kwa jamii. Utafiti umechunguza mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao wa Lulindi. Data zote zimeonyeshwa kwenye jedwali la matokeo.

Mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kwa jamii ni muhimu. Kama yalivyoelezwa na wanajamii ya Lulindi kuwa mafunzo hayo ni moja ya njia ya kumpa kijana njia bora ya kupambana na maisha ya kiutu uzima. Maisha ya kiutu uzima yanahitaji busara. Kwa vile mtu mzima ni kioo cha jamii, basi inategemewa kuwa anayeyapata atakuwa ni mmoja wa viongozi katika jamii.

Elimu ya jando na unyago inatolewa kwa namna tofauti katika kila jamii. Kila jamii ina namna yake ya utoaji wa elimu hii. Hapa Tanzania jamii nyingi zina mafunzo ya jando na unyago. Lakini inatolewa kwa namna tofauti kutegemeana na mahitaji ya jamii yake. Jamii ya watu wa Lulindi wanatoa mafunzo hayo kwa kuwapeleka vijana mahali maalumu pa kutolea elimu hiyo. Wanapelekwa porini mbali kabisa na makazi ya watu ambako hutengenezewa makazi ya muda ya kuishi.

Wembah (1975) ameandika kuwa vijana wakiwa jandoni na unyagoni ngoma za aina mbalimbali zinachezwa zenye lengo la kuwaasa wari na kuwapa burudani ili kuwasahaulisha na maisha ya nyumbani. Ngoma za kunengua huchezwa wakati huo.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Ni mitazamo ya wadau wa elimu na taasisi za kiraia juu ya mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kuwa nyimbo hizo hazina manufaa yoyote kutumiwa na jamii na ni chanzo cha mmomonyoko wa maadili katika jamii ya Wahiyao wa Lulindi. Utafiti umechunguza ubora na udhaifu unaojitokeza katika fasihi hiyo simulizi kwa jamii.

Utafiti unaeleza kuwa mafunzo ya nyimbo za jando na unyago yalilenga kumwandaa kijana katika maisha ya utu uzima. Kinyume na matarajio ya jamii, tatizo linaelezwa kuwa linajitokeza katika uendeshaji wa mafunzo hayo. Hapo awali mafunzo yalitolewa kwa vijana wa umri mkubwa wa kuanzia miaka 9 hadi 12. Vijana waliotarajiwa kubalehe au kuvunja ungo au wameshakuwa, ambao walielewa mafunzo ya kiutu uzima.

Mafunzo hayo yaliwafaa kwa vile tayari walikuwa na umri wa kupevuka. Umri ambao kijana anauwezo wa kuchambua mazuri na mabaya katika maisha yake. Na anaweza kuoa au kuolewa na kuweza kutunza familia yake.

Utafiti unatueleza kuwa mafunzo hayo hivi sasa yanatolewa bila kuzingatia umri wa vijana. Wazazi wanawapeleka vijana wao jandoni na unyagoni pale tu wanapojisikia kuwa wana uwezo kwa mwaka huo wa kufanya sherehe za jando na unyago kwa kijana wake bila kujali baada ya kuhitimu atakuwa na mwelekeo gani wa maisha baada ya kupata elimu hiyo. Abdallah (1993) katika *The Yaos-Chikala cha Wayao,* anafafanua kwa kusema kuwa: “Unyago nga janguya, kwaina achalume achamuno achimbumba, mpaka aiche usongolo wambone, ne wisichana wambone”.

## 1.4 Tarjima

"Unyago wakati wa zamani haukuharakishwa. Kuwaingiza vijana wa kiume jandoni ni mpaka wafikie umri mzuri, na wasichana mpaka usicha mzuri."

Kinyume na mafunzo yanayotolewa sasa, jamii inawapeleka vijana jandoni na unyagoni wakiwa na umri mdogo wa miaka 2 hadi 5. Mafunzo yanayotolewa ni yale ya kiutu uzima. Kutokana na umri wao kuwa mdogo, wanashindwa kutunza siri ya nyimbo za jando na unyago na kujaribu kutenda kile kilicho cha siri.

Nyimbo za jando na unyago ni siri ya kiutu uzima. Anayeipata anatakiwa kuwa msiri wa kile alichojifunza ili aweze kukitumia katika utu uzima wake. Moja ya mambo wanayofundishwa ni pamoja na heshima, utii na malezi. Ni mafunzo ya utu uzima yanayomjenga mtu mzima katika maisha mema na jamii.

Utafiti huu unaeleza kuwa kutokana na vijana kukosa mafunzo kikamilifu, tabia na mwenendo wao unapotoka na kwenda kinyume na matarajio ya jamii. Mafunzo hayo yanamjenga kuwa bora katika jamii. Kwa vile vijana ni wadogo wanashindwa kupokea maarifa hayo kikamilifu. Kutokana na vijana kukosa elimu hiyo kikamilifu hata maadili na miiko ya jamii wanaikosa. Matokeo yake vijana wanaishi kwa kufuata misimamo yao ambayo haina miiko ya jamii. Matokeo yake ni vijana kupoteza mwelekeo wa maisha bora. Vijana hawana heshima, wavivu, hawana woga wa kutenda jambo lolote.

Vijana wakiwa jandoni na unyagoni wanafundishwa ukakamavu, uvumilivu, kazi, heshima, utii na malezi ya familia. Haya ni mafunzo ya kiutu uzima, ya kumuandaa kijana maisha ya kiutu uzima. Mafunzo haya hivi sasa hayafundishwi kikamilifu. Na

kile wanachofundishwa hawakitilii maanani na badala yake wanafanya majaribio ya yale waliyofundishwa kama kinyume na siri ya jando na unyago.

Hapo awali, kabla ya kuwapeleka vijana jandoni na unyagoni, kulikuwa na maandalizi yaliyokuwa yanafanyika. Wazazi walikaa pamoja na kukubaliana muda wa kupeleka vijana jandoni na unyagoni. Waliwajadili vijana waliotarajiwa kama walikubalika. Sababu ya kufanya hivyo ni kutokana na siri iliyokuwepo jandoni na unyagoni. Waliona kuwa haimstahili kijana mdogo.

Pia walikubaliana taratibu za uendeshaji wake kama, kukusanya vyakula vitakavyoliwa na vijana na warombo wakiwa jandoni. Chakula kilicholiwa jandoni na unyagoni kilikuwa ni cha aina moja kwa wote. Wazazi walikusanya mbaazi, kunde, choroko mtama na mahindi kiasi kilichotosha kwa matumizi ya muda wote wa mafunzo hayo. Taratibu hizo zilisaidia kuwaweka vijana kuwa jamii moja isiyo na tofauti kimaisha. Wazazi walipewa muda wa kujiandaa. Kinyume na taratibu za sasa. Kila mzazi anawajibika mwenyewe kumtunza kijana wake akiwa jandoni au unyagoni. Hali hiyo haiwajengi vijana katika umoja kama jamii ya Wahiyao wanavyohitaji.

Elimu ya nyimbo za jando na unyago inahitaji siri kubwa kwa anayeipata. Na ili iwe siri anayepewa ni lazima awe amepevuka kiakili na kimwili. Lakini elimu hiyo inaelekea kupotea mwelekeo wake kutokana na kupeleka mafunzoni vijana wadogo ambao hawawezi kumudu kuwa na siri. Hatima yake, wafundishwao haiwajengi akilini kama ilivyokusudiwa na jamii.

Matokeo ya kutojengeka huko ni kuelekea kupotea kwa mila hiyo. Kwa vile mafunzo hayo hawajayapati kikamilifu, vijana wengi wanaonekana kukosa maadili mema. Vijana hawana heshima, wavivu, wakaidi na hawathamini wazee kwa kujiona kama wao si miongoni mwa wanajamii. Hawawezi kuonywa na wazee kwa matendo maovu wanayoyafanya.

Kutolewa kwa elimu hiyo kwa vijina wadogo, kunawafanya vijana hao kushindwa kumudu maisha ya ki utu uzima. Wanategemea zaidi kuendeshewa maisha na wazazi wao. Hali hiyo inawafanya vijana wengi wa Kihiyao kuonekana kukata tamaa, na hivyo kufikiria kuwa maisha bora yako mijini na hivyo kukimbilia huko kutafuta maisha bora kumbe wanakutana na bora maisha. Na wengine kuishia kunywa pombe aina ya gongo ambayo inaathiri afya zao kwa kudhohofika na kushindwa kufanya kazi za kilimo zitakazowasaidia kupata chakula na kuinua kipato chao kwa kuuza mazao yao.

## 1.5 Madhumuni ya Utafiti

1.5.1 Kuchunguza matatizo linalojitokeza kutokana na elimu ya nyimbo za jando na unyago linalolenga kujenga na kuimarisha maisha yenye maadili kwa jamii.

1.5.2 Kuchunguza jinsi gani elimu ya nyimbo za jando na unyago inavyosaidia kurekebisha maisha ya jamii.

1.5.3 Kutafuta njia au mbinu ya kushawishi uimarishaji na ushawishi wa nyimbo za jando na unyago. Maswali ya utafiti ni:

(i) Ni tatizo lipi linajitokeza kutokana na mafunzo ya jando na unyago?

(ii) Je, mafunzo ya jando na unyago yana manufaa yoyote kwa maisha ya jamii ya leo ya Wahiyao wa Lulindi Masasi?

(iii) Ni njia au mbinu zipi zinatumika kushawishi uimarishaji na ustawishaji wa nyimbo za jando na unyago?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu ni muhimu kwa jamii ya Wahiyao wa Lulindi Masasi, kwa matarajio kwamba itawasaidia kufahamu makosa ya utovu wa maadili kwa jamii na namna ya kuyakabili na kuyarekebisha.

Utafiti umechunguza umuhimu wa nyimbo za jando na za unyago. Nyimbo hizo zinawafundisha vijana wajibati zao pindi watakapokuwa watu wazima. Zinafundisha utamaduni wa jamii yao na umuhimu wa kujua na kuitumia mila yao ya kihiyao. Utafiti umesaidia kujua ubora na udhaifu wa nyimbo za jando na za unyago ambao umefafanuliwa katika jedwali la ukusanyaji wa data.

Fasihi simulizi inajumuisha Sanaa inayotumia lugha ya mazungumzo. Ni chombo kinachomlinda na kumwelimisha mwanajamii katika maisha yake. Fasihi simulizi inatumiwa na jamii kulingana na mila na desturi zao. Kila jamii ina mahitaji yake. Utafiti huu umejihusisha na ushairi simulizi wa jamii ya Wahiyao. Umechunguza mafunzo yaliyomo katika nyimbo za jando na unyago. Nyimbo za jando na unyago za kabila la Wahiyao hazijapata mtafiti aliyewahi kufanya utafiti juu ya udhaifu au ubora wa nyimbo hizo. Hivyo utafiti huu umechunguza ubora na udhaifu unaojitokeza.

Umuhimu wa nyimbo za jando kwa jamii ya Wahiyao ni kuwaandaa vijana kuwa walezi bora wa familia zao hapo baadaye. Zinafundisha kazi, heshima na kuishi kwa kusaidiana na kupendana katika jamii. Nyimbo za jando na Unyago zinawafanya vijana kuwa mashujaa katika kupambana na maadui wa jamii yao.

Mtafiti amefanya hojaji kwa vijana hamsini (50) wa kiume na wa kike hamsini (50) kufanya jumla ya hojaji mia moja (100) kujua kama kuna umuhimu wa nyimbo za jando na unyago. Majibu ya hojaji hizi yameonyeshwa kwenye majedwali ya ukusanyaji wa data.

# SURA YA PILI

# 2.0 KAZI TANGULIZI

## 2.1 Utangulizi

Nyimbo ni sanaa ambayo hutoa ujumbe kwa njia ya kuimba. Nyimbo hutumia lugha teule na fupi na ambayo huimbwa kwa sauti maalumu. Nyimbo zina sifa zinazoambatana nazo kama:

(i) Nyimbo hutumia kiimbo au sauti maalumu

(ii) Zinaambatana na ala za muziki

(iii) Huimbwa na mtu mmoja au na watu wengi; wakati mwingine nyimbo huimbwa kwa kupokezana.

(iv) Hutumia lugha ya mkato

(v) Hurudiarudia maneno ili kusisitiza ujumbe

Kobia (2006) anasema nyimbo zinaburudisha jamii baada ya kazi za mchana kutwa, zinaelimisha, zinafunza, zinaonya na kuelekeza. Nyimbo pia zinariwadha, kusifia jambo zuri linapotendwa na wanajamii. Nyimbo zinaunganisha jamii, kudumisha au kuhifadhi utamaduni wa jamii, kukuza talanta, na sanaa katika jamii na hutumika katika mbinu nyingine za fasihi kama vile hadithi.

Taban (1972) anaeleza kuwa nyimbo zinatumika kumliwaza mtu mwenye kupatwa na matatizo au huzuni. Kwa mfano kama binti amepatwa na uja uzito kwa mara ya kwanza,kwa kawaida huwa anapatwa na huzuni kwa vile haelewi nini kitatokea kadri mimba inavyokuwa. Kwa jamii ya Wahiyao wa Lulindi, wanatumia fasihi simulizi ya nyimbo kumpa elimu binti juu ya malezi ya ujauzito wake na anafundishwa dalili

mbalimbali za maendeleo ya hali yake. Bi Zainabu Mkumbila alieleza kuwa, nyimbo hizo za unyago zinamuaanda binti kwa malezi ya mtoto wake kuanzia mimba hadi mtoto kuzaliwa. Nyimbo hizo zinaitwa nyimbo za litivo.

Mulokozi (1999) anaeleza kuwa, nyimbo zinasawiri migongano ya mifumo ya jamii. Tofauti ya maisha ya watu inafanya kuwepo kwa migongano inayosababisha kuishi kwa woga na kutoaminiana. Wataalamu mbalimbali wamejaribu kueleza maana na dhima ya nyimbo za jando na unyago maishani. Sengo (1978) amedokeza, "Nadharia ya kiafrika itajengeka na kudhihirika baada ya uchunguzi mkubwa wa kifasihi simulizi, ambamo ndimo mlimo na kunga na siri kuu za nadharia zetu. Nyimbo za jando na unyago hutolewa kwa lengo la kuelimisha jamii. Ni vigumu kulifuta suala hili katika jamii zetu.

Manufaa yanayopatikana jandoni na unyagoni hujenga jamii yenye mwelekeo. Sengo amesema pia kwamba kwake yeye, kumdondoa Maganga, Mazengo, au Semindu, huwa ni fakhari kubwa zaidi kuliko kumdondoa Mao, Marx na Lenin. Hapa Sengo anazidi kusisitiza kuwa Fasihi simulizi ya kiafrika ni muhimu sana kwetu kuliko kufuata fasihi ya kizungu (kigeni). Anasisitiza kwa kusema kuwa fasihi hiyo ndiyo itakayomsaidia Mtanzania (Mwaafrika) kujikomboa kutokana na utumwa wa kutawaliwa kimwili na kifikra.

Njiru (1981) anasema kuna uhusiano kati ya fasihi simulizi na amali za jamii. Fasihi simulizi inawafundisha jamii kujua amali za jamii yake na kuzitumia kama zilivyokusudiwa. Amali za jamii kama utamaduni, mila na desturi za jamii hiyo. Nyimbo kama tanzu ya fasihi simulizi, zinaelezea utamaduni, mila na desturi za jamii.

Bukenya (1994) ameandika kuwa fasihi simulizi ni sehemu ya masimulizi ya utamaduni wa jamii inaelezea ukweli wa maisha ya jamii, utamaduni, ufundi, nyimbo, mila na amali zake. Kwa hiyo kuna mahusiano ya moja kwa moja baina ya fasihi simulizi na maisha ya jamii. Nyimbo za jando na unyago zinatumika kufundisha vijana maisha ya kweli ya jamii. Baadhi ya jamii, wazee ndiyo walimu wa mafunzo bora ya jamii.

Jan (1985) anasema kuwa fasihi simulizi huelezea maisha ya jamii husika kulingana na wakati. Kila wakati wa maisha ya jamii, una matukio yake yanayojitokeza, ambayo jamii haina budi kuyachambua na kuyaelezea kwa jamii kwa kuangalia manufaa kwa jamii yake. Kila linalojitokeza kwa jamii ya wahiyao, linaelezwa katika nyimbo zake za jando na unyago kama sehemu ya Chuo cha kutolea mafunzo yake kwa jamii.

Okpewho (1992) anadokeza kwa kusema kuwa, katika jamii yao fasihi simulizi ni ubunifu ambao unatokana na hisia ya mambo yanayotokea katika jamii. Matendo hayo siyo matukio yanayoandikwa magazetini, redioni, wala matukio ya kihistoria. Mafunzo ya jando na unyago ni masimulizi ya matukio yanayotokea katika jamii ya kila siku. Nyimbo za jando na unyago zinaakisi maisha ya kila siku ya jamii yake. Yanaweza kuwa matukio ya kubuni au ambayo yamewahi kutoke au yanaweza kutokea katika maisha ya kawaida ya jamii yao.

Hoopes (1979) anaongeza kwa kusema kuwa masimulizi ya kihistoria yanatokana na mazungumzo ya mtu binafsi, juu ya maisha yake, watu wanaomzunguka na matukio yanayotokea. Kila jamii ina historia ya maisha yake. Historia hiyo ndiyo inayoifanya

jamii ya Wahiyao wa Lulindi kurithisha kizazi chao. Suala la jando na unyago lilianza tangu zamani. Wahiyao wameendelea kutoa elimu ya jadi kwa jamii yake ili kukuza na kuendeleza utamaduni wake.

TUKI (1989) imetaja kuwa hapa Tanzania kuna nyimbo za aina nyingi ziimbwazo katika shughuli mbalimbali, zikiwamo nyimbo za watoto, kazi, jando, unyago, vita, kuaga mwaka, nyimbo za mawaidha, uvuvi, sherehe na kubembelezea watoto. Uchunguzi wetu, umetupa data kamili ya aina ya nyimbo kutokana na zile zilizokusanywa jandoni na unyagoni.

Nyimbo huimbwa kwa ajili ya mahitaji ya jamii. Kama jamii ya Wahiyao wa Lulindi pamoja na kuwa na nyimbo za jando na unyago, wana nyimbo za kuchapusha kazi, za kuomboleza msiba, kubembeleza watoto nakadhalika.

Nyimbo za jando na unyago zina mtindo, mahadhi, na namna ya uimbaji wa aina yake. Uimbaji wa nyimbo za jando na unyago ni ule unaosisitiza kuelimisha jamii kama ilivyokusudiwa.

Nyimbo za jando na unyago zinaadabisha, zinaonya, na zinatoa maadili kwa vijana wanaopitia jandoni na unyagoni, kwa lengo la kuwatoa utotoni na kuwaelekeza maisha ya kiutu uzima. Nyimbo za jando na unyago zimeandaliwa kwa malengo kama njia pekee ya kijadi ya kutolea elimu ya jadi ambayo ndiyo inakuza kijana na maisha ya jamii yake.

Senkoro (1982) amefafanua ushairi kuwa “Ushairi ni utanzu wa fasihi unaotumia mpangilio wa lugha ya mkato, ya kipicha na yenye mapigo katika kutowa maudhui

yake” Nyimbo za jando na unyago hutumia lugha maalumu iliyojaa picha, ishara na taswira. Ukweli wa hili mtafiti ameupata wakati wa utafiti baada ya kukusanya nyimbo za jando na unyago kuzichambua kulingana na vigezo vinavyokubalika Kitaalimu kama inavyoonyeshwa kwenye uchambuzi wa data.

Bernth na Ulla (wahariri) (1976) wamefafanua kuwa ushairi ni hisi za kubuni za mambo ya kweli yanayotumikia katika jamii. Yana dhahania maalum au mpango maalum. Katika utafiti wetu tumekusanya ushairi wa nyimbo za jando na unyago na kuchunguza hisi zinazojitokeza katika nyimbo hizo na hisi hizo zinavyoshabihiana na maisha ya jamii.

Wanaufafanua ushairi kuwa unajumuisha mpangilio wa vina na mizani kwa kufuata utoshelevu na kuleta maana, matamshi sahihi, sauti sahihi muundo na mvuto wa mistari ya ushairi. Katika nyimbo za jando na unyago, zina mpangilio mzuri wa sauti yenye muundo sahihi wa lugha, matamshi yake ni sahihi na ambayo yanaleta maana na mvuto ingawa lugha yake ni ya mafumbo.

Ulli na Beier (1967) amesema nyimbo za ngoma za jando na unyago hutumika kutoa mafunzo kuhusu mambo mbalimbali katika maisha. Shughuli za jando na unyago lazima ziendeshwe kwa utaratibu na umakinifu ili kujenga jamii yenye mwelekeo. Wazo la Taifa la kukuza fasihi ya Tanzania kwa Kiswahili na kuendeleza kwa ubora wa pekee, fasihi ya Waswahili –Wapwani wake ni uswahilini; ni la Sengo (2009) ambaye hilo ndilo amesema ni wazo linalojenga, kukuza na kuendeleza utamaduni, mila na desturi za Tanzania.

Kutokana na fasihi simulizi, jamii zimeweza kufichua maovu yanayojitokeza miongoni mwa jamii na kuweza kurekebisha maovu hayo. Nyimbo za jando na unyago zina kazi ya kuwafunza vijana maisha ya utu uzima. Zinaelezea ubora wa mtu katika maisha kwa jamii. Zinahimiza watu katika jamii kuishi kwa kuzingatia miiko ya jamii.

Wembah (1975) anaeleza kuwa jamii ya Wahiyao wana nyimbo zinazoimbwa jandoni katika kuwarithisha vijana utamaduni, mila na desturi za Kihiyao. Nyimbo hizo zinaimbwa na wazee waliopewa jukumu na Mwenye (kiongozi mkuu aliye na busara katika ukoo) la kuwafundisha vijana. Kwa kufanya hivyo kunasaidia kurithisha kizazi hadi kizazi na kuwafanya vijana waishi wakiwa wanajua mila, desturi na utamaduni wao.

Ngugi (1990) anaeleza kwa kusema kuwa jando na unyago katika jamii yake ni fasihi inayomjenga mwanajamii. Jamii yenye utamaduni wa kuwapeleka vijana jandoni na unyagoni inaaminika kuwa ni jamii yenye mwelekeo bora katika maisha. Jamii lazima itakuwa na heshima na utii.

Pia itaimarika kimaadili. Kutompeleka jandoni kijana, ni sawa na kumlea kijana huyo kama mdudu ambaye hana umuhimu wa mafunzo zaidi ya uwezo wa kutafuta chakula ale ashibe aweze kuishi. Anakemea jamii isiyokwenda jandoni kwenda kuoa jamii iliyokwenda jando na unyago. Lazima jamii hizo ziwe tofauti kimaadili. Utofauti huo unaweza kusababisha jamii kupoteza mwelekeo wa maisha yake, na pia kuweza kupoteza utamaduni, mila na desturi za jamii yake.

Taban (1972) anafafanua umuhimu wa kijana kupelekwa jandoni kutahiriwa pindi anapofikia karibu na utu uzima kwa lengo la kumuandaa katika maisha ya kiutu uzima. Kutotahiriwa hadi anapofikia umri wa utu uzima, jamii inamtenga na kumuona kuwa hana akili timamu. Jandoni kijana anafundishwa uwezo wa kumiliki familia yake pamoja na mali zake.

Wembah (1975) anaeleza kuwa jando na unyago ni Chuo cha kutolea mafunzo ya kiutu uzima yanayomtoa kijana utotoni na kumuandaa maisha ya kiutu uzima. Mafunzo yanamuandaa kijana kuweza kujitegemea na kumudu maisha ya kiutu uzima bila kutegemea mtu mwingine. Mafunzo hayo yanatolewa na watu wazima waliopitia jando na unyago. Nyimbo na masimulizi ya mambo mbalimbali ya jamii zinatumika katika utoaji wa mafunzo hayo. Nyimbo zinazoimbwa jandoni na unyagoni ni siri kubwa.

Samora (1977) amesema, ni lazima tufahamu kuwa, ujinga wa mtu mmoja ni udhaifu wa jamii nzima na ujinga huo huathiri kazi ya kila mmoja wetu. Kwa hiyo jando na unyago ni sehemu ya fasihi simulizi ambayo nyimbo zake zina nafasi ya kutoa elimu kwa jamii ili kuondokana na ujinga uliyopo ili kuifanya jamii hiyo kuwa na mwelekeo mzuri na kuzingatia maadili mema.

Nyimbo za jando na unyago zinamtoa kijana katika utoto na kuwa mtu mzima. Mafuzo yanayotolewa ni ya kumuandaa kijana kuweza kuyamudu maisha ya kiutu uzima, yanamfunza kuweza kujitegemea badala ya kutegemea watu wengine. Kila mmoja katika jamii ya Wahiyao lazima aipitie mila hiyo, muda na wakati ukifika.

Minduva (2004) katika Sahil (2000) ameandika kuwa mtu anapata mahitaji yake kutoka katika mazingira yanayomzunguka. Kwa maelezo hayo, kila jamii ina fasihi yake kulingana na mahitaji ya jamii hiyo. Kuifuja fasihi simulizi ya jamii ni sawa na kutia ukame wa maadili kwa jamii hiyo. Jamii bila ya maadili huwa hasi zaidi ya jamii ya wanyama na wadudu.

Okpewho (1992) anaeleza kwa kusema kuwa, jamii zinatofautiana katika utamaduni. Kila jamii ina namna yake ya kuishi kutegemeana na asili na utamaduni wake. Jamii ya Wahiyao wana mahitaji ya vijana wao kuwapeleka jandoni na unyagoni kwa lengo la kuwa na namna moja ya kuishi, kuwa na jamii yenye mahitaji sawa na mwelekeo unaofanana kimaisha. Ni elimu iliyorithishwa tangu zamani. Kwao Wahiyao ni elimu inayoendelezwa hadi sasa.

Nkwera (1978) amesema, maudhui ya nyimbo hutegemea hadhira inayolengwa. Hadhira ya nyimbo za jando na unyago ni vijana waliolengwa kupatiwa elimu ya chuo hicho. Kutokana na utafiti tulioufanya tumejifunza kuwa jamii ya Wahiyao wanatoa elimu ya nyimbo za jando na unyago kwa makundi mawili tofauti ya vijana. Kundi la kwanza ni lile la vijana ambao hawajavunja ungo na hawajabalehe. Kundi lingine ni la vijana ambao wamevunja ungo na kubalehe. Utafiti umetueleza kuwa vijana wasiobalehe na kuvunja ungo ni wale wanaopelekwa jandoni kutahiriwa kwa wanaume na unyagoni kwa vijana wa kike ambao hupelekwa kufundwa kwa lengo la kuwaondoa maisha ya utotoni na kuingizwa katika utu uzima. Hawa huimbiwa nyimbo zinazowaelekeza maisha ya utu uzima yanavyokuwa. Kila wimbo unaoimbwa una tafsiri yake, maana yake na ujumbe wake maalum. Nia ya kila

wimbo ni kumjenga kijana awe na maisha bora, aenende kama jamii inavyohitaji. Nyimbo zote zinaimbwa kwa lugha ya Kihiyao.

## 2.2 Maana ya Ushairi wa Nyimbo

Inapoelezwa maana ya nyimbo hatuwezi kukwepa kugusa ushairi. Wataalamu waliofafanua ushairi wameuhusisha na nyimbo. TUKI (1987) inafafanua kuwa ushairi hujumuisha nyimbo. Nyimbo ni moja ya tanzu muhimu katika ushairi. Inatoa maana ya nyimbo kuwa ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mapigo na muwala. Nyimbo huweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi cha watu wengi. Mtu mmoja anaanzisha na wengine huitikia.

Miruka (2001) anasema, ushairi (nyimbo) ni maneno yanayoelezea hisia za binadamu, fikra na mawazo yaliyo pangwa kwa mpango maalum uitwao beti Kimantiki, vielezea vya nyimbo haviwezi kumalizia kwenye mpangilio mzuri wa maneno tu. Bali nyimbo ni sanaa ya lugha, lazima maneno yanapoelezea hizo hisia na fikra, yawe mateule yaliyofinyangwa na kusukwa kwa nidhamu na mvuto unaopendezesha mwimbaji na kumvutia msikilizaji.

Nyimbo zina umuhimu mkubwa kwa maisha ya jamii na huambatana na matukio mbalimbali kama vile sherehe za jando na unyago, harusi na mikutano ya siasa kulingana na mahitaji ya tukiyo. Kitu muhimu ni kwamba lazima nyimbo iwe na ujumbe unaolenga jamii husika. Austin (1968) anaeleza kuwa nyimbo zinaimbwa kwa lengo la kuelezea jambo linalomkera mtu miongoni mwa jamii yake. Kwa kufanya hivyo jamii inatambua ilipo na jukumu lake kama mwanajamii.

Kipury (2002) anasema kwamba kwa hali yoyote iwayo, nyimbo haiwezi kuepuka kuelezea falsafa ya maisha ya watu wajamii inayohusika, imani, silka, na desturi zao. Maelezo haya yanatupa ukweli kwamba nyimbo si ya mwimbaji pekee bali ni ya jamii nzima. Kinacho imbwa ni lazima kitokane na kikubalike na jamii kwa sababu nyimbo zinaangalia maendeleo ya maisha ya jamii. Gerard. A.S (1971) anasema kuwa kutokana na ushairi unaweza kumkomboa mwanajamii kutokana na utumwa wa kutawaliwa unaofifisha utamaduni, mila na desturi za jamii. Kama ushairi utajali utamaduni wa jamii husika, basi utakomboa jamii hiyo.

Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa (1988) imeeleza maana ya nyimbo kuwa ni tungo za kishairi zenye kutumia mahadhi, melodia, mapigo, muwala. TUKI (1987) imehusisha ushairi kuwa ni fungu linalojumuisha tungo zote za fasihi simulizi zenye kutumia mapigo kwa utaratibu maalumu. Hamadi na wenzake (1972) ameeleza kuwa nyimbo ni mashairi mafupi ambayo hujitokeza katika sehemu nyingi za jamii. Nyimbo inaweza kuwa na ubeti mmoja au zaidi. Kwa hiyo nyimbo zinafuata tungo za kishairi.

Nyimbo huweza kuimbwa na kuchezwa kwa kutumia muziki au kipekee. Zipo nyimbo za aina nyingi. Katika jamii kutegemeana na matukio. Wahiyao wa Lulindi wana nyimbo za jando na unyago. Huimbwa na mtu mmoja na wengine wakiitikia na wakati mwingine wakicheza. Wahiyao wana nyimbo za ngoma ya unyagoni ziitwazo "**Ndindi**" Wembah (1975) ameeleza maana ya "**Ndindi"** kuwa ni nyimbo za ngoma za unyago anazofundishwa kijana wajibati zake katika kuandaa chakula cha ndoa atakapoolewa. Anafundishwa tofauti ya majukumu kati yake na mwanaume na

majukumu yake kama mwanamke kwa mume wake. Pia binti anafundishwa malezi ya familia yake pindi awapo na familia. Dada wa mwenye anapewa jukumu la kuwafundisha vijana katika ukoo wake akishirikiana na wanawake wazee walioteuliwa kwa kusaidia kazi ya kufundisha.

Ni nyimbo za ngoma ya kumfundisha msichana kuwa mke bora ndani mwao ili kumfurahisha mume wake wakati wa chakula cha ndoa. Si chombo cha starehe bali ni starehe ya ndoa kwa mume na mke. Nyimbo hizo huambatana na upigaji wa ngoma. Ngoma hiyo huchezwa porini na baadaye wakishajua kuicheza mabinti huchezeshwa hadharani wakiwa wamezungukwa na wake kwa wanaume, kushuhudia kama wari wameiva, tayari kwa kuposwa na kuolewa. Nyimbo zinaweza kuwa na ubeti mmoja au zaidi.

Mambo muhimu yanayotambulisha nyimbo ni kuwepo kwa muziki wa sauti ya mwimbaji, muziki wa ala, maneno yanayoimbwa, hadhira inayoimbiwa na muktadha unaofungamana na wimbo huo. Nyimbo ni sanaa yenye dhima kubwa katika jamii za kiafrika. Nyimbo huburudisha wakati wa mapumziko, huonya, hufunza huomboleza hubembeleza mtoto ili alale, huhimiza kazi, pia hutia hamasa.

Nyimbo za unyago kwa Wahiyao wanaziita “chiputu” na za Jando “Lupanda”. Nyimbo hizi huimbwa jandoni na unyagoni vijana wakiwa porini sehemu ya makazi yao ya mafunzu. Nyimbo hizo hukusudiwa kuwaasa wari kuhusu wajibati zao za kiutu uzima baada ya kuhitimu jando au unyago. Katika Lupanda ilijengwa nyumba ya nyasi kubwa na kuwekwa vijana wa kiume. Ndani kuliwashwa moto mkubwa na kucheza ngoma inayoitwa masanje (madange). Ndani ya michezo hiyo vijana

walifundishwa mambo mengi kama yakutunza mke na watoto, namna ya kupata watoto, na michezo hiyo iliambatana na mafunzo ya ushujaa na kazi mbalimbali.

Msokile (1992) ameeleza kuwa nyimbo za jando na unyago huimbwa kwa mafumbo na huimbwa kwa lengo la kutoa mafunzo kwa jamii. Kinachoimbwa lazima kitoke miongoni mwa jamii. Ndani ya jamii kuna mambo mengi yanayotendeka. Nyimbo za jando na unyago zinaimbwa na jamii ili kuhimiza mwenendo bora unaojenga maisha yenye amani na yenye kuleta maendeleo. Mara zote nyimbo hizo hukemea na kufunza wanawari.

Nkwera (1978) anafafanua nyimbo ni kipengele muhimu cha ushairi katika fasihi simulizi. Ushairi na nyimbo za makabila mbalimbali umeshika mafundisho ya hekima na malezi ya busara ya wahenga. Ni mafunzo ya maisha mazima ya mtu. Kila kipindi cha maisha ya mtu kina maelekezo yake na nyimbo zake. Kwa mfano mtoto kuzaliwa, mvulana kubalehe, msichana kuvunja ungo, kuowa au kuolewa, sherehe mtu kujinusurisha na majanga kama vile ya Ukimwi nakadharika. Kulingana na hatua hizo za maisha kuna nyimbo za jando na, harusi vita matanga na vilio, matambiko na kadhalika.

Holt na wenzake (2001) wanaeleza kuwa nyimbo za ushairi zinafundisha watoto licha ya kubembeleza. Mama anaimba kwa lengo la kumuelekeza mtoto wake maisha ya baadae atakapokuwa mtu mzima. Anafundishwa pia wajibati yake katika maisha yake ya baadae, anaelekezwa kuwa atakuwa baba, mama na atategemewa na jamii. Jamii ya Wahiyao pia wana nyimbo za kubembeleza watoto. Nyimbo hizo

zinawafundisha vijana maisha ya malezi ya familia yake atakapokuwa mtu mzima. Nyimbo hizo zinafundisha kazi, heshima na maadili mengine.

Nyimbo za jando na unyago zinaimbwa kutegemeana na wakati na mazingira ya wakati husika. Hii inatokana kuwa kila kipindi cha maisha ya mtu kina maelekezo yake. Kwa nyimbo za jando na unyago za Wahiyao, utafiti umeeleza kuwa zinaimbwa kutegemeana na umri wa kijana na wakati wake wa kupata mafunzo hayo. Nyimbo zinafunda kutegemea mahitaji ya wakati huo kama nyimbo za kijana kubalehe au kuvunja ungo zinafundisha zaidi kijana kuwa msafi, kuwa na heshima na kuwa mlezi wa familia, kuna nyimbo zinazoimbwa kwa binti anapokuwa mjamzito. Hizi zinamuandaa binti kuwa mlezi na anafundishwa namna ya kujisaidia mwenyewe kama atapata tatizo akiwa peke yake na namna atakavyoweza kujisaidia.

Ndungo na mwenzake (1993) wamesema, nyimbo ni utanzu wa ushairi simulizi wenye maudhuwi ya kutoa mafundisho ya hekima, malezi na busara za wahenga. Katika nyimbo za jando na unyago za Wahiyao utafiti unaeleza kwamba zilianza kuimbwa tangu zamani na Wahenga katika kuwaandaa vijana wao kupambana na maisha ya kiutu uzima. Nyimbo hizo zimerithishwa kutoka kwa mababu. Mabadiliko ya wakati na mazingira hayaathiri uimbaji wa nyimbo hizo katika utoaji wa mafunzo yake. Kinachoweza kubadilika ni namna ya uwasilishaji wa ujumbe wake. Hekima, busara na malezi katika jamii ni jambo linalokuza na kujenga jamii bora yenye mwelekeo wa maisha bora.

Mulokozi (1996) ameandika kuwa nyimbo ni kile kinachoimbwa. Ameangalia nyimbo kwa ujumla, kwa kutoa maana ya juu juu. Kwa hiyo tunajifunza kuwa kila

kinachoimbwa ni nyimbo hata kama hakina mpangilio. Yeye hajaangalia ushairi na kanuni za mashairi. Au hakuzingatia mpangilio maalumu wa mashairi. Nyimbo ni lazima zifuate maadili ya jamii husika. Na hivyo nyimbo za jando na unyago ni lazima zifuate maadili ya jamii yenye jando na unyago.

Kipury (2000) anafafanua kuwa nyimbo lazima zitumike kuichambua na kuelezea falsafa ya maisha ya jamii ya watu husika, utamaduni na historia ya maendeleo ya jamii hiyo. Maelezo haya yanatuthibitishia kwamba nyimbo ni zao la jamii nzima na si mali ya mtu mmoja. Vilevile nyimbo za jando na unyago si mali ya vijana wanaoandaliwa katika maisha ya ki u-tu uzima, bali hata mzee inamuhusu kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, kama mzee hakupata mafunzo ya jando na unyago kisawasawa tangu umri wa ujana, basi anaweza kupata hata akiwa mzee. Lengo la fasihi simulizi ni kuifundisha jamii pale inapokwenda kinyume na matakwa ya jamii yake. Mwenye kuipata anategemewa kuijenga jamii yenye historia bora.

Fasihi simulizi katika jamii ya wahiyao ilianza tangu zamani. Ilitolewa kwa vijana wadogo kwa kuwafundisha miiko fulani kwa njia ya hadithi pamoja na nyimbo. Nyimbo ziliibwa zikiwa zinaelezea matukio yaliyowahi kutokea katika jamii yao na yale ambayo yangewahi kutokea hapo baadaye. Nyimbo mara nyingi hutolewa kwa nia ya kuendeleza mafundisho, hekima na malezi ya vijana. Ni mafunzo ya maisha mema. Nyimbo huimbwa kwa malengo maalum. Zipo nyimbo za kuzaliwa mtoto, mvulana kubalekhe, na msichana kuvunja ungo, za harusi,za mazishi,za kuomboleza na za mapenzi. Nyimbo hizo zinaimbwa kutegemeana na muktadha. Utanzu huu unatumika sana na jamii ya Wahiyao katika kuelimisha jamii. Awapo katika

mafunzo ya kubalehe au kuvunja ungo ,kijana anafundishwa usafi wa mwili, mavazi, pamoja na kufundishwa kuwa kuvunja ungo ni kukomaa kwa viungo vya mwili, na hivyo kwa mtoto wa kike yuko tayari kwa kubeba mimba na mtoto wa kiume anaweza kumzalisha binti. Mafunzo hayo hupewa awapo chuoni kwa kutumia nyimbo kama anapokuwa katika mafunzo ya ndoa anafundishwa namna ya kumtuza mume kwa kumpa heshima yake, kumpikia chakula ili ale ashibe asiende kutafuta kwingine, pamoja na kumtii kwani mume ndiye mkuu katika ndoa.

Soyinka (1975) anasema kuwa mwanamke ni pambo la mwanaume. Hivyo wakati wote mwanamke anatakiwa kuwa msafi kwa mume wake na jamii inayomzunguka. Pia anahimizwa kuwa na upendo kwa mume wake na familia yake. Mwanamke wa Kihiyao hayo anafundishwa akiwa unyagoni na mafundo ya ndoa. Ismail na Lienhardt (wahariri na wafasiri) (1968) wanasisitiza kwa kusema kuwa, mama ana wajibu wa kumfundisha binti yake malezi bora ya familia ili anapofikia binti kuolewa aweze kutunza vizuri familia yake. Anafundishwa uvumilivu na kuwa na siri ya mume na mke.

Moja ya mafunzo ya nyimbo za jando na unyago ya jamii ya Wahiyao wa Lulindi kuwa ni siri. Mashowali wanaelekeza wari kuwa na siri ya yale wanayofundishwa kwa watu wasiopitia jando na unyago. Siri ya jando na unyago ibaki kwa wale waliopitia mafunzo hayo. Allen (1971) anasisitiza kuwa binti anafundishwa jandoni kutokuwa na hasira. Hasira zinasababisha mtu kuzungumza jambo lisilofaa. Anafundishwa pia kuwa na adabu na ulimi wenye thawabu.

Liyong (1972) anasema kuwa, mwanamke baada ya kufanya kazi anatakiwa aoge na kuwa msafi. Siyo vema mwanamke kukaa mbele ya mume wake akiwa mchafu.

Inaweza kusababisha kukosekana kwa mvuto kwa mwanamke. Jamii ya Wahiyao wanamfunda binti kuwa pambo wakati wote la mume wake. Kwa kutofanya hivyo kunampa nafasi mume kutafuta mke anayevutia. Kwa hiyo binti anafundishwa kutotoa nafasi ya mume kutafuta mke mwingine msafi. Kwao ni aibu kubwa, kwani binti anaonekana hakupata mafunzo kisawasawa.

Ukichunguza nyimbo za jando na unyago za jamii ya Wahiyao wa Lulindi uchezaji wake ni wa kunengua na kupiga makofi. Hili limethibitishwa katika mjadala wa Wabunge bungeni Augusta 22/2006 wakati Mwantumu Mahiza, alipokemea juu ya mavazi ya wanamuziki wa kike kuwa ni mavazi ya nusu uchi. Alielekeza mavazi hayo yatumike kwenye ngoma za ndani tu ambazo hapo kale zilichezwa kwa lengo la unyago au jando, huku watu wachache tu ambao hualikwa na yale yanayofanyika huko ni siri yao tu. Haipendezi aina nyingine ya unenguaji hadharani. Anatuthibitishia kuwa katika jamii zetu kuna jando na unyago elimu inayoambatana na unenguaji.

TUKI (1981) imeandika maana ya unyago kuwa ni mkutano wa watu maalumu mahali maalumu pa siri panapofundishwa mizungu ya mila za kabila kwa vijana. Au ni ngoma ya kuwafundisha wari mila za kabila lao. Jando na unyago ni mila inayosisitiza uwepo wa siri kwa yale yaliyofundishwa Inategemewa kuwa yanayofundishwa yanamlenga tu yule anayekaribia utu uzima. Kumfundisha mtoto mdogo ni kumuingiza katika mazingira yasiyokuwa yake. Hatima ya hilo ni kumfanya afanye majaribio ya yale aliyofundishwa. Na matokeo ya hayo ni kuwepo kwa mmomonyoko wa maadili kwa jamii.

Harries (1965) anasema kuwa muda mzuri wa kumpeleka binti kufundwa (mwari) ni kuanzia miaka 11. Ni umri mzuri kwa kungwi kumfunda mwari na kumwelekeza mahitaji muhimu ya mume na urembo wa mwanamke kwa mume kama kuvaa shanga kiunoni (utandu).

Kabila la Wahiyao wa Lulindi hapo zamani waliingiza vijana wao jandoni na unyagoni katika umri wa miaka kuanzia 9 hadi 12 kwa vijana wa kiume na umri wa miaka 10 hadi 12 kwa vijana wa kike. Umri huu ulikadiriwa kuwa ni wa kijana kubalehe au kuvunja ungo kwa vijana wa kike. Kilikuwa ni kipindi kizuri kumpa maadili ya kiutu uzima,na kwamba tayari anafahamu madhara ya kufanya kinyume cha matakwa ya jamii.

Allen (1971) katika Mwanakupona, anaeleza kuwa, kumfundisha kijana mdogo ni kumlazimisha maisha ya kiutu uzima ambayo atayajaribu na hatimaye kutokea kwa mmomonyoko wa maadili. Kila mafunzo yafunzwe kwa wakati wake kulingana na umri wa kijana.

Hivi sasa vijana wa kihiyao wa Lulindi wanapelekwa jandoni na unyagoni wakiwa na umri mdogo kutokana na tamaa ya pesa ya wazazi au kutokana na ushawishi wa kundi rika. Mafunzo wanayopewa ni yaleyale ya watu wazima. Kutokana na uwezo wao kuwa mdogo, vijana wanashindwa kupembua mafunzo wanayopewa na badala yake mafunzo hayo wanayafanyia majaribio. Matokeo ya majaribio hayo ni vijana wa kike kupata mimba za utotoni.

Kutokana na kupanda kwa maisha kiuchumi, vijana hao wanashindwa kuwalea watoto wao na hivyo kujikuta wanaingia kwenye dimbwi la makahaba wa mijini, na

hatima yake ni kupata UKIMWI ambao ni tatizo kubwa kwa jamii zetu. Vijana wa kiume hujiingiza kwenye makundi ya uvutaji na utumiaji wa madawa ya kulevya.

## 2.3 Sifa za Ushairi wa Nyimbo

Ushairi wa nyimbo una sifa zinazoambatana nazo. Ushairi wa nyimbo unashawishi jamii kulipenda jambo fulani ambalo lina manufaa kwa maisha ya kila siku ya mwanajamii. Pia unaelezea majukumu ya jamii kwa familia zao kama majukumu ya mume kwa mke na mke kwa mume. Vile vile ushairi wa nyimbo unaonya tabia chafu zinazofanywa na jamii kama anavyosema Harries (Mhariri) (1965) anasemakuwa:

"All the Poems were prompted by the need to rebuke afriend whose wife's waywardness was the result of her husband's failure to behave decently towards her"

Mnyama hana utashi wa kumtunza na kumchunga mke, bali binadamu kutokana na utashi wake ana wajibu wa kumtunza mke na kumlinda ili aweze kutunza familia yake.

Soyinka (Mharir) (1975) ameandika kuwa mashairi yanatetea maisha ya jamii kwa kuelezea ugumu wa maisha ya jamii unaotokana na nini. Vilevile unaelezea ubaya wa kuwa mbali na mazingira ya mila, desturi na utamaduni wa jamii yako. Kila jamii inahitaji kujifunza yake kwa yao.

## 2.4 Jando na Unyago

Jando na unyago ni vyuo vikuu muhimu kwa jamii ya Wahiyao waishio Lulindi, Masasi. Ni ishara ya kuutoka utoto na kuuendea utu uzima. Katika utafiti huu, Watafitiwa wameeleza kuwa ni vijana wa umri wa miaka tisa hadi kumi waliingizwa jandoni na unyagoni. Na ikiwa kijana hakupitia Chuo hicho, aliitwa msongo au lingoni.

Kabila la Wahiyao makazi yao yanaingiliana na kabila la Wangoni na hivyo wanafahamu kuwa kabila hilo hawana jadi ya kutahiri vijana. Kwa hiyo kuitwa “Lingoni” kwao Wahiyao ni kumdharau mtu huyo. Ingawa hivi sasa Wangoni wanaoishi Lulindi wanafuata utamaduni wa wahiyao wa kutahiri vijana wao na kuwaingiza unyagoni. Kijana ambaye hakupitia jando na unyago hakuruhusiwa kuoa au kuolewa, kwani nidharau kubwa kwa jamii ya Wahiyao. Wahiyao wanaamini kuwa mafunzo ya siri yanayotolewa jandoni na unyagoni yanajenga tabia njema kwa kijana ambaye anategemea kuwa na familia ambayo ataifundisha kuwa na tabia njema.

Jando na unyago ni sehemu ya elimu ya jadi za makabila mengi hapa Afrika. Jando ni chuo cha vijana wa kiume,na unyago ni cha vijana wa kike. Chimbuko au isimu ya jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao tumeelezwa utafitini kuwa ni kutokana na mahitaji ya fasihi simulizi kwa jamii hiyo. Dhima ya fasihi simulizi ni kuelimisha jamii kuenenda vema. Ili kuwa na mwenendo na maisha bora, jamii inalazimika kufuata utamaduni, mila na desturi zilizopo. Kuheshimiana kunajenga ushirikiano na kusaidiana, kazi inajenga utu na heshima ya mtu, malezi ya familia yanajenga familia bora na yenye mwelekeo mzuri kimaisha.

Tumeelezwa utafitini kuwa jando na unyago ni chuo kikuu cha kutolea elimu kwa jamii hiyo ikifuatiwa na elimu ya kujua kusoma, kuandika na kuhesabu. Utaratibu wa kijana kupelekwa shuleni kajifunze elimu ya anga na elimu ya dunia, inafuatiwa baada ya kijana kuhitimu elimu ya jando na nyago. Tulifanya mahojiana na mtendaji wa kijiji Bi Asha Mohamedi Akida kujua ni mbinu gani wanatumia kuwashawishi

wazazi kuwapeleka vijana wao shuleni baada ya elimu ya jando na unyago. Yeye alitueleza yafuatayo:

(i) Utaratibu wa kuwapeleka watoto jandoni na unyagoni unaanzia na wazazi kuwaandikisha watoto wao wanaotarajia kupelekwa jandoni ili serikali ya kijiji kujua idadi ya watoto wanaohitajika kuingizwa jandoni kwa mwaka huo.

(ii) Baada ya kujua idadi ya watoto, kinafanyika kikao maalumu cha wazazi na serikali ya kijiji cha kuwekeana makubaliano na masharti ya kumuingiza mtoto jandoni, yakiwemo kila mzazi kuandaa vifaa vya kumtahiri mtoto kwa wale wa kiume ili kuepuka kutumia kifaa kimoja cha kutahiri kutokana na hali ya ugonjwa wa UKIMWI, pia kukubaliana kuwa vazi rasmi litakalovaliwa siku vijana wanahitimu (kutoka jandoni na unyagoni) liwe sare ya shule.

(iii) Wanashawishi walimu wa shule za msingi kufanya sensa ya vijana wenye umri wa kuanza darasa la kwanza kwa muhula mpya.

## 2.5 Chanzo cha Nyimbo za Jando na Unyago

Ili kujua chanzo cha nyimbo za jando na unyago, yatupasa tuakisi historia ya maisha ya jamii katika Afrika. Wataalamu wa urudhi ya Kiswahili wamechambua na kufafanua kuwa bahari za kishairi, asili yake ni nyimbo za jadi zilizokuwa zikiimbwa na manju, waimbaji stadi wa matukio na hafla mbalimbali kama za jando na unyago, harusi, matanga, ngoma na shangwe za maishani.

Ushairi uliambatana na nyimbo za kienyeji (Nyimbo za kiafrika). Kila kabila lilikuwa na ushairi wake au nyimbo zake zenye undani uliolenga sababu maalumu na tukio maalumu katika jamii. Tungo za Fumo Liongo ni moja ya nyimbo za kishairi zilizokuwa zikiimbwa hapo kale.

Nyimbo za jando na unyago ni miongoni mwa ushairi wa tangu awali. Ni nyimbo zilizolenga kwa ajili ya shughuli maalumu za kuwaandaa vijana katika maisha ya kiutu uzima. Ndani ya nyimbo hizo kuna mafundisho mema kwa vijana ambayo yamemjengea kijana msingi mzuri wa maisha yake ya baadaye na jamii yake. Nyimbo za kale zilikuwa na sanaa fulani ambayo haikuwa rasmi. Na hivyo haikuwa rahisi kutofautisha na umbo la wimbo na umbo la shairi.

Katika miaka ya karibuni ushairi au nyimbo za kienyeji zilikuwa zinaimbwa na watu walipojumuika katika matukio na hafla mbalimbali kama za jando na unyago, harusi, matanga, ngoma na shamrashamra zao za maisha. Kwa sasa nyimbo hizo zimefifia na badala yake muziki wa kizazi kipya umetawala. Watu kadhaa hufurahishwa zaidi na muziki huo na kuacha nyimbo za kienyeji ambazo zina mafunzo kwa jamii licha ya kuburudisha.

Nyimbo za Wahiyao wa Lulindi zinaimbwa kutegemeana na mazingira ya hafla. Kuna nyimbo zinazoimbwa jandoni na unyagoni ambazo ni za siri za kumfunda mwari. Nyimbo za shughuli zingine kama harusi, msiba, sherehe na kadhalika, nazo huchukua nafasi ya kutoa maonyo kwa watu wazima waliopitia jandoni na unyagoni lakini wanatenda kinyume na matakwa ya jamii.

Lengo la mafunzo ya nyimbo za jando na unyago ni kumfanya kijana asitende kinyume na maadili ya jamii. Jamii ina taratibu zake zinazolinda jamii hiyo. Nyimbo za jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao ni elimu kwa vijana wao. Inawaandaa vijana kwa maisha ya kiutu uzima.

Hapo zamani nyimbo za kufunda wari ziliimbwa jandoni na unyagoni kwa kuwaeleza vijana matendo mabaya yaliyotendwa na watu wazima. Walielezwa kwa mifano halisi kuwa mtu fulani, wanayemfahamu, ametenda jambo fulani baya. Kwa vile ni siri, hakuna aliyepata kutoa siri hiyo walipotoka jandoni au unyagoni. Kutokana na ukweli na uwazi uliotanda duniani, jamii ya Wahiyao wa Lulindi, sasa wameamua kuziimba nyimbo hizo za kuadilisha au kuadabisha watu hadharani. Lengo ni kuwafanya wenye tabia chafu wajifahamu na wafahamu kuwa watu wengine wamebaini maovu yao.

Kifasihi nyimbo hizo zinaimbwa kwa mafumbo, mafunbo ambayo ni rahisi kueleweka kwa kila mtu. Kwa vile jambo lililotendeka lilifahamika na baadhi ya watu, kwa kuimba, watu wanaulizana kuwa jambo hili limetokea wapi, lini na ndipo sasa linasambaa kwa jamii yote. Kwa kufanya hivyo mwenye kutenda jambo hilo anatambua kuwa jamii yote inafahamu na hivyo hawezi kutenda tena. Na kwa jamii kila mmoja anajaribu kufuata taratibu zilizoko katika jamii ili kukwepa aibu itakayojitokeza. Kwa vile dhamira ya fasihi ni kufichua maovu yaliyosakini kwa jamii, na nyimbo za jando na unyago ni moja ya tanzu ya fasihi simulizi basi zina nafasi ya kuelimisha jamii.

Jamii ya Wahiyao kama jamii nyingine hapa Tanzania, lugha yao inakuwa na kukomaa. Nyimbo zinazoimbwa zina mchanganyiko wa lugha ya Kiswahili katika kuelimisha jamii. Hali hiyo inatokana na kuzuka kwa nyimbo nyingi zinazotumia lugha ya Kiswahili katika kutoa maadili yake na kuacha kutumia lugha yao kwa kiasi kikubwa. Nyimbo hizo zimeshika kasi kubwa miongoni mwa nyimbo za Kihiyao.

Hali hiyo inafanya nyimbo nyingi za kiyao kusahaulika. Waimbaji wa nyimbo hizo za Kiswahili wanashindwa wakati mwingine kubadilisha maneno ya Kihiyao na kuyapangilia kiwimbo katika lugha ya Kiswahili kutokana na maneno ya Kihiyao kuwa magumu katika tarjima na yanapowezekana hupoteza maana ya wimbo huo. Nyimbo nyingi za ngoma kama za maseve, likwata, nkala na mayonjo (singenge) haziimbwi tena.

Nyimbo za wahiyao wa Lulindi siyo tu zinatumika jandoni na unyagoni, bali zinatumika pia kuchapusha kazi, kubembeleza watoto, kujiburudisha baada ya kazi, na kuomboleza. Nyimbo za jando na unyago zina tungo sawa na ushairi wa Kiswahili. Maneno yamepangiliwa. Watunzi wa nyimbo za jando na unyago wanaonyesha ujuzi wa kutosha katika kazi yao na wanaimudu lugha ya Kihiyao vizuri. Kutunga na kupangilia maneno ni kazi kubwa. Kunataka utuvu, shibe, utulivu, amani na taqiwa anasema Sengo (2009) ili kuweza kuwasilisha kitu bora kwa jamii husika.

## 2.6 Maudhui ya Nyimbo za Jando na Unyago

Maudhui ya nyimbo za jando na unyago ni kurithisha mila na desturi za jamii kutoka kizazi hadi kizazi kingine. Lengo ni kumuondolea kijana utoto na kumkuza awe mtu mzima ili aweze kutekeleza wajibati zake. Vilevile ni kurithisha mila na desturi za jamii ya Kihiyao. Utafiti umebainisha mambo mbalimbali anayofundishwa kijana ya kumtoa utoto ambayo yameonyeshwa kwenye uchambuzi wa data. Jamii ya Wahiyao waliona njia pekee ya kutoa elimu inayolingana na mahitaji ya jamii ni kuwafunza vijana wao kwa njia ya nyimbo. Hawakuwa na njia mbadala ya kuwaelimisha vijana

wao. Mafunzo yalitolewa kwa vijana waliokaribia kuwa watu wazima, na ambao walielewa na kuzingatia kile walichofundishwa.

Jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao wakati wa nyuma, vilikuwa vyuo vilivyokusudiwa kumjenga na kumwandaa kijana kwa maisha ya baadaye. Kwa hivi sasa jando na unyago havitiliwi mkazo. Ni vyuo vinavyopuuzwa. Katika utafiti wetu tumejifunza tofauti ya taratibu za jando na unyago zilivyoendeshwa na jamii ya Wahiyao hapo awali kabla ya wanasiasa kuingilia kati taratibu hizo. Katika utafiti wetu, wazee wa Kihiyao wameonesha kulalamikia kupotea kwa jadi yao. Hivi sasa hakuna jando na unyago kama la wakati wa zamani. Tumeelezwa kuwa hivi sasa vijana wanatahiriwa sana mahospitalini na kuishi nyumbani badala ya kukaa chuoni ambako wanapewa mafunzo kisawaswa.

Utafiti umebaini kuwa sababu kubwa ni kutokana na hali ya kiuchumi ya wanajamii. Kuwaweka vijana chuoni ni kutumia gharama kubwa za kuishi kuliko kuwaweka nyumbani. Wakiwa nyumbani vijana wanapata mahitaji sawa na wengine. Sababu za kuwapeleka hospitali ni kupata huduma ya karibu na waganga wa kutibu kitaalimu, na hivyo wanapona haraka vidonda vyao.

Kwa hiyo utafiti huu, umechunguza mafunzo ya nyimbo za jando na unyago na matokeo ya mafunzo hayo kwa vijana wa jamii ya Wahiyao wa Tarafa ya Lulindi Masasi. Mafunzo ya nyimbo za jando na unyago yanakuza utu. Inamtoa mtu katika utoto na kuelekezwa katika maisha ya ki-utu uzima Howani.H (2004). Nyimbo ni moja ya tanzu za fasihi simulizi. Maudhui ya nyimbo ni kuelimisha, kuburudisha na pamoja na kuonyesha maendeleo ya nchi. Nyimbo za jando na unyago zinaelimisha

vijana maisha ya kiutu uzima. Elimu ya nyimbo za jando na unyago zinamweleza kijana ni maisha gani ya utu uzima anatakiwa aishi. Kijana anatakiwa aishi kwa kufanya kazi, kujali malezi ya familia, kutunza na kujali ndoa. Yote haya ni maisha ya utu uzima. Sengo (2008) amesema kuwa fasihi simulizi inajali utu wa mtu.

Sengo (2009) vilevile amesema kitambulisho cha utu uzima ni uungwana, ustaarabu, heshima, busara, fikira na hadhira za mtu. Mtu akikosekana na haya yote, utu wake unapotea. Nyimbo za jando na unyago zinamfundisha mtu kuwa na utu bora katika maisha yake ya kila siku. Fasihi simulizi inajali utu wa mtu kwa kuitazama jamii na kuielekeza kwa kufichua maovu yanayojitokeza kwa jamii. TUKI (1985) inaelezea jinsi ushairi unavyoshika nafasi ya kufichua maovu kwa jamii.

Kila mmoja katika jamii ni kiongozi wa mweziwe wa kufichua maovu yanayojitokeza jamiini. Mwanajamii ndiye anayefahamu mahitaji ya jamii yake. Mtu kutoka jamii nyingine ni vigumu kuelewa mahitaji ya jamii nyingine. Mila na desturi na utamaduni wa jamii fulani wanaofahamu ni wanajamii wenyewe. Uchumi ni jambo muhimu sana kwa maisha ya jamii. Uchumi ndiyo chanzo cha maendeleo ya jamii. Ili kujenga uchumi bora, jamii haina budi kufanya kazi. Kazi ni msingi wa uchumi wa jamii.

Sengo (2008) pia amesema “Vijana katika jamii ni vema wapate mafundo ya awali ambayo yanawasaidia kupata maadili mema”. Kijana asiyepata, kuishi maisha yasiyo na heshima, hawi mtu wa kisawasawa. Kwa vile fasihi simulizi huelimisha jamii, vijana wasiopata elimu ya awali, huyapata kwa njia hii ya fasihi simulizi na hivyo kuweza kubadilika na kuwa wanajamii bora. Kudumisha fasihi simulizi ni

kudumisha utamaduni wa wanajamii na wakati mwingine inasaidia kurahisisha ubadilishanaji wa maarifa na utendaji kazi. Kazi ndicho kitivo cha uhai wa mtu. Mtu lazima afanye kazi ili apate uzima bora bila kujali aina ya kazi.

Uchumi na jamii ni taasisi zinazohusiana katika utoaji wa kazi ya fasihi. Kila kazi za fasihi ni lazima iguse jamii ili iweze kufikia lengo lake. TUKI (2000) imeandika kuwa hali ya uchumi ndiyo inayochipuza hadhira ya wasomaji. Kusoma kunategemea uwezo wa jamii au mtu wa kununua vitabu, magazeti na majarida. Fasili za fasihi zimeegemea kuielezea jamii uhusiano wake na jamii. Inaeleza kuwa fasihi ni taasisi ya jamii na uhusiano wake na jamii ni wa karibu sana. Fasihi inachukuliwa kama sehemu ya maisha ya jamii.

Ni taasisi ya jamii kwa sababu fasihi inatumia lugha ambayo ni zao la jamii. Inazungumzia maisha yanayohusu uhalisia wa kijamii. Kama fasihi inawahusu watu fulani basi fasihi hiyo inahusu jamii hiyo. Yanayozungumziwa yanatokana na maisha ya jamii hiyo. Mtunzi wa kazi za fasihi ni mwanajamii ambaye ana nafsi na tabaka fulani katika jamii yake. Hawezi kukwepa athari yoyote katika kazi yake ya fasihi. Maendeleo na mabadiliko ya jamii yanaambatana na mabadiliko ya fasihi.

Uhusiano huu unatokea kwa sababu maisha ya jamii yanapobadilika, mwelekeo, utamaduni na maadili ya jamii nayo yatabadiika. Mabadiliko ya fasihi simulizi ni zao la mabadiliko katika maisha ya jamii. Jamii ya Wahiyao wa Lulindi wanatumia fasihi simulizi katika kuelimisha watu wao. Wanatumia jando na unyago kuwa Chuo cha kutolea elimu yao ya jadi. Elimu hiyo inalenga kumuondoa kijana utotoni na kuwa mtu mzima. Mafunzo yanayotolewa ni ya kiutu uzima. Mafunzo hayo kwa kipindi

cha nyuma utafiti unatueleza kuwa vijana wenye umri wa miaka kuanzika 9 hadi 12 ndiyo waliopelekwa jandoni na unyagoni. Ni umri uliokadiriwa kuwa kijana alibalehe au alivunja ungo. Huo ni utu uzima. Na hivyo walipotoka jandoni kijana wa kiume aliweza kuoa na wa kike kuolewa.

Jando na unyago kwa watoto wa umri mdogo katika jamii ya Wahiyo sasa umekithiri na kumejitokeza hali ya mashindano makubwa ya nani ana uwezo zaidi kiuchumi kuliko mwingine. Wazazi wanatumia rasilimali nyingi kufanya sherehe kubwa za jando na unyago kwa watoto wao bila kuwa na mafanikio ya malengo ya elimu hiyo. Wakati wa sherehe hizo vyakula na pesa nyingi zinatumika kwa kununulia mavazi ya watoto na chakula kingi kinatumika kwa kuwalisha watu naa kupika pombe na togwa, vinywaji kwa ajili ya wageni wengi wanaoalikwa na wasioalikwa.

Shughuli zote za jando na unyago zinaandaliwa na bibi na babu wa watoto. Ni kipindi cha wazazi wa watoto hao kurudi kutoka mijini kuja kusherehekea. Matumizi ya pombe yanakua ni makubwa kwa kipndi hicho. Pombe ni mama wa maasi. Haimpi muda wa mtu kufanya maamuzi. Kutokana na siku hiyo jamii kuwaacha vijana huru huku wakisherehekea, mambo mengi kama ngono huria, na wizi vinajitokeza. Kwa hali hiyo yawezekana ndiyo kipindi mimba nyingi zinazaliwa, na maambukizi ya UKIMWI yanaweza kujitokeza. Sherehe hizo tumeelezwa kuwa zinaanzia mchana, zinakesha hadi siku ya pili.

Diwani Bi Asha Akida ametueleza kuwa, kutokana na kutumika kwa chakula kingi katika shughuli hiyo, Wahiyao wa Lulindi wamekuwa wanakumbwa na tatizo la njaa

la mara kwa mara hasa kipindi cha kuanzia mwezi Desemba hadi Machi. Ni kipindi kigumu kwao hadi mazao mapya yanapokuwa yameiva.

Tumefanya mahojiano na wazazi ishirini na 25 wa kike na ishirini na 25 wa kiume kujua ni hatua gani wanazichukuwa kukabiliana na tatizo hilo. Wote kwa asilimia mia moja wametueleza kuwa wao na vijana wao, kipindi cha mwezi wa Oktoba hadi Novemba wanafanya biashara ya kubadilishana maji na makopa kutoka vijiji vya jirani vya Wilaya ya Newala ambavyo ni Mkoma na Chitekete. Inawalazimu kubeba maji vichwani yasiyopungua lita ishirini kichwani na kupandisha kwenye miinuko mikali iliyopo maeneo hayo. Kwa asili Wilaya hiyo ina shida kubwa ya upatikanaji wa maji. Hivyo maji hayo ni muhimu kwao na hivyo wanayakubali kwa kubadilishana na makopa. Mara mvua zinapoanza kunyesha biashara hiyo inajifunga. Hata hivyo walitueleza kuwa biashara hiyo ni ngumu kwao kwa sababu inatumia nguvu nyingi kwa kutembea na faida yake ni ndogo. Kutokana na hali hiyo, vyungu na maji yanayobeba ni kiasi kidogo na haikidhi haja. Chakula kinachopatikana ni kidogo na kinatumika kwa muda mfupi wa miezi miwili hadi mitatu. Inapofikia mwezi wa pili njaa inazidi kuwa kali na maisha kuwa magumu zaidi. Kwao kipindi hicho wamekipa jina la “Febu “Yaani Februari. Wamekipa jina hilo kwa sababu kila mwaka kipindi hicho ni cha njaa kali.

## 2.7 Umuhimu wa Jando

Nyimbo za Jando na unyago ni muhimu kwa jamii ya Wahiyao. Ni mila iliyoanza tangu zamani kwa jamii hiyo. Jando ni shule ya pili kwa kijana wa kiume. Wakiwa jandoni vijana wanapewa mafunzo ya ki-utu uzima. Yanayomuandaa kijana kuwa mtu mzima mwenye maadili mema kwa jamii yake. Howani.H (2004) anadokeza

kwa kuandika kuwa tangu zamani mtoto wa jamii yoyote alipovunja ungo au kubalehe alipelekwa kuchezwa (kumtoa utotoni) na kumfundisha majukumu ya ki-utu uzima. Majukumu yanayofundishwa ni yale yanayohusu utamaduni wa jamii yake kama**:**

(i) Kuheshimu wakubwa

(ii) Kuwa shupavu

(iii) Uwajibikaji

(iv) Majukumu ya kulea familia na ukoo na kabila lake.

Ni mafunzo yaliyolenga kumuingiza kijana katika utu uzima. Wakati huo vijana waliingizwa jandoni katika umri wa miaka 9 hadi 12 . Wanawake hawakuruhusiwa kuingia jandoni. Sababu za haki za binadamu. Si vema mwanamke kushuhudia kijana wa kiume anavuliwa nguo na kuona kila jambo analotendewa wakati anatahiriwa. Watoto wanapotahiliwa wanapata maumivu makali. Kwa vile mwanamke ana huruma, akiruhusiwa kuingia anaweza kusababisha kuwakatisha tamaa vijana nao kuweza kushindwa kuvumilia. Wakiwa jandoni vijana wanafundishwa nyimbo zinazosisitiza wanawake hawatakiwi jandoni.

Vijana waliimba nyimbo za kuabudu Miungu wao. Wahiyao kabla ya kuingia dini ya Allah (S.W) na dini ya kikristo waliamini katika kuabudu mizimu kuwa ndiyo iliyowasaidia katika kufanikisha mambo yao. Miungu hiyo iliitwa “Achimasoka” Waliomba chini ya miti mikubwa, au chini ya milima kwenye mapango ambapo waliyaita “Msolo” Waliombwa ili kuwaponesha vijana waliotahiriwa na kuwasaidia kuishi kwa amani huko porini. Wembah. R (1975) anaeleza pia kuwa kabla ya kuwapeleke vijana jandoni, Mwenye na wazee walioteuliwa akiwamo dada wa

Mwenye (mkuu wa ukoo) kwanza hufanya zindiko eneo litakalotumika kwa shughuli za jando (kutahiri).

## 2.8 Umuhimu wa Unyago

Unyago ni sehemu ya elimu ya jadi kwa vijana wa kike. Ni sehemu muhimu ya utamaduni wa jamii ya Wahiyao. Mabinti wakiwa unyagoni wanafundishwa wajibati zao watakapokuwa watu wazima (Mulokozi katika TUKI, 1999) anaeleza kuwa vijana wakiwa unyagoni mabinti wanafundishwa masuala ya uzazi na namna ya kulea watoto. Binti anafundishwa usafi wa mwili na mavazi. Anafundishwa pia kujipamba kwa ajili ya mume wake ili aweze kumpokea akiwa nadhifu itakayomvutia mume huyo. Pia unyagoni wanafundishwa kutomnyima mume chochote anachohitaji kwa mke wake na kumuhudumia vizuri katika chakula cha ndoa. Mume pia anafundishwa namna ya kumtunza mke kwa kumpa upendo na kumsaidia katika mambo ya kifamilia.

Mabinti wanafundishwa namna ya kuishi na watu wa jamii yake, na ndani ya nyumba na mume wake bila mikwaruzano. Mwanamke anafundishwa namna mbalimbali ya kujinusuru katika ndoa na kuepuka shari ili kuifanya ndoa yake idumu muda mrefu. Njia mojawapo wanayofundishwa ni kumtii mume wake kwa lile asemalo, kutabasamu amuonapo, kutojibizana pale anapokemewa kama ametenda kosa au hakutenda. Mke bora ni yule anayemtii mume wake na mara zote ana tabia ya kuomba radhi kwa mume wake pale anapomkosea mume wake. Uzuri wa mapenzi ya kusikiliza ni kujenga jamii yenye amani na furaha.

Mwanamke anatakiwa kuwa na sanaa katika kumpendezesha mume wake ili awe mke bora kuliko wote. Anatakiwa awe mvumilivu hata anapotendewa makosa.

Mwanamke anatakiwa kujua kuwa maisha ya mume na mke yanahitaji siri. Kazi ya wazazi kwa watoto wa kike ni kutoa mafunzo kwa mabinti zao.

Unyago kwa jamii ya Wahiyao ni sehemu ya kufundishia mabinti zao utulivu,umakini katika matendo yao, kutopenda tabia ya kuropoka, kuwa na lugha tamu kwa mume, kuwa na mapenzi yanayomthamini mume na kutukuza penzi lake, pamoja na kumpa mapumziko mume wake baada ya kazi ngumu. Mwanamke anafundishwa kutojibizana na mume wake. Anatakiwa kumsikiliza na kumtii. Uaminifu wake ndio utakaojenga maisha ya ndoa ya kudumu hadi Allah (S.W) atakapomchukua (Waawy, 2011).

Katika jamii ya Wahiyao mume ndiye kiongozi katika familia. Ndiye msemaji wa kila jambo katika familia. Mke ana kazi ya kumtii mume kwa lile asemalo. Vedasto (2010) pamoja na kufundishwa na hayo yote, mwanamke anapaswa kuchunguza mume bora atakayemfaa katika maisha yake ya ndoa siyo bora mume. Jamii ya wahiyao inamuandaa binti kuwa ni mtu wa kutulia nyumbani.Utulivu wake ndio utakaomfanya aolewe. Wanaamini kuwa mwanamke asiyeolewa anaonekana ana kasoro miongoni mwa wanajamii yake.

Walombo waliwafundisha wasichana jinsi ya kutunza familia zao, jinsi ya kutayarisha chakula cha ndowa kwa kuwafundisha ngoma ya kunengua iitwayo “Chamba” Wasichana walichezwa unyago katika umri wa kuanzia miaka kumi (10) na kuendelea. Yalikuwa ni maandalizi ya kuolewa na kuzaa watoto. Wakiwa unyagoni waliimba nyimbo za kumfundisha mwari namna ya kufanya mapenzi.

# SURA YA TATU

## 3.0 NADHARIYA TETE

### 3.1 Utangulizi

Hali halisi ya kitu au jambo ndiyo inayofanyisha kitu au jambo hilo. Utafiti wetu umethibitisha ukweli wa nadharia ya Sengo ya "Uhalisia wa Kiafrika" ambao hutendeza mambo na majambo kulingana na hali halisi ya maisha ya jamii (Sengo, 2009).

Sengo (2009) ameandika kuwa kila jamii ina mila na desturi zake. Mila na desturi hizo ndizo zinazolinda maisha ya jamii hiyo. Ili kujenga maisha ya kweli ya jamii, tabia na mwenendo wa jamii hiyo ni lazima yaambatane na vitendo vya kweli na vya kiutu kwa kila mmoja jamiini. Matendo hayo ndiyo yanayodhihirisha mwelekeo wa maisha ya jamii hiyo.

Uhalisia katika jamii unajitambulisha kwa maisha ya kweli wanayoishi wanajamii. Jamii inahitaji kuheshimiana, kusaidiana, kutambuana, kufanya kazi, kushirikiana na kuishi kwa amani. Kama jamii haitatambua hali hizo na kuishi kinyume cha matakwa hayo ya jamii basi inalazimika kuchukua mkondo wake wa kufahamisha jamii itambue na kuyarekebisha maovu yanayojitokeza.

Ili kujenga jamii iliyo sawa ambayo ina mwelekeo mzuri wa maisha, jamii hainabudi kuangalia matendo ya jamii kama yanaenda sambamba na matakwa yake; Kama yanatendwa kinyume yanaelekezwa ili yaende sawa. Jamii nyingi za kiafrika zinatoa mafunzo kwa vijana ya mila na desturi kwa kupitia mafunzo ya jando na unyago. Ni chuo pekee kinachomjenga kijana katika maadili mema (Mulokozi 1999).

Mafunzo hayo yanamtoa kijana katika maisha ya utoto ambayo yanategemea baba na mama na kumfundisha maisha ya kiutu uzima, ambayo anafundishwa namna bora ya kuishi na watu katika jamii. Jamii ya Wahiyao wanaonyesha uhalisia huo kwa kutoa mafunzo kwa vijana kupitia jando na unyago. Mafunzo ambayo yanaongoza maisha ya jamii. Tabia na mwenendo bora unaoelekezwa jandoni na unyagoni ambako uhalisia huelekezwa.

Siri ya nyimbo za jando na unyago za Wahiyao yajulikana na Warombo waliopitishwa katika Taasisi hizo huko Uyaoni na jamii yenyewe ya Wahiyao. Utafiti wetu umetuthibitishia nadharia ya Sengo. Inatupa picha kuwa, mgeni ni jogoo la shamba, haliwiki mjini. Anayejua siri za jando na unyago ni Warombo na vijana waliopitia jando na unyago na kuona manufaa ya chuo hicho. Anayejua mila na desturi za jamii fulani ni aliyezaliwa na anayetoka katika jamii hiyo. Atokaye jamii nyingine ni lazima ajifunze kutoka kwa jamii husika, ndipo aweze kujua mila na desturi za jamii hiyo. Ni kosa kuisemea jamii nyingine ili hali hujua mahitaji ya jamii hiyo. Haitoshi kwa kusema mimi ni kabila la wahiyao kwa ukabila, wakati hujazaliwa na kuishi uyaoni na kujua maisha yake yanaendeshwaje. Ni mila na desturi zipi zinafuatwa.

Lawuo (1981) anaeleza kwa kusema kuwa, utoaji wa elimu kwa vijana katika kila jamii unatofautiana. Mafunzo hayo yanatofautiana katika muundo na yafundishwayo. Lakini lengo la kila jamii ni kuwajenga vijana kwa maisha yao ya baadaye ya kiutu uzima na kuweza kuhifadhi, kulinda na kuendeleza mila na desturi za jamii zao. Uhalisia katika jamii unazingatia zaidi ukweli wa maisha ya jamii. Jamii ndiyo

wahusika mahsusi katika mazingira yao mahususi wanayoishi. Kila kinachotendeka katika jamii ni zao la hiyo. Kutokana na mabadiliko ya maendeleo ya kisayansi, jamii zimeathiriwa na uhalisia wake. Mivutano ya maisha kwa jamii imejitokeza kuwa mikubwa sana. Mila na desturi za jadi za jamii zinafifia na kufuata zaidi mabadiliko ya maisha ya kisayansi yanayojali matumizi ya teknolojia mpya kama kutumia komputa na setilaiti katika mawasiliano.

Utafiti umebaini kuwa mafunzo ya jando na unyago, hayaendeshwi kisawasawa kama hapo awali. Kinachojitokeza hivi sasa ni kutimiza mila hiyo tu lakini mafunzo yanayotolewa hayakidhi haja ya jamii kutokana na umri wa vijana kuwa ni mdogo tofauti na malengo ya elimu hiyo ya kuwaandaa maisha ya kiutu uzima (Lawuo 1981). Kinachofundishwa hakimjengi kisawasawa mwari. Mila ya jando na unyago imepungua thamani yake.

Watu wengi katika jamii hawapendi kuwapeleka vijana wao porini ambako ndiko tangu awali elimu ya jando na unyago imekuwa ikitolewa kama sehemu ya chuo hicho. Badala yake wanapelekwa hospitali kwa madaktari kuwasafisha bila kupewa mafunzo yoyote kwa upande wa vijana wa kiume. Na wale wa kike wanabaki nyumbani kwa wazazi wao, wakihudumiwa na familia na kupewa maelekezo ya kifamilia kama aoshe vyombo, asiwe mbishi na kuamkia watu wazima. Mafunzo ya kiutu uzima mzazi si rahisi kumfundisha mtoto wake majukumu ya kiutu uzima kama kumtunza mume, kuzaa na kutunza familia, kwa sababu kwa kufanya hivyo ni kama mzazi anajidhalilisha mwenyewe.

Nyimbo za jando na unyago ni mila ambayo inatoa mafunzo ya kiutu uzima, yanayomuandaa kijana kuwa na maisha bora hapo baadaye. Ukamilifu wa mafunzo

hayo ndiyo unaompa mwelekeo mzuri wa maisha ya kijana. Kwao Wahiyao kuikosa elimu hiyo ni sawa na kuishi bila kuvaa nguo. Kama kila nadharia ina kwao na kwa sababu zake utafiti umetudhihirishia kuwa Wayao wanatumiya nadharia ya uhalisia. Hali halisi ya mafunzo ya jando na unyago ndiyo msingi wa maisha ya jamii ya Wahiyao. Wahiyao wanatumia fasihi simulizi katika kueleza uhalisia wa maisha yao ya kila siku. Jando na unyago ni sehemu ya fasihi simulizi ya wahiyao.

## 3.2 Mkabala wa Kinadharia

(i) Fasihi simulizi ya jando na unyago ina nyimbo, tumezikusanya nyimbo hizo wakati wa utafiti.

(ii) Ushairi-simulizi una kwao (Sengo 2009) tumeuona ukwao wa nyimbo za jando na unyago za Wahiyao kwenye utendezi wa nyimbo hizi.

(a) Nyimbo za jando na unyago zina mafunzo, tumeyaona mafunzo hayo hasa kwenye maadili ya nyimbo hizo tulipotembelea jandoni na kumbi za unyago na kujionea wenyewe yanayofundishwa.

(b) Uhusiano kati ya fasihi simulizi na nyimbo za jando na unyago tumeuona baada ya kukusanya data na kuzichambua.

(c) Fani na Maudhui ya nyimbo za jando na unyago, zimejidhihirisha wakati wa utafiti kama zilivyo kazi zingine za kifasihi hasa katika nyimbo zake za kufunda wali.

(d) Umuhimu wa jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao, tumeuona wakati wa utafiti baada ya kukusanya nyimbo zake na kuzichambua.

Mkoa wa Mtwara unajumuisha makabila ya Wamakonde, Wahiyao, Wamakuwa na Wamwera. Makabila hayo yanafanana kiutamaduni, kimila na kidesturi. Ni eneo ambalo limekumbwa na tatizo la vijana wengi wasio na maadili. Vijana wengi hawapendi kufanya kazi wala kusoma. Badala yake, wanakimbilia mijini, hasa jiji la Dar es Salaam kutafuta kazi. Hatimaye wanakosa ajira na kujikuta wanaishia kuwa vibaka kukidhi njaa na mabinti kuuza miili yao na kujitumbukiza kwenye bahari ya UKIMWI kwa hiyari zao.

Tulifanya mahojiano na mtendaji wa kijiji ambaye jina lake alitutambulisha kuwa ni bwana Hamza Selemani alisema kuwa tatizo kubwa ni hali ya uchumi ya chini na hivyo wanakuwa na tamaa ya kwenda mijini kutafuta kazi ili wainue maisha ya familia zao. Amesema kuwa vijana wengi wamerudi mijini wakiwa wagonjwa na kuishia kifo. Kuna nadharia mbalimbali za fasihi na za fasihi simulizi:

### 3.3 Nadharia ya Kijamii

Sengo (2009) anasema kuwa nadharia hii inaangalia vitendo vya jamii na namna jamii inavyotumia vitendo hivyo katika kuleta maendeleo. Kwa kuwa jamii inakua, inabadilika na kuingiza fikra na mawazo mapya, inawajibu wa kuwafundisha watu katika jamii mwelekeo mzuru wa maisha yake. (Mulokozi, 2002) ameandika kuwa tabia na mwenendo mwema miongoni mwa wanajamii ndiyo chanzo bora cha maendeleo ya jamii husika.

Dorson (1968) anafafanua kwa kusema watu katika jamii wanalazimika kufuata taratibu zilizowekwa kwa vile zipo na lazima zifuatwe. Kutokana na hilo ili taratibu hizo zidumu ni lazima jamii walazimike kuzipenda. Mfano jamii inalazimika

kuupenda utamaduni wa jamii yake kwa vile ndimo alimozaliwa katika utamaduni huo. Jamii itastaajabu mtu akiukataa utamaduni wake kwa kuona kuwa ni mbaya ukilinganisha na utamaduni wa jamii nyingine. Kwa vile ni jambo linalorithishwa, jamii haina budi kuukubali na kulazimika kuuzoea. Jambo la muhimu kwa wanajamii, ni kuurekebisha utamaduni huo na kuuweka katika hali bora.

Kila mtu ana hisia yake kulingana na mungu alivyomuumba. Kazi za fasihi ni budi zihakikiwe. Mhakiki wa kazi ya fasihi ana uhuru wa kuisoma kazi ya fasihi ya mwanafasihi asilia na kuirekebisha vile aonavyo bila kubadili dhima ya kazi hiyo. Ana uhuru wa kuongeza au kupunguza maneno makali yenye sumu kwa jamii kwa lengo ya kuijenga na siyo kuipotosha jamii. Ana uhuru wa kuwakosoa wanafasihi pale wanaposema kinyume na matakwa ya jamii. Ana haki ya kuchambua uzuri na ubaya wa kazi ya fasihi ki-fani na ki-maudhui. Nadharia hii inaangalia vitendo vya jamii na namna jamii inavyotumia vitendo hivyo katika kuleta maendeleo.

Shaaban Robert (1991) anahimiza mapenzi bora miongoni mwa wanajamii. Anakemea chuki. Chuki ikitawala miongoni mwa wanajamii, inapandwa mbegu mbaya. Jamii yenye chuki haina utaratibu bora wa maisha yake. Shaaban Robert asema ‘’Chuki wenyewe wanyama mwitu’’ Nadharia ya jamii inapogundua mapungufu kwa jamii inasimamia kuyakemea na kuyarekebisha haraka kabla mbegu mbaya haijapandikizwa.

Mvungi (1982) anaielekeza jamii kuondokana na uroho na hali ya ubinafsi unaotokana na kijilimbikizia mali ya jamii kwa manufaa ya mtu mmoja. Matarajio ya wanajamii ni kuishi maisha ya raha kutokana na matunda ya kazi zao. Kwa hiyo

nadharia ya kijamii itajengeka kama jamii yenyewe itaijenga nadharia hiyo kwa kuacha matendo maovu.

Katika jamii ya Wahiyao, nyimbo za jando na za unyago hutumika kuelimisha vijana wao. Nyimbo hutaja matendo mabaya yaliyotendwa na mwanajamii. Katika nyimbo hizo hufichua vitendo viovu vya wanajamii kama njia ya kuonya. Na wakati mwingine nyimbo hutaja hata jina la mtu aliyefanya kinyume na matakwa ya jamii ili watu wengine wamjue alichofanya na hivyo ni rahisi kujirekebisha Sengo (2009) katika *Tungizi za Mnyagatwa*, ambaye kwa kuwa kafundwa katika vyuo viwili vya jadi, (1959) na (1960), hasiti na yeye kufunda wengine. Utafiti wetu umekusanya nyimbo za jando na unyago zinazoimbwa na Wahiyao kwa lengo la kuwarekebisha waliotenda makosa hayo. Hapa ndipo uhalisia wa Kiafrika (Sengo 2009) unapojidhihirisha kuwa ni Nadharia hai maishani.

### 3.4 Nadharia ya Kiushumuzi

Nadharia nyingine ni ile ya kiushumuzi Sengo (2009). Nadharia hii inampa nafasi mtu kutoa kero zilizoko moyoni mwake. Mvungi (1982) anaitazama jamii ya Tanzania na kuikosoa. Jamii inatazamia kupata raha kila siku za maisha yake. Kuwa na raha katika maisha ni kutenda mema kwa kubadili tabia na mwenendo mbaya. Mafunzo ya jando na unyago yanafundisha vijana kero zinazoweza kutokea kwa jamii na athari zake kwa jamii. Jamii inapopatwa na kero amani na utulivu hupotea; Kwa hiyo nadharia inahimiza kuwepo kwa amani miongoni mwa wanajamii.

Mloka (1997) amekemea watu katika jamii wasiofuata utamaduni, mila na desturi za jamii yake. Kila jamii ina utamaduni, mila na desturi zake. Hivi ndivyo

vinavyoongoza maisha ya jamii. Jamii isiyokuwa na utamaduni, mila na desturi, ni sawa na kuku asiyewaza kesho atakula nini. Kila mtu katika jamii anapaswa kuishi kwa kufuata taratibu zilizokubaliwa na jamii hiyo. Taratibu zisipofuatwa inakuwa ni kero kwa jamii yote. Kazi ya fasihi na fasihi simulizi ni kufichua ouzo uliosakini kwa jamii.

Hii itamsaidia mtu kupata ahuweni wa kile kinachomkera. Kazi ya fasihi na fasihi simulizi ni kufichua uozo uliosakini kwa jamii. Nadharia hii inaangalia tabia na mwenendo wa mtu katika jamii. Kwa kutumia ushumuzi, mtu hufahamika nia na matakwa yake. Kama tabia na mwenyendo wa mtu huyo ni kinyume cha maadili ya jamii, basi fasihi simulizi huchukuwa mkondo wake kuubadili mwenendo na tabia hiyo haraka. Kwa mfano vijana au watoto, katika umri wa utoto, wanapoonyesha tabia fulani kama vile uvivu, wizi, kuvuta au kutumia madawa ya kulevya, kiburi, na jeuri na ngono nje ya ndoa, ulevi kupindukia, nadharia ya ushumuzi au jamii, hukomesha ila hizo kwa kuwafichua kwa kuimbiwa nyimbo wakati wa jando na unyago.

### 3.5 Nadharia ya Kielimu

Nadharia ya kielimu inaelezea juu ya fasihi inavyoelimisha (TUKI, 1978) Ni wajibu wa fasihi kuiangalia jamii kama ilivyo. Fasihi iiangalie jamii kwa karibu matatizo yanayoisonga na kuikandamiza jamii. Matatizo hayo yawe halisi na si ya kubuni ili kuifanya jamii ibaini mapungufu yake ya utovu wa maadili. Ni muhimu fasihi ifichue, ichambue, na ichochee jamii. Fasihi iwafungue watu macho na ifichue uchafu uliosakini miongoni mwa wanajamii. Wakandamizwaji wapate muongozo

sahihi ili waitambue hali yao ya kukandamizwa. Fasihi ielekeze jamii kutolalamika bali wafanye kazi. Fasihi iwe ni kichocheo na iwasuke wanyonge ili waweze kupambana na wakandamizaji. Fasihi inafichua maovu yaliyo sakini jamiini na kuyatafutia suluhishi. Kwa elimu, fasihi simulizi humaliza migogoro inayojitokeza kwa jamii kwa mifano hai ya tanzu zake.

### 3.6 Nadharia ya Fasihi

Nadharia ya fasihi inayoangalia fasihi na jamii. Sengo (2009) ameigawa nadharia hii katika sehemu kuu mbili. Nadharia ya fani ambayo katika kazi ya fasihi kuna lisemwalo na namna ya kulisema, mbinu, mtindo na uzungumzaji wake. Pili ni nadharia ya dhima na kazi. Kazi ya fasihi ni kuyaweka mambo wazi, kazi ya fasihi katika jamii ni kumshawishi mwanajamii kuitumia lugha yake kwa umahiri. Fasihi inamfundisha mtu mwenye kuitaka lugha.

Mbogo (2011) ameandika kuwa fasihi huchota maudhui na visa vyake kutokana na maisha ya jamii na ulimwengu anaoishi. Huzungumzia matukia halisi katika uhusiano na jamii, inaangalia histori ya jamii, imani na itikadi mbalimbali, fikra na ubunifu wake mwanajamii, maumbile na mazingira halisi ya jamii pamoja na sayansi katika jamii. Maendeleo ya jamii, ni lazima yaletwe na watu wachache katika jamii na ambao wamejitoa muhanga katika kupigania maisha ya jamii. Mwanafasihi uiangalia jamii na matendo yake na kisha kufichua uovu uliosakini. Kazi ya fasihi ni kutoa mafunzo kwa jamii. Mafunzo yanayotokana na uhalisia kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni vilivyo katika mfumo wa jamii (Senkoro, 2011). Yanayoelezwa katika fasihi ni uhalisia wa maisha ya jamii yanayoandikiwa kazi ya fasihi hiyo.

Mbogo (2008) ameiangalia jamii jinsi inavyotumia fasihi katika maisha ya kila siku. Maisha ya watu katika jamii yamejaa ukatili, vitisho na mbinu za sihiri, hali inayoifanya jamii kuishi kwa woga na wasiwasi. Kazi ya fasihi ni kufichua maovu yaliyosakini kwa jamii. Vitisho na ukatili vinavuruga amani ya wanajamii kwa kuishi kwa woga na kutoaminiana vyote hutokomezwa na kazi za kifasihi. Fasihi ni zao la jamii, ina wajibu wa kuifichua na kukemea maovu yanajitokeza kila siku katika jamii kwa lengo la kuiweka sawa jamii husika. Vitisho na sihiri vimejengwa jamiini ili kupunguza uhuru wa wanajamii kutenda vitendo bila woga ingawa vitisho vinajenga uwezo mdogo wa kufikiri na kuleta maendeleo finyu miongoni mwa wanajamii.

Jamii ya Wahiyao wa Lulindi wanatumia fasihi katika kuyaweka wazi matukio ya jamii hiyo. Kila jambo linalotokea linawekwa wazi kwa kutumia nyimbo za jando na unyago Mulokozi (1999, kwa mfano kama suala la malezi ya mtoto, inapotokea mtu ameonyesha kutojali malezi ya mtoto wake hutungiwa wimbo na kiimbiwa wakati wa shughuli za jando na unyago. Kwa vile fasihi ni zao la jamii inajitambua na kuweza kuyarekebisha maovu yake.

Pia jamii inahimiza kuwepo kwa ndoa. Jamii ya Wahiyao wana dini zao za kiislamu na kikristo zinazohimiza mume kuoa na mke kuolewa kwa amri za Allah (S.W). Inapotokea mume au mke wa mtu amebainika kufanya mapenzi kinyume na maadili basi jamii ya Wahiyao wanalikemea kwa kuliimbia nyimbo za maonyo ili jambo hilo lisiendelezwe. Zipo nyimbo mbalimbali zinazowafundisha vijana kuogopa kutembea na waume au wake za watu. Madhara ya hayo ni kukitafuta kifo, kwa hali ya maisha ya hivi sasa ni kukaribisha janga la UKIMWI kwenye ndoa yenu. Na hatima ya UKIMWI ni kuziacha familia yatima.

Nadharia ya fasihi inatazamwa kama kiwakilishi cha jamii TUMI (1988). Fasihi inaelezea siasa, sera, utendaji kazi, desturi na mila za kabila husika. Fasihi ina mguso kwa jamii kisanaa. Jamii ya Wahiyao wa Lulindi wana siasa, sera, utendaji kazi, desturi na mila zao. Wana mgawanyo wa kazi kama wanaume wanashiriki kazi za kilimo, kutunza familia, kuwinda na kazi za ulinzi katika ukoo na wanawake kazi zao ni kupika, kulea watoto, kukata kuni, kufua nguo za baba na watoto, kuchota maji mtoni au visimani na kumtunza mume asitoke kwenda kutafuta chakula kizuri ashibe, pia wana mila zao kama kupeleka watoto jandoni na unyagoni, kufanya matambiko, kuzikana.

Nadharia ya fasihi huwakilisha uhalisia wa jamii (Ntarangwi, 2004). Fasihi huelezea uhalisia wa jamii. Fasihi huelezea ukweli wa matukio yanayojitokeza kwa jamii na kuyaweka wazi. Uhalisia huamini demokrasia kama hali ya maisha na malighafi inayoelezea maisha ni ya kawaida katika maisha ya kila siku ya jamii. Uhalisia unaangalia matukio na matokeo ya matukio hayo yanavyothibitika. Fasihi ina kazi ya kuyaweka matukio ya jamii katika ulimwengu wa kawaida na wa kweli ambao unaelezea uhalisia wa yale yanayotendwa na jamii. Mara zote yanayoelezwa katika fasihi ni uhalisia wa maisha ya jamii inayoandikiwa fasihi hiyo (Senkoro na Kahigi, 2002).

Fasihi inamfundisha mtu mwenye kuitaka lugha. Kila lugha ina muundo wake, na muundo wa lugha unategemea mahitaji ya jamii hiyo. Fasihi inazingatia ni muundo gani utumike ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii yake. Utafiti unatueleza kuwa jamii ya Wahiyao wanatumia lugha ya Kihiyao katika kutoa mafunzo ya jando na unyago.

Dorson (1968) kwa kusema kuwa kila neno lina asili yake kutegemeana na wakati uliopo. Fasihi ina tabia ya kubadilika kutegemeana na matukio ya jamii. Kinachozungumziwa kwa wakati huo ndicho kinachotarajiwa na watu kwa wakati huo. Asili ya lugha ya kifasihi ni matukio yanayojiri jamiini na mahitaji ya jamii husika. Nyimbo zinaweza kuimbwa kutegemea na mahitaji ya jamii. Kwa nini jamii inahitaji watu wake wajengeke na nchi? Wanahitaji mambo gani yarekebishwa kulingana na wakati uliopo na mahitaji ya jamii? Hii inatokana kuwa jamii kila siku inahitaji mahitaji tofauti na jana ili kuendesha maisha yake kisawasawa.

### 3.7 Nadharia ya Kiafrika

Nadharia ya Kiafrika inaangalia waafrika na Uafrika wao, na mambo yao. Afrika inajali kazi Sengo (2009) ina mengi yanayofanya, lakini kazi ndiyo kipimo cha utu wake na ndiyo msingi wa maisha bora. Fasihi ya kiafrika inasisitiza mtu asichague kazi. Kazi ni kazi, kazi ndicho kitivo cha uhai wa mtu. Kila mtu amejaaliwa kazi yake kuanzia utopasi hadi uprofesa.

Fasihi inaweza kuelezeka kutegemea nyakati na mazingira mbalimbali; Kuna fasihi ya Kiulimwengu (*world wide literature*), ya kimabara, na fasihi ya kiafrika. Fasihi ya Kiafrika ni fasihi inayoshughulikia jamii na mazingira ya kiafrika. Fasihi hiyo inazungumzia ukoloni mkongwe, umasikini, ukoloni mamboleo, vita vya wenyewe kwa wenyewe nakadharika. Mgogoro mkubwa unaoikumba fasihi ya Kiswahili; ni nani ni Mswahili?

Mvungi (1982) anasema, kila jamii ina utaratibu wake na mambo yake yanayoendesha maisha yake. Afrika kama jamii ina watu wake, viongozi yake, kazi

zake na utaratibu wake wa maisha. Kila jamii ingependa ijitawale na kuendesha mambo yake. Nadharia hii ikijengeka italeta manufaa makubwa kwa jamii kiuchumi. Hakuna uchumi unaoletwa kwa maneno bali kazi ndiyo hukuza uchumi wa mtu na Taifa kwa ujumla wake. Fasihi inahimiza kazi kwa kila jamii. Inafichua uozo uliosakini miongoni mwa wanajamii. Uvivu ni adui mkubwa kwa jamii yoyote.

### 3.8 Nadharia ya Fasihi Simulizi

Nadharia ya fasihi simulizi inazingatia zaidi tanzu na fani ambazo zimegawanyika kwa kusadifu matumizi ya mtindo wa lugha zilizotumika kuzisawilisha. Mitindo ya lugha katika fasihi simulizi iko ya kinathari. Mtindo wa kishairi ni wa kutumia mapigo kwa utaratibu maalum. Kuna mtindo wa mashairi unaotumia urari wa vina na mizani. Vina ni silabi za mwisho za kila nusu mstari wa shairi, na mizani ni idadi ya silabi zilizomo kwenye mstari wa shairi au utenzi (Msokile. 1992).

Mashairi mengine ni yale yasiyofuata urari wa vina na mizani. Mashairi haya pia huitwa mapingiti au masivina. Mtindo wa mashairi hayo unazingatia zaidi ujumbe unaotolewa kwa jamii husika. Binadamu walianza kuitumia fasihi simulizi ya awali baada ya kumudu lugha ya mazungumzo. Lugha hiyo ilifungamana na mwigo wa sauti za zana za kazi milio ya wanyama pamoja na sauti za vishindo vya kazi mbalimbali walizokuwa wanafanya. Lugha hizo zilimsaidia mwanajamii kupambana na mazingira alimokuwa anaishi Senkoro (1987).

Mfumo wa fasihi simulizi ulilenga zaidi kurithisha mila, desturi na utamaduni wa jamii kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Fasihi ilizingatia uwepo wa hadhira na fanani kwa pamoja. Fasihi simulizi kwa wakati huo ilihifadhiwa kichwani na

kurithishwa kwa kila kizazi. Jinsi fasihi simulizi ilivyoendelea kurithishwa, ilipoteza baadhi ya maadili kutokana na sababu ya udhaifu wa uhifadhi. Kusahaulika kwa baadhi ya maadili, hakukufanya kupoteza utamaduni wa jamii kwa vile bado ulikuwa haujaingiliwa na utamaduni wa kigeni. Mmiliki wa fasihi simulizi ni wanajamii wote.

Kirumbi (1976) ameeleza juu ya fasihi na itikadi, kuwa fasihi humtazama binadamu na uhusiano wake na binadamu wenzake na mazingira yake pamoja na viumbe wengine na itikadi waliyonayo kuhusu mambo ya kiroho kama pepo, maruhani, mashetani, majini na miungu. Fasihi humzingatia binadamu katika hali yake ya upweke, furaha, huzuni, raha, taabu, shida, mashaka na jinsi anavyochanganyika na wengine. Fasihi ni kioo na mwozi wa maisha ya jamii, hivyo ni sehemu ya utamaduni wa jamii.

Fasihi huchota mawazo kutoka kwa jamii yake Nkwera (1978). Kazi zake hubaki kuwa mali ya jamii. Fasihi humtazama binadamu na mazingira yake na kumfanya binadamu huyo ayaangalie mazingira hayo kwa udadisi kwa lengo la kumfanya afikirie kwa manufaa yake. Historia ya jamii imegawanyika katika mifumo ya kiitikidi Mapunda (1979) itikadi hizo zimezingatia maisha ya jamii katika uzalishaji mali na mahusiano ya tabaka katika jamii kwa wakati uliopo na maendeleo yake.

Mlacha (1995) anasema fasihi simulizi ni nyanja ya maisha ya jamii na ambayo huchangia kuendeleza na kudumisha historia ya jamii husika. Fasihi similizi inaelimisha jamii juu ya asili chanzo na maendeleo ya utamaduni na maisha ya jamii husika. Ni chombo muhimu cha jamii kwa vile ndani yake kuna ubunifu unaoibua

nadharia ya kijamii, kiuchumi na kisiasa (Kimani, N.2006). Fasihi simulizi ni uti wa mgongo wa maendeleo ya jamii. Huipasha jamii juu ya utamaduni wake, historia ya jamii, mtazamo na matazamio ya jamii hiyo (Wamitila, 2003).

Jamii hapo awali ilikuwa na upeo mkubwa katika kutawala mazingira yake. Waliishi kwa kuzingatia miiko (Kisanji, 2011). Maadili yalitolewa kwa ajili ya miiko, kwa mfano mama mjamzito alipewa maadili ya kutunza mimba kwa kupewa miiko ya ujauzito kama kutokula vyakula vinavyomuongezea uzito mtoto kama mayai kwa madai kuwa, akila mayai atazaa mtoto asiyekua na nywele (Makumbusho ya Taifa la Tanzania, 2003).

Miiko hiyo iliwasaidia kuepuka mama kufanyiwa upasuaji wa kujifungua mtoto kwa vile kwa kipindi hicho teknolojia hiyo haikuwepo katika jamii zetu. Jamii ya Wamwera wana miiko inayowafundisha akina mama kutofanya mapenzi na mwanaume asiyetahiriwa na ambaye hajapitia mafunzo ya jando. Sababu kubwa ni kuwafanya akina mama wasiweze kuambukizwa na magonjwa, kwani mwanaume asiyetahiriwa ana uwezekano mkubwa wa kuhifadhi magonjwa kama kisonono na kaswende. Pia jamii ina miiko ya kutoolewa au kuoa mtu wa kutoka ukoo mmoja. Sababu kubwa ni kwamba wanaamini kuwa watu wa ukoo mmoja ni ndugu moja hata kama hamjazaliwa baba na mama mmoja. Hiyo inasaidia kuepuka kuzaa watoto wenye matatizo yanayofanana kama vichaa, kifua kikuu na kuzaliwa vilema (Nyagali, 1990).

Mfano mwingine wa kabila la Wanyaturu mkoani Singida; Mila na desturi zao pia zilielekeza baadhi ya miiko kama mama akishajifungua mtoto haruhusiwi kuishi na

mume wake kwa kipindi cha miaka miwili hadi mitatu. Wao wanaamini kuwa kwa kuishi pamoja kunaweza kuharibu mtoto kwa kutokukua vizuri au kupoteza maisha ya mtoto. Hivyo mama anaishi kwa wazazi wake hadi mtoto huyo akue.

Mfumo wa utumwa ulifuata. Matabaka yalianza kujitokeza katika mfumo huu, kulikuwa na mabwana ambao ni tabaka tawala na watwana ambao ni tabaka lililozalisha kwa ajili ya mabwana. Mfumo ulikuwa na vyombo vya dola kama polisi, mahakama na jeshi. Itikadi ilikuwa inatetea maslahi ya tabaka tawala. Fasihi simulizi inatueleza kuwa kila jamii ina matabaka. Kuna mabwana na watumwa, kila mtu anatumikia tabaka lake Kikamilifu. Tabaka la Watumwa huunda au kuanzisha kazi za fasihi kama nyimbo na mashairi yanayootetea maslahi yao (Senkoro, 1987). Jamii ilipinga mfumo huo wa kinyonyaji kwa kuwaunganisha wanajamii wenye kuzungumza lugha moja ili kuondoa unyanyasaji huo.

Mfumo wa umwinyi ni mfumo unaotawala uchumi na utamaduni wa jamii husika. Fasihi ya wakati huo ilikuwa na falsafa iliyowatenga wenye nacho na wasionanacho. Wenye nacho walimiliki njia kuu za uchumi kwa jamii (Senkoro, 1987). Mfumo wa umwinyi ulileetwa na wageni kutoka bara la Asia, ambao walikuja katika jamii zetu kwa shughuli za kibiashara katika pwani ya Afrika Mashariki. Mfumo uliabudu au kutetea zaidi mapambano, urembo, majumba ya kifahari na starehe au anasa anuwai. Unamchukulia mwanamke kama pambo. Ni mfumo unaomdhalilisha mwanamke. Mwanakupona Binti Mshamu (1858) anadhihirisha itikadi ya kimwinyi.

Katika utafiti wetu tumeelezwa kuwa jamii ya Wahiyao wa Lulindi, wana itikadi ya umwinyi. Kila ukoo una mwinyi wake. Kuna mwinyi Machemba, Akululindi,

Akutukulu,na Akuchisanga. Mwinyi aliheshimiwa na kuaminiwa, alipewa mamlaka ya kuamua jambo katika ukoo. Alihudumiwa kwa kupewa mali kama chakula, mifugo na pesa. Kutokana na majukumu yake hakuweza kufanya kazi za kiuchumi zaidi ya kusuluhisha migogoro na kuiongoza jamii. Pamoja na yote Mwinyi alipewa jukumu la kuwalea wajane kama wake zake pamoja na watoto yatima. Mwinyi alikuwa na uwezo mkubwa kiuchumi. Tulifanya mahojiano na Mwinyi "Chisanga" kujua kama jambo hili bado linaendelea alijibu kuwa siku hizi hakuna kurithi mke ni mila iliyopitwa na wakati. Na kutokana na hali ya kuyumba kwa uchumi duniani hakuna tena mwanajamii anayewajibika kutoa sehemu ya mali yake kwa Mwinyi. Alisema bado umwinyi upo, kwani kazi yake bado ipo palepale ya kuiongoza jamii na ukoo wake.

Kama Mwanakupona alivyomuasa binti yake, Wahiyao wanawafundisha mabinti zao wakiwa jandoni kumtukuza mume kwa kumpa mapenzi mema kwa kumpikia chakula ale ashibe ili isitafute kwa kwenda kula, kumuheshimu na kumtii, ili kuwa mke bora. Kwao Wahiyao mwanamke ni chombo cha kumstarehesha mwanamume na anafundishwa maadili mema yatakayomfanya adumu kwenye ndoa yake hadi Allah (S.W) atakapompa umauti wake.

Akiwa unyagoni mwanamke anafundishwa nyimbo mbalimbali zinamwongoza kujua tabia za wanaume kwa wake zao na maadili mengine kama kumueleza kuwa atakapoolewa ni lazima atabeba ujauzito na kuzaa. Na hivyo anafundishwa athari za kuzaa katika viungo vyake kuwa sasa anatoka katika usichana na kuwa mama. Pia anafundishwa kutomshawishi mume wake kujamiiana akiwa na mtoto mdogo kwani anaweza kuzaa kabla mtoto hajakuwa.

Kuna nyimbo zinazowafundisha mabinti kuwa matokeo ya kufanya ngono ni kupata ujauzito. Na ujauzito unaambatana na kuugua na hivyo ni vyema kufanya ngono ndani ya ndoa ili kupata mume atakayeweza kumsaidia pindi atakapoanza kuugulia ujauzito. Kuna nyimbo zinazomfundisha binti akiwa unyagoni dalili zinazojitokeza kuwa tayari anataka kujifungua mtoto kwa muda ule ili ajiandae kwa kutayarisha nguo za kuvaa mtoto na kujihifadhi yeye mama.

Mfumo mwingine ni ule wa ubepari. Itikadi ya mfumo huu inazingatia uzalishaji mali. Fasihi katika mfumo huu ni chombo cha uzalishaji mali. Msingi mkubwa wa ubepari ni mtaji. Kila kinachozalishwa ni bidhaa. Fasihi katika mfumo huu haitumikii jamii kwa uaminifu. Msanii anajitenga na jamii yake. Ni mtu aliyevaa uso wa udanganyifu. Jambo muhimu kwake ni kupata pesa, na si kuelimisha jamii ili iondokane na unyonge aliokuwanao (Senkoro 1987).

Msanii anachota malighafi ya maudhui na fani kutoka popote hata kama ni hewani. Katika kuifanya kazi yake ipendwe na watu wengi na iuzike kwa jamii, ni lazima iongeze utamaduni wa kigeni unaopendwa na watu au kundi fulani la jamii. Mfumo unamtenga mwanajamii na uhalisia wa matatizo yake. Mfumo hauelekezi juu ya maadili mema yanayohitajika na jamii, badala yake mwanajamii anaiga tabia na mwenendo wa jamii za kimagharibi ambazo ni maadili tofauti na maadli yetu ya kiafrika.

Fasihi katika mfumo wa kibepari, mwanamke ni chombo cha kufanikisha uzalishaji mali. Lengo ni kutaka wanawake hao wawe wazalishaji hasa katika kazi za kilimo. Fasihi katika mfumo wa ubepari haushughulikii matatizo ya msingi ya jamii.

Haionyeshi migongano ya kitabaka iliyopo. Mifumo yote inaelekeza mfumo mmoja kwa ajili ya jamii. Kuwa kila jamii inahitaji kuishi vile itakavyo. Hakuna jamii inayoweza kuielekeza jamii nyingine iishi kama inavyoishi jamii nyingine kwa vile kila jamii inamahitaji yake kwa haja zake.

### 3.9 Nadharia ya Kitanzania

Nadharia ya Kitanzania inasisitiza kuwepo kwa fasihi ya Kitanzania. TUKI (2000) amesema kuwa fasihi ya Tanzania inaangalia utamaduni wa Kitanzania. Kwa mfano ,kuna kazi mbalimbali za fasihi zilizoandaliwa na Watanzania na ambazo zimetumia lugha ya Kiswahili, na kuelezea maisha na utamaduni wa Mtanzania kama kazi za akina Kiango, Mbogo, Sengo, Balisidya, Shaaban Robert,na wengine. Lugha inayotumika kufikisha ujumbe ndiyo kigezo kikubwa cha kuiita fasihi hiyo kuwa ya Tanzania. Lugha ya Taifa inayotumika Tanzania ni Kiswahili. Kwa hiyo Fasihi ya Tanzania inasambazwa kwa lugha ya Kiswahili.

Kwa vile fasihi inachota mawazo kutoka kwa jamii, basi inafuata utamaduni wa jamii husika. Katika Tanzania kuna makabila mengi, na kila kabila lina utamaduni wake. Na hivyo ni vigumu kushawishi kuwa fasihi ya Tanzania ni fasihi ya Kiswahili kwa vile jamii za Tanzania ni nyingi na kila jamii ina utamaduni wake, na utamaduni unajuisha Lugha inayotumiwa na jamii husika basi fasihi ya Tanzania ni ya jamii ya Tanzania ikiwa na lugha zake za kimakabila na lugha ya Taifa ya Kiswahili.

Lugha ya Kiswahili ni lugha ya Taifa la Tanzania. Taifa ni watu wa makabila mbalimbali kama Wamakonde, Wahiyao, Wamakuwa, Wachaga, Wasambaa nakadharika. Taifa kama jamii moja (Tanzania) linaunganishwa na lugha ya

Kiswahili. Tunapotaka kuelezea mila, desturi na mali za Tanzania, kama jamii moja tutatumiya lugha ya Kiswahili. Kwa mtazamo wa Sengo (2009) fasihi ya Kiswahili ipo.

TUKI (1978) wameandika kuwa mtazamo wa fasihi Kiafrika (Kitanzania) ni mtazamo unaoongozwa na Sengo unapingana kimsingi na mitazamo mingine kuhusu fasihi na maisha kwa ujumla. Lengo la Sengo ni kuzalisha nadharia ya fasihi itakayozingatia "Uafrika". Anaposema 'Nadharia ya Kiafrika itajengeka na kudhihirika baada ya uchunguzi mkubwa wa fasihi simulizi ambamo ndimo mlimo na kunga na siri kuu za nadharia zetu"

Ushahidi wa mtazamo huu umepatikana katika utafiti kwa kabila la Wahiyao kuhusu jando na unyago. Umeelezwa kuwa siri ya nyimbo za jando na unyagoni ni kuwa ndani yake kuna fasihi simulizi kubwa iliyojificha. Kila jamii ina maadili yake yanayofundishwa. Kama jamii ya wawindaji na wafugaji watafundisha uwindaji. Hivyo kila jamii ina kunga na siri yake katika fasihi simulizi. Kila jamii inategemea fasihi simulizi yake, kulingana na mahitaji yake. Msingi mkubwa wa fasihi kwa jamii ni kuiweka jamii yake sawasawa na kuitenganisha na jamii nyingine.

Nadharia hii itajengeka endapo Waafrika tutajitambua, kuutambua na kuuthamini Uafrika wetu. Kwa jamii ya Wahiyao inaelekeza vijana kutenda kulingana na mahitaji ya mila na desturi za kihiyao.

### 3.10 Nadharia ya Kiulimbe

Nadharia ya kiulimbe inapingana na nadharia ya fasihi simulizi. Fasihi simulizi ni zao la jamii. Huchota mawazo kutoka kwa jamii husika. Nadharia ya kiulimbe

inazingatia zaidi mabadiliko yanayotokea duniani. Inajadili fasihi simulizi kisayansi. Uwasilishaji na utendekaji wake ni wa kisayansi na teknolojia. Inazingatia matumizi ya kompyuta katika kuwasilisha fasihi simulizi. Inatumia pia kanda za kaseti, za video na runinga katika kuwasilisha kazi ya fasihi.

Fasihi simulizi katika teknolojia mpya inatumika katika kuhifadhi, kuiwasilisha, kuikosoa na kuburudisha jamii. Kuwepo kwa teknolojia hii inasaidia kuwasilisha ujumbe kwa jamii kwa sehemu kubwa kwa wakati mmoja. Uwasilishaji huu unamtenga fanani na hadhira. Hadhira ina kazi ya kupokea tu kile kinachoelezwa bila hata ya kuhoji. Jambo ambalo kwa jamii inaweza kujifunza maadili tofauti na yale yaliyotarajiwa na jamii hiyo. Uhifadhi huu ni wa kudumu kwa muda mrefu kutokana na kuwepo kwa kumbukumbu ya muda mrefu ambayo kila kizazi kinaweza kurithishwa kile kilichokusudiwa.

Fasihi simulizi katika ulimbe inatumika kuikosoa jamii kwa kufichua maovu yanayojitokeza. Kwa mfano, katika runinga, na kanda za video tunaonyeshwa michezo ya kuigiza inayoelezea maisha ya jamii. Maisha hayo yanaweza kuwa ni yale yanayofanywa kinyume na matakwa ya jamii na mengine yanayofundisha jamii ukweli wa maisha ya jamii. Hata hivyo si maadili yote yanayoonyeshwa kuwa yako sawa na yale yanayofundishwa katika vyuo vyetu vya asili ambavyo vinatoa mafunzo ya jando na unyago. Kila jamii ina maadili yake yanayofundishwa kulingana na mahitaji yake. Hivyo teknolojia mpya haiwezi kukidhi matakwa ya kila jamii.kinachofundishwa kinalenga jamii zote kwa ujumla.

Fasihi katika nadharia hii hakuna staara iliyojengwa na jamii kulingana na mahitaji yake. Kwa mfano, kuna matumizi ya picha za ngono katika sinema zinazoonyeshwa

katika intaneti ambazo kila mmoja katika jamii bila kujali mkubwa au mdogo ana uhuru wa kuziangalia, na hakuna uhalisia wa yale yanayofundishwa kiasi cha kupoteza maadili ya jamii zetu kwani unakuta vijana wengi wanajaribu kufuatisha yale yanayoonyeshwa kiasi cha kupoteza maadili ya jamii zetu za kitanzania.

Jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao ni elimu ya mafunzo ya siri kwa faida ya baadaye ya kiutu uzima ya kijana. Mafunzo wanayoyapata kutokana na kukuwa kwa sayansi na teknolojia, vijana wanatumia maarifa hayo kwa kuhawilisha na kile alichojifunza jandoni. Matokeo ya hayo ni kumomonyoka kwa maadili.

### 3.11 Nadharia ya Kiafya

Nadharia ya kiafya inaangaliwa na fasihi simulizi kama njia mojawapo ya kuimarisha afya ya wanajamii fulani. Jamii ya Wahiyao wa Lulindi wana jando na unyago. Dhima mmojawapo ya jando ni kuwatahiri vijana wa kiume. Kutahiri kunaweka via vya uzazi vya kijana wa kiume safi kwa kwa kuondoa sehemu ya ngozi inayozunguka via hiyo. Kutolewa kwa sehemu hiyo ya ngozi, Wahiyao wanaamini kuwa kijana anaweza kuzaa watoto. Kwamba sasa hakuna kikwazo cha uzazi wake na pia anakuwa safi.  Kwa kijana wa kike inawafundisha kuwa safi wanapokuwa katika hedhi na wakati wote wa maisha yake. Kuwa safi kunampunguzia maradhi mwilini mwake. Kwa Wahiyao wa Lulindi wanaamini kuwa binti anapokuwa msafi ni rahisi kuolewa.

Nadharia ya kijamii ambayo inaangalia hali halisi ya maisha ya jamii,na nadharia ya fasihi simulizi ambayo fasihi simulizi ni zao la la jamii,ni chombo kinachotumika

kumkosoa mwanajamii katika jamii yake, ndizo nadharia zilizotumika kukamilisha utafiti huu. Utafiti unatoa ukweli kuwa:

(i) Nyimbo za jando na unyago ni Chuo cha kutolea elimu ya awali kwa maisha ya Jamii ya Wahiyao. Chuo mbadala, ikiwa ni sehemu ya jamii ya kuwakuzia vijana na mabinti kuwa watu wazima kiurombo. Wasukuma wamekiri kuwa hawakuwa na jadi ya kutahiri wanaume (Mayala, 2009) ila kwa sasa baada ya kuadibishwa na mabinti wa Kiswahili – Mwambao (Sengo, 2009) ndipo wanakwenda kwa matabibu kuwekewa sawa mambo yao.

(ii) Kwa vile jando na unyago ni sehemu ya fasihi simulizi, basi hata mtu mzima aliyekosa kufundwa lazima afundike pale anapokwenda kinyume na maadili na mafundo ya nyimbo za jando na unyago.

(iii) Jando na unyago ni Chuo cha mafunzo ya jamii kwa kutumia nyimbo katika kutoa mafundo na adhabu za jamii. Kijana hupewa mafunzo juu ya usafi wa mwili na mavazi. Kama vile watoto hufunzwa kunawa maji baada ya kujisaidia badala ya kusota, hufundishwa kuvaa nguo za heshima mbele ya baba, na mama.

Binti anafundishwa kuvaa nguo zisizoonyesha viungo vyake hasa vya siri mbele ya baba, mjomba, kaka na watu wengine wenye heshima au wakubwa zake. Pia wanafundishwa kuwa na siri kwa kila jambo lisilohitajika kujulikana na wengine nje ya familia yao. Wanafundishwa kuogopa vitu vya watu. Kwa watoto wa kiume wanafundishwa kutofanya mapenzi na mke wa mtu pindi atakapo balehe, kwani ni kujitafutia kifo.

Mkabala wa kimaadili na mkabala wa kiushumuzi hukamilisha mawasiliano na uhusiano kwa wanajamii. Nadharia hii inafaa kwa sababu nyimbo zinapoimbwa hukutanisha watu wengi na hapo ndipo uhusiano wa kijamii hukuzwa. Kwa hiyo, katika utafiti huu nadharia ya "Uhalisia wa Kiafrika" Ambayo iliasisiwa na Prof.Sengo 2009 imetumika katika kukamilisha kazi hii. Nyimbo zilizokusanywa zimeitumia nadharia hii katika kutafutia siri za nyimbo za jando na unyago za Wahiyao.

# SURA YA NNE

# 4.0 MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

## 4.1 Muundo wa Utafiti

Kothari (1993) ametoa tafsiri ya muundo wa utafiti kuwa ni dhana ya kinadharia inayomuongoza mtafiti wakati wa kufanya utafiti, kukusanya taarifa, kuzipima na kuzifanyia uchambuzi. Keya na wenzake (1999) wameeleza kuwa muundo wa utafiti ni jumla ya hatua zitakazotumika katika utafiti kutoka mwanzo hadi taarifa yenyewe, ambazo ni hatua ya kukusanya data, kuzichambua na kuzipima ili kupata ukweli wa tatizo. Katika utafiti huu tumetumia muundo wa kukusanya data na kuzichambua na kupata taarifa kamili ya tatizo.

## 4.2 Mbinu za Utafiti

### 4.2.1 Mbinu ya Usaili

Katika utafiti huu, tumetumia mbinu ya usaili. Hii ni njia inayokusudia kukusanya taarifa za kutosha kwa kundi kubwa kwa muda maalumu. Ni mbinu inayojumuisha takwimu za matatizo zinazotokana na idadi kubwa ya watu. Best na Kahn (1998) wameeleza usaili kuwa ni majibizano ya watu wawili yenye lengo maalumu la mtafiti kupata taarifa zenye ushahidi, inajumuisha ukusanyaji wa taarifa kutokana na mazungumzo ya moja kwa moja kati ya mtu na mtu.

Denscombe (1998) ameeleza kuwa usaili unajumuisha utambuzi na ufahamu kuhusu jambo linalosailiwa, ambalo ni muhimu na halina masihara. Usaili ni mzuri kwa sababu ni rahisi kubadilisha swali kama swali lililoulizwa halijaeleweka au gumu kulijibu. Denscombe (1998) amehadharisha kuwa msailiwa anaweza kujiona kama

amekerwa, kama vile amelengwa yeye, akaona aibu au akasisimka, akajisikia vibaya kujibu. Wakati huo anaweza asiwe tayari kujibu maswali au swali linaloweza kuwa na makosa kiasi cha kumfanya msailiwa kuchukuwa muda mrefu kulijibu.

Kwa upande mwingine, Keya na wenzake (1989) wameeleza kuwa mwelekeo binafsi wakati wa usaili unasababishwa na hali ya msaili jinsi alivyo, tabaka, jinsia na umri wake. Kwa hiyo, msailiwa anatakiwa kujiamini na kuwa makini. Kidadisi kinaweza kuwa na maswali ya kuandika au maswali tu ya kujibiwa. Katika utafiti huu tumetumia maswali huru ya kupata taarifa kutoka kwa makungwi 5 kwa majando 5 na kumbi 5 za unyago. Maswali yaliyoulizwa kuhusu jando na unyago, yalikuwa maswali ya kujibu na siyo ya kuandika. Majibu yaliyopatikana katika usaili huo yameonyeshwa kwenye jedwali la matokeo ya utafiti (tazama jedwali la pili).

### 4.2.2 Mbinu ya Hojaji

Mbinu ya hojaji katika kukusanya data inampa mwongozo anayehojiwa kujibu maswali akiwa pekee. Minduva (2004) katika Keya na wenzake wameeleza kuwa hojaji ni muundo wa maswali yanayoandaliwa kulingana na malengo ya utafiti. Ni maswali sawa na ya usaili ila usaili ni wa uso kwa macho na hojaji ni la kutafutiwa karatasi na kalamu au na kirimbo.

Pia Minduna (2004) katika Enon (1998) ameeleza kuwa sababu kubwa ya kuandaa hojaji ni kupata ushahidi wa utafiti kutokana na maelezo ya mtu binafsi juu ya jambo linalofanyiwa utafiti. Mbinu hii inatumia muda na pesa nyingi katika kuandaa na kuyasambaza mahojaji. Ameeleza pia, kuna uwezekanao wa kukosa uwezo wa kuyasafirisha ama vyombo vya kusafirishia na pia urudishwaji wa mahojaji

kucheleweshwa, kutorudishwa kabisa na/ au kurudishwa bila kujibiwa. Hali hiyo inaweza kumfanya mtafiti kushindwa kupata taarifa za kutosha au kukosa taarifa kabisa.

Denscombe (1998) anatahadharisha kwamba hojaji ina upungufu wake. Miongoni mwa upungufu huyo ni kuwa kuna wakati muhojaji anaweza kuelemea upande mmoja wa maoni. Au wakati fulani anaweza kuona aibu kutokana na hali ya mtu kuwa mwanamke kama muhojaji ni mwanaume, au mwanaume kuhojiwa na mwanamke, au kijana kumuhoji mzee, au wakati fulani muhojaji akakasirishwa akakosa subira, au akapata msisimko kutokana na mavazi aliyovaa mtu anayehojiwa. Wakati wa utafiti Mtafiti amefanikiwa kuwahoji vijina 50 wa kike na 50 wa kiume waliopitia jando na unyago. Vijana wote walirudisha hojaji.Hii imesaidia kukidhi haja ya utafiti kama ilivyokusudiwa. Pia tuliwapa hojaji wazazi 25 wa kiume na 25 wa kike waliopitia jando na unyago ili kuweza kujaza na kutupatia taarifa iliyotarajiwa kutoka kwenye kumbi za unyago 5 na majando 5, kati ya vijiji 10 vilivyotarajiwa.

Mbinu hii ilitumika kupata uhalisia wa nyimbo za jando na unyago pale tulipotembelea kumbi za jando na unyago kujionea yale wafanyayo wao kwa wao. Mbinu hii iligharimu muda hadi kukubaliwa kuingia jandoni ambako wanawake hawaruhusiwi kuingia jandoni hapo. Takribani ilichukua siku nne, baada ya vikao vya kamati za watendaji za kijiji na kamati ya jando na unyago kukubaliana na kuona umuhimu wa jambo lenyewe. Pia kulikuwa na makubaliano kati ya warombo, mangariba na wazazi hadi kuruhusiwa kuingia na kufanya mahojiano.

### 4.3 Mbinu ya Ushiriki/Umakinifu

Enon (1998) ameeleza kuwa hii ni mbinu ya ukusanyaji data kwa mtafiti kushiriki mwenyewe katika kuhisi na hali zote za jamii. Ni njia inayovutia kwa mtafiti kwani kuna uwezekano wa kupata taarifa za moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa, hasa baada ya kuzoweleka na kuchukulika kana kwamba yu mwenyeji mwenzao. Best na Kahn (1993) wamesema kuwa umuhimu wa njia hii ni kwamba mtafiti anajionea mwenyewe vitu mbalimbali vinavyoambatana na mila kadhaa na kwa hiyo mtafiti anapata nguvu na uwezo wa kukusanya data.

Cohen na Keith (2001) wamesema kuwa ushiriki unamfanya mtafiti avutiwe kukusanya takwimu za moja kwa moja kutoka kwenye tukio halisi. Katika utafiti huu, mtafiti ameshiriki moja kwa moja kusikiliza nyimbo zilizokuwa zinaimbwa na vijana, pamoja vitendo vinanyifanywa jandoni na unyagoni.

Morrison (1993) amesema kuwa uchunguzi unamwezesha mtafiti kukusanya taarifa kutoka kwenye chanzo hasa kutoka ndani ya mazingira ya shughuli za kiuchumi na za jamii. Udhaifu wa njia hii ni uwezekano wa kushindwa kupata tafsiri sahihi ya jambo linalotendeka ukilinganisha na jambo linalotafutwa kulingana utafiti wako. Kwa mfano lugha inayotumika kwa watafitiwa na vitendo vinavyofanyika. Katika utafiti huu maswali yaliulizwa pale ambapo mtafiti alishindwa kuelewa tarjima yake kwa kile kilichokuwa kinaelezwa, mkarimani wake alitoa tarjima.

Katika utafiti huu mbinu ya ushiriki /umakinifu imetumika kwa kwenda jandoni na unyagoni na kuongea na vijana walioko jandoni, waliopitia jando na unyago, makungwi na mangariba pamoja na manyakanga.

Utafiti umechunguza shughuli za jando na unyago zinavyoendeshwa na jamii ya Wahiyao wa Lulindi Masasi na namna nyimbo zake zinavyoathiri maisha yao kwa kutilia maanani nadharia, mbinu na njia za Sengo (2009) za "Ndani –Nnje, "Uhalisia wa kiafrika na Kila fasihi ina Kwao"

Uhalisia wa kiafrika unajieleza pale kila jamii inapoelezea utamaduni wake. Utamaduni ni pamoja na lugha inayotumika na jamii hiyo, aina ya mavazi yanayovaliwa chakula kinacholiwa pamoja na mila na desturi za jamii hiyo. Kama wahiyao wa Lulindi wanavyoitumiya mila na desturi yao ya kutoa elimu kupitia Chuo chao maalumu cha jando na unyago. Makabila mengi hapa Afrika yana mila hii ya jando na unyago. Ndiyo Chuo pekee cha kutolea elimu ya jadi. Ni Chuo cha mwanzo kabisa cha kutolea maadili ya ki-utu uzima.

Sengo (1978) ameeleza umuhimu wa mwaafrika kutukuza fasihi yake badala ya kuiga fasihi ya kigeni ambayo haina manufaa kwetu. Lengo la fasihi ya kiafrika ni kumkomboa Mwafrika kutoka katika utumwa wa kutawaliwa kimwili na kifikra. Dhima ya fasihi ya Kiafrika ni kumjenga kijana katika maisha ya kiafrika asilia (Sengo 2009) ili popote awapo awe ni kielelezo cha jamii ya kiafrika.

## 4.4 Njia za Utafiti

Katika utafiti huu njia ya kukusanya data za mafunzo ya nyimbo za jando na unyagona kuzichambua data hizo ili kujua.

## 4.5 Uteuzi wa Watafitiwa

Utafiti umezingatia uteuzi wa makundi tofauti ya wanajamii waliopitia mafunzo ya nyimbo za jando na unyago. Kila kundi limepewa jukumu lake la kukamilisha utafiti

huu. Eneo la Tarafa ya Lulindi ni kubwa. Na hivyo utafiti umeteua kufanya utafiti tarafa hiyo kwa kuteua vijiji vya Lulindi madukani, Ndwika, Chiwambo, Namajani, Mpopo, Mkaseka, Msanga, Mburusa, Mitesa, na Mtakuja.

Minduva (2004) kutoka Best na Khan (1993) kwa yao waliyoyasema wamesema kuwa uwingi wa watu katika utafiti huu utazingatia watu watakaofanyiwa utafiti kwa niaba ya jamii nzima. Kwa jamii ya Wahiyao wameshirikishwa viongozi wa vijiji wakiwamo wenyeviti wa vijiji vitatu Lulindi, Luagala na Chiwambo, Makungwi, Diwani wa kata, Mtendaji kata, Ngariba, Warombo, wazazi na vijana waliopitia jandoni na unyagoni.

Minduva (2004) kutoka Cohen na wenzake (2001) wamesema uteuzi hufanywa kwa kundi dogo linalowakilisha kundi kubwa la watu ambalo linafanyiwa utafiti. Mueller (1970) yeye amesema sababu ya kutumia kundi dogo kuwakilisha kundi kubwa kiutafiti ni kupunguza gharama ili kukidhi mahitaji na muda. Keya na Colleques (1989) wameongeza kwa kusema hii inatokana na hali ya kifedha na ya mazingira ya kundi hilo linalofanyiwa utafiti.

Enon (1998) amesema kuwa, uwakilishi wa kundi dogo la watu ambao anawatumia mtafiti ni ile hali ya mtafiti kuchaguwa wawakilishi kwa kuzingatia malengo maalumu. Mtafiti anachagua matatizo ambayo yalihusisha kundi la vijana tu kwa kuzingatia utoaji wa maamuzi ya ndani kabisa kutoka kwa wanajamii. Utafiti huu ulijumuisha uteuzi wa kundi dogo ambalo lilizingatia maamuzi na elimu ya mwanajamii.

Cohen na wenzake (2000) wamesema, katika uwakilishi wa kundi dogo la watu, kila mmoja atakuwa na nafasi sawa na mwenzake. Munn na Drever (1996) wamesema, njia hii inasaidia kupunguza upendeleo au ubaguzi katika utafiti. Pia ni njia inayotowa uhuru kwa mtafiti na watafitiwa. Enon (1998) ameeleza udhaifu wa njia hii ni muda mwingi unaotumika katika kukamilisha taarifa kutokana na hatua zinazofuatwa. Utafiti huu umeteua makundi matano ya watafitiwa kuwakilisha wanajamii wa Lulindi ili kupunguza muda.

## 4.6 Ubora wa Utafiti

Bali na wenzake (1998) wameeleza kuwa ubora wa utafiti ni namna ya mtafiti alivyo na fikira zake anavyozipangilia. Ubora wa utafiti ni kipengele muhimu katika kufanikisha utafiti. Enon (1998) ametoa ushauri wa mambo ya kufuata katika kuhakikisha kuwepo kwa ubora wa vifaa vya utafiti. Amesema ubora wa vifaa hivyo unategemea kipimo cha mwanzo hadi mwisho cha wakati wa utafiti (yaani tangu ukusanyaji wa data hadi uchambuzi wa data kulingana na tatizo la utafiti linaloshughulikiwa). Hii ni idadi ya vifaa na uwezo wa kuwashirikisha wanaotafitiwa na maelekezo yanayotolewa kwa wote wanaotumia vifaa hivyo vya utafiti.

## 4.7 Vifaa vya Kukusanyia Data

Katika utafiti huu vifaa mbalimbali vimetumika katika kukusanya data. Miongoni mwa vifaa hivyo ni:

### 4.7.1 Kirimbo

Kirimbo, kwa kurekodi mahojiano na nyimbo za jando na unyago. Nyimbo za jando na unyago zilirekodiwa jandoni na unyago ambako vijana walipatikana kwa muda

maalumu. Nyimbo zote ziliimbwa kwa lugha ya Kihiyao na zilirekodiwa hivyo hinyo bila kuwa na tarjima.

### 4.7.2 Ngamizi

Ngamizi, kwa ajili ya kuchapa au kucharazia kazi ya utafiti wa nyimbo za jando na unyago.

### 4.7.3 Kamera

Mtafiti alitumia kamera, kwa ajili ya kupiga picha maeneo ya shughuli za jando na unyago Utafiti huu ulikusudiwa kutembelea sehemu za jando na za unyago katika maeneo kumi (10) ya vijiji vya Lulindi Masasi. Maeneo hayo ni Lulindi madukani, Ndwika, Chiwambo, Namajani, Mpopo, Mkaseka, Msanga, Mburusa, Mitesa, na Mtakuja. Kati ya maeneo hayo,ni majando 5 na kumbi 5 za unyago zimefanikiwa kupata data zilizo kamili.

# SURA YA TANO

# 5.0 UCHAMBUZI WA DATA

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea eneo la utafiti, aina ya nyimbo zilizokusanywa, upungufu wa utafiti, uchanganuzi wa data pamoja na muundo wa lugha inayotumiwa na jamii ya wahiyao.

## 5.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu umefanyika Mkoa wa Mtwara, Wilaya ya Masasi maalumu Tarafa ya Lulindi. Kwa sababu eneo hilo ndilo linakaliwa na kabila la Wahiyao kwa asilimia kubwa katika Wilaya ya Masasi ukilinganisha na tarafa nyingine za wilaya hiyo. Ni eneo ambalo ni rahisi kutathmini juu ya mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kwa vile halina mchanganyiko mkubwa wa makabila mengine. Zaidi ya hayo, Tarafa ya Lulindi, ina eneo kubwa ambalo limetupatia data za kutosha kutokana na ukubwa wake na kuufanya utafiti huu kuwa wa uhakika.

## 5.3 Aina ya Nyimbo

Katika utafiti wetu tumekusanya nyimbo za aina tatu za jando na unyago kutoka vijiji kumi vya tarafa ya Lulindi kwa ajili ya uchambuzi wa utafiti huu. Nyimbo zilizokusanywa ni za jando, za unyago za vijana waliokaribia kubalehe na kuvunja ungo kwa lengo la kuwatoa utotoni na kuwaandaa maisha ya kiutu uzima, nyimbo za vijana waliobalehe na kuvunja ungo ambao wanaandaliwa kwa maisha ya kuoa au kuolewa na nyimbo za vijana wa kike waliopata mimba au kuzaa kwa mara ya

kwanza na vijana wa kiume waliowapa mimba au kuwazalisha kwa mara ya kwanza ili kuwapa mafunzo ya kulea watoto wao ili wasiweze kuzaa tena kabla ya mtoto wa kwanza hajakuwa. Vijana wanaelekezwa maisha bora na yenye amani kila siku ya maisha yao. Nyimbo hizi za jando na unyago zina lengo la kumfunda mwari ili awe mtu bora kwa jamii yake.

## 5.4 Nyimbo za Jando na Unyago Zilizokusanywa

**Wimbo**

Chonde achinannungu vetu,

Nkajigala achalume,

Ntame mkunguru umo,

Tung'we mesi ga isima uchenene.

**Tarjima**

Chonde miungu wetu,

Usiwachukue wanaume hawa,

Kaeni pamoja,

Tunywe maji ya visima kwa utulivu.

Wimbo huu unaimbwa wakati vijana wanaandaliwa kwenda jandoni na unyagoni porini. Wazee wanafanya matambiko kwa kuiomba miungu iwasaidia kufanikisha shughuli yao. Lugha iliyotumika ina fasihi kubwa kwa jamii. Mtunzi ametumia neno ***Ntame mkunguru umo,*** sawa na kusema mkae duara moja kulinda shughuli ya unyago na jando isiingiliwe na watu wabaya walioko jamiini wenye nia ya kuharibu

ufanikishaji wa utoaji wa mafunzo hayo na kuwafanya mangariba na makungwi washindwe ili wachekwe na kupoteza ualimu wao.

**Wimbo**

Ubaya, ubaya ubaya welewo,

Wosye vankwaonao ankuiye mmwe,

Mama Venu veleo, baba venu valeo,

Mati venu veleo,

Malavi pa nchichinda lijele pe koyo

Mwanja kumigunda ajenu ngaona,

Ubaya ubaya.

**Tarjima**

Acha ubaya kijana

Wote unaowaona wamekufuata wewe

Huyo ni mama yako, na huyo ni baba yako na shangazi yako

Kesho wakipata tatizo usiende shambani

Wasaidie Kama wanavyokusaidia wewe

Acha ubaya.

Wimbo huu unawafundisha vijana kuishi kwa kusaidiana, kuheshimiana na kuthaminiana.

**Wimbo**

Amamaa ngaika kunola nne,

Pangulaga,

Tundu kapende nchitala,

Tundu kapende, nchitala

Tundu kapende nchitala.

**Tarjima**

Mama huji kuniona mimi,

Ninapopata shida,

Wakati nimetolewa kangozi

Wimbo huu unaimbwa na vijana wa kiume wakiwa jandoni baada ya kutahiliwa. Unawafundisha kuwa mashujaa katika maisha na waweze kujitegemea. Wimbo umetumia lugha ya picha inayomfundisha kijana kujitegemea. Neno ***tundu kapete nchitala***, inahusisha suala zima la kutahiri linavyohitaji siri na ushujaa wa kutomtegemea mama kusaidia njia yoyote.

**Wimbo**

Changa we changa, changa mbilimbili,

Kila siku kusagamila, vajigele majambia,

Chipula na upanga na chipande cha muwa,

Mbeleka chambunga, mbunga nkolesye moto,

Tulole mashaka.

**Tarjima**

Mtoto wewe mtoto

Mbilimbili naota kila siku

Watoto wachanga walichukua majambia,

Kisu na panga na kipande cha muwa,

Ukaja upepo ukawasha moto, tuone mashaka

Neno ***kusagamila*** ni neno linalomjenga kijana tabia ya kukumbuka mambo aliyofundishwa jandoni na unyago. Linasisitiza kujenga taswira ya mambo anayojifunza kila siku ya maisha yake.

**Wimbo**

Njinje kachechemele nnalye

Nnalye ya chinsene bila mbika

Kuleka ngali va kunseka

Mauti kulindimila

**Tarjima**

Njinje kula kwa taratibu

Usile vitu vya watu bila mipaka

Kuacha hakuna atakayekucheka

Kifo unakitafuta.

**Wimbo**

Katuputupu atupwileee,

Mwanache kasongoningo,

Natiji susuvaa

Vauleje mwana

**Tarjima**

Alimkata mwanae kiume,

Kwa kufikiri kuchezewa jando,

Mtoto anakatwa kiume chote,

Mwisho akamuuwa.

Wimbo huu unawaonya watu wenye tamaa ya kutaka kuwatahili watoto bila kupata mafunzo kutoka kwa wazee. Kazi ya kutahiri kwa mujibu wa mahojiano na Ngariba amesema inahitaji mafunzo na usimamizi hadi mtu atakapopata uzoefu. Kazi ya kutahiri inahitaji umakini na ushujaa. Kinyume na hapo ni kusababisha vifo kwa vijana. Kuwa mtaalamu kunakwepesha umwagaji wa damu nyingi. Mtunzi ametumia tashibiha katika neno ***susuva.*** Ina maana ya jipu. Amefananisha jipu na jinsia ya kiume.

**Wimbo**

Nalitendeleee, nalindele

Nambo ajenu niyakutenda,

Tombu tombu

**Tarjima**

Mwari wewe,

Wenzako wanafanya hivi,

Kwenye chakula cha ndoa.

Ukiwa unaimbwa wimbo huu, mabinti wanakuwa wamevuliwa nguo huku wamepanuliwa miguu wakionyeshwa jinsi ya kumpa mume chakula ndoa.

***Nalitendelee*** ni msichana kigori. ***Tombu tombu*** ni tanakali sauti ya ngoma inayochezwa ya kuandaa chakula cha ndoa.

**Wimbo**

Alianza nani mambo haya

Alianza mama kumwambia baba

Mtoto amekuwa tuncheze

Wewe mama ooooh

Mwana ju akusile.

**Tarjima**

Mwana ju akusile " mototo amekua"

Wimbo unawaonya wazazi wasiowapeleka watoto wao jandoni na unyago wakati umri wao umeshafikia.

**Wimbo**

Akaika alamu woo

Alamu mbalanganda

Winji ya kuvechetavecheta

Kusala ya kuuvelesi

Mala mandenga winji

Nang'ongo ukulu

Makutu kama mawiwi

Akaika

**Tarjima**

Shemeji asije kwenye uzazi

Amezidi umbeya

Mengi anapenda kuongea

Amchunguza maumbile ya mzazi

Asije.

Wimbo huu umetumia sitiari katika kufundisha mabinti kuondokana na umbea. Mtunzi ametumia neno ***Makutu kama mawiwi*** kuelezea via vya uzazi vya mwanamke vinavyokua wakati wa kujifungua. Anafundishwa kijana kutotoa siri za uzazi kwani kila mwanamke anapitia kazi hiyo. Je, inapotokea kuwa ni wewe utolewe siri zako?

**Wimbo**

Abesa aaa, Abesaaa!

Abesa kulavalava Abesaaa,

Kwasa mwana.

Nkatenda yeleyo, yeleyele yeleyo,

Ubaya ubaya.

**Tarjima**

Abesa

Acha kutangatanga

Unamtupa mtoto,

Usifanye hivyo

Vibaya

**Wimbo**

Akwegwe eee

Akwegwe mbite nchisosa

Kutama kwa pamusi

Kulokota ya ngali yenu

Lyuva kuvalika kuuja ni lupesa.

**Tarjima**

Mkwe nimekwenda kutafuta

Kukaa kwa nyumbani unaweza kuokota vitu vya watu

Jua likiwaka utarudi na vyako.

**Wimbo**

Nlikule, nlikule

Achalongwa anchinjangu njise

Kulombwa kwa mavasa ngava kulombwa,

Tambala checheliche

Litongo lyekulupuche.

**Tarjima**

Mwabieni mwambieni

Jamaa ndugu njooni msikilize

Kuolewa wa uke wenza siyo kuolewa

Jogoo akiwika mume anaondoka.

Wimbo huu umetumia taswira katika "***nlikule***" lina maana kusema bila mficho. Imefananishwa na mti unavyong'olewa bila kubakisha mizizi. Na hivyo binti anafundishwa kumtunza mume asije mume kuoa mke mwingine.

**Wimbo**

Akumbilile, akumbilile,

Amau kumbeleka,

Ni kumba valume kola,

Kumikaga katumbo,

Ni kutandaga chupa kasika,

Mwanache kolotoka,

Mwavilanje Akumbilila,

Nguma jitende nsalala,

Kutyoka kwake lupindo lukata.

**Tarjima**

Wakubwa zangu

Mama alinipeleka kuolewa

Nikapata mimba

Akanifundisha kuwa kuzaa unatokwa maji kisha mtoto

Ukiona hivyo waite wakubwa

Njia ya kutokea mtoto itakuwa imejifungua

**Wimbo wa kubembeleza watoto**

Mwanangu wowowo

Mama apile moto

Moto akuteleka

Aninkuteleka matimba.

**Tarjima**

Mwanagu wowowo

Mwanangu nyamaza

Mama ameungua moto

Akiwa anapika ugali wa pumba.

Vijana wakiwa unyagoni wanafundishwa malezi ya watoto. Malezi hayo ni pamoja na kuwaelekeza watoto kwa kuwapa mafundisho mema. Mtunzi ametumia neno "***kuteleka matimba*"** matimba ni pumba za mtama au mahindi zinazotumika kwa kula ugali. Neno hili limejenga taswira ya maisha ya jamii ya Wahiyao kuwa wanategemea kilimo katika kuendesha maisha yao. Mazao ya mahindi na mtama ndiyo mazao makuu ya chakula katika jamii hiyo.

**Wimbo**

Aliunyelu, aliunyelu, aliunyelu,

Aliunyelu mwanja, kuleka mapemba ga ngacha

**Tarjima**

Aliunyelu, anaondoka

Anaacha mtama haujachanua

***"Aliunyelu"*** ni aina ya ndege anayepatikana maeneo ya wakulima wa mtama. Ndege huyo hupatikana wakati mtama unachananu. Ukishavunwa haonekani wala kusikia tena. Wimbo unamjengea taswira mwanajamii anapozaliwa na kukua anakuwa na sifa tele. Sifa za utu wake zinamalizika baada ya kifo chake.

Wimbo huu ni wa kuomboleza. Mara nyingi huimbwa na watani wakati maiti ikiondolewa kwenda kuzikwa makaburini. Ni utambulisho kwa wafiwa na watu wengine wawe tayari kufanya maombi ya kuzika salama.

**Wmbo**

Mbungo lelo, mbungo,

Mbungo leleo, mbungo

Eeee, mbungo

Naiche kolokola yembe.Wimbo huu ni wa kuchapusha kazi. Jandoni na unyago wanauimba ili kuhimiza kazi kwa vijana. Wimbo umetumia takiriri katika kuweka msisitizo wa umuhimu wa kazi katika maisha. Kipimo cha utu wa mwaafrika ni kazi (Sengo 2009).

**Wimbo**

Mama mbeleche ngasyome duwa

Ngajimanye halifu duwa

Maulana, halifu duwa

Nabilalamina.

**Tarjima**

Mama nipeleke nikajifunze duwa

Nikaijue halifu duwa

Maulana, halifu duwa

Labilalamina.

Neno ***halifu duwa*** limejirudia ili kuweka msisitizo kwa wanajamii kuijua dini yao ya kiislamu na kwamba wakati wote wamjue Mungu (S, W).

Wakristo nao wana nyimbo zao za kuomboleza kama:

**Wimbo**

Ulendo ulendo ulendo ula

Ulendo uiche kwa bwana yesu

Mkamule msalaba mwakuye

Ulendo kwa bwana yusu utimile.

**Tarjima**

Safari ile imewadia

Safari kwa bwana Yesu

Kamata msalaba umfuate

Akuonyeshe njia.

Takiriri imetumika katika neno ***ulendo.*** Limejirudia kusisitiza wanajamii kuwa kifo kipo kwa kila binadamu. Jambo la muhimu ni kumjua Mungu. Ulendo ni safari. Utafiti umefanya usaili na makungwi kujua kwanini vijana wanafundishwa hata nyimbo za kuomboleza, walisema kuwa vijana wa kiume wanafundishwa kuwa katika jamii, kuna kufa na kuzikana. Hakuna binadamu anayekufa akaachwa bila kuzikwa.

Hivyo anajengwa tangu akiwa mdogo kujifunza mazishi. Walisema pia kama inatokea kijana wa kiume anafariki akiwa jandoni (porini) mafunzoni, anazikwa hukohuko jandoni na vijana wenzake wakiongozwa na mangariba, makungwi, wazazi wa kiume, pamoja na warombo. Mazishi hayo yanakuwa ni siri, wazazi wa kike wanafahamishwa siku moja usiku kabla ya jando kumalizika, ili watakapokuja vijana kujitambulisha kusiwe kitu kigeni kwao.

## 5.5 Upungufu wa Ukamilishaji wa Utafiti

Utafiti ulikabiliwa na Upungufu/ au matatizo yafuatayo:

### 5.5.1 Watafitiwa Kushindwa Kutoa Maelezo

Baadhi ya watafitwa wameshindwa kutoa maelezo juu ya mafunzo wayapatayo wakiwa jandoni na unyagoni kwa madai kwamba ni siri ya jandoni na unyagoni. Endapo angeweza kuitoa siri hiyo jamii isingemwelewa na hatimaye angeweza kutengwa. Uwazi usio mipaka ni utoto na uhenye. Mtoto mdogo wa miaka miwili mitatu, kuvua nguo na kujitia mchanga, ni jambo la kawaida. Akifikia umri, kilicho cha wazi huwa cha faragha, cha siri. Huo ni utu uzima.

### 5.5.2 Kutokuyafikia Baadhi Ya Maeneo

Kutokuyafikia baadhi ya maeneo ya utafiti kutokana na umbali na uhaba wa usafiri, kwani maeneo hayo yanamito, milima na mabonde makubwa na yana wanyama wakali kama chui, samba na mamba nakadharika. Sikuweza kupata msaada kayakabili matatizo hayo.

### 5.5.3 Baadhi ya Watafitiwa Wameshindwa Kutoa Maelezo Sahihi

Baadhi ya watafitiwa wameshindwa kutoa maelezo sahihi kwa fikra kwamba mtafiti atafaidika kwa kuuza mawazo yao na kupata pesa, na wengine kutokuamini kwamba kazi hizi sizo zile zilizofanywa na wazungu walioishia kuwabeza, kuwatukana na kuwakebehi.

### 5.5.4 Kukosekana kwa Vyombo vya Kurekodia Nyimbo

Kukosekana kwa vyombo vya kurekodia nyimbo. Jitihada zote zilishindikana kutokana na kukosa pesa za utafiti za kukidhi haya.

### 5.5.5 Ugumu wa Baadhi ya Maneno ya Kihiyao Katika Kuyatarijima kwa Kiswahili

Ugumu wa baadhi ya maneno ya Kihiyao katika kuyatarjima kwa Kiswahili. Huu ni ushahidi kwamba kila lugha ni lugha inayojitosha na Kiswahili chajitosha zaidi kwa kuwa chenyewe kina umataifa na mchanganyiko tata wa tamaduni nyingi zaidi kuliko Kihiyao. Nyimbo za jando na unyago zinazoimbwa na Wahiyao wa Lulindi zina umuhimu kwa jamii hiyo kwani zina mafunzo mazuri ya kumjenga kijana katika maadili mema. Zinafunza maisha ya ki-utu uzima. Mafunzo hayo yanamjenga kijana

katika maadili mema kama kuwa mtii, na kuweza kujitegemea. Upungufu mwingine wa utafiti huu uliojitokeza katika matumizi ya tanakali sauti unaojitokeza katika nyimbo za unyagoni. Tanakali sauti ni tamathali ya usemi ambayo sauti ya kitu fulani inaigwa na kuchukulia sauti yake na kutumika.

Tarjima za nyimbo za jando na unyago ki-uhalisia tuliupata wakati wa utafiti. Nyimbo nyingi ni za matusi, ambayo tumeona si vyema na siyo ustaarabu kuandika matusi hayo katika kazi hii ingawa tarjima zake zinafanana. Neno linaweza kuigwa kutokana na mwigo wa sauti ya kitu fulani na kulitumia katika kutoa mafunzo kwa wari. Lakini neno hilo lina maana kubwa sana kwa maisha ya wanajamii. Kama maadili ya ndoa ili ndoa ziweze kudumu. Utafiti umebaini neno ***"checheliche"*** kutokana na mwigo sauti ya jogoo anapowika asubuhi. Pia neno ***"Lyekulupuche".*** Katika mafunzo yao ya unyago mabinti wanafundishwa kuzitunza ndoa zao ili mume asiende kutafuta mke wa pili, kutafuta starehe ya chakula cha ndoa. Kwa hiyo tumeelezwa kuwa neno hilo linawafundisha mabinti kumtunza mume asije akaona usiku ni mrefu na kutamani kutoka asubuhi mapema kwenda kutafuta mke wa kumpa starehe.

## 5.6 Ukusanyaji wa Data

Data zilizopatikana kutoka jandoni na kumbi zilizohojiwa ni kama ifuatavyo:

1. Utafiti umeeleza hali halisi ya maisha ya vijana wawapo jandoni. Aina ya mavazi wanayovaa.Vijana wanavalishwa kanga au kitenge wakiwa wamefunga kiunoni ama begani (kingolingoli).

2. Sehemu ya makazi yao wigo umezungushwa na mabua ya mtama ukutani na paa kuezekwa kwa mabua hayo.

3. Mazingira ya makazi hayo ni porini mbali kabisa na makazi ya jamii kwa lengo la kuficha siri ya jandoni na unyagoni.

4. Wakiwa jandoni vijana wanakuwa walinzi wa jando lao wakiwa na silaha kama fimbo, marungu pamoja na visu na mapanga. Mara tu tulipoingia lango kubwa, vijana walijitokeza haraka na kutoa amri ya kutoingia. Walipoona ni mwanamke walipiga filimbi na vijana wote (walikuwa 120), walizingira jando lote tayari kwa mapigano. Hata hivyo warombo walipiga filimbi ya kuashiria amani na hivyo vijana wote walirudi ndani wakisubiri kupewa taarifa.

5. Utafiti umefanikiwa kujua mgawanyo wa kazi wa vijana wakiwa jandoni na unyagoni, tangu wanapoamka hadi jioni. Vijana wanapewa kazi ya kukata kuni kwa makundi na zamu ya kupika ingawa wanasaidiwa na warombo, kutokana na umri wa vijana kuwa ni wadogo wasingeweza kupika chakula cha watu 120 na warombo wao, zamu za ulinzi wa lango kubwa, kuchota maji mtoni, kuwinda, pamoja na zamu za kuongoza kuimba nyimbo zenye mafunzo mbalimbali kama kuheshimu baba, mama, kutunza siri za jandoni, ushujaa, malezi na kuogopa wake za watu.

6. Mahojiano yalifanyika kwa vijana 50 wa kiume na wakike 50 sawa na asilimia 100 kutokana na vijana waliotarajiwa kuhojiwa.

7. Utafiti uliona mazingira ya maisha ya vijana wakiwa jandoni na unyagoni. Malazi ni chini wakiwa wametandikiwa mikeka au magunia, pamoja na

majamvi. Vyoo wanavyotumia ni hafifu na viko karibu na maeneo ya kulala. Vyakula ni vingi na vingine vilitoka nyumbani kwa wazazi mmojammoja kwa lengo la kubadilisha aina ya chakula cha watoto wao.

8. Utafiti umekusanya nyimbo nyingi zilizorekodiwa, na nyingine ziliandikwa kwa vile zilikuwa fupi.

**Matatizo:**

1. Baadhi ya nyimbo walikataa kutoa tarjima yake kwa vile walisema ni siri ya jandoni.
2. Mahojiano kwa kiasi kikubwa yalitawala lugha ya Kihiyao ingawa wakati mwingine walitumia Kiswahili. Hata hivyo mtafiti alikuwa na mkalimani wa lugha hiyo ambaye alisaidia kupata tarjima ya maneno ya Kihiyao.
3. Katika utafiti huu tukiwa jandoni, walitutaka tutoe kiingilio cha uwanja huo Kama faini ya kuvunja sheria kiasi cha Tsh.20, 000/=, tulifanya hivyo ingawa kiasi cha pesa tulichokuwa nacho kilikuwa kidogo kwa mahitaji ya utafiti.

Kwa upande wa watafitiwa walipata faida ya kuona kuwa kumbe jando na unyago ni jambo muhimu hadi linafanyiwa uchunguzi na watu mbalimbali. Na upande wa watafiti wamefaidika kupata uhalisiya wa nyimbo za jandoni na unyagoni. Tumegundua kuwa nyimbo za jando na unyago zina tofauti na kicheni pate na mapasuaji ya hospitali. Nyimbo za jando na unyago zinafundisha “Utamaduni wa jamii, na nadharia ya Utu na Mtu kwao” (Sengo 2009) ndipo inapojidhihirisha.

Katika utafiti huu wa nyimbo za jando na unyago, zimekusanywa kutoka kwa:

(i) Watungaji wa nyimbo za jando na unyago

(ii) Waimbaji wa nyimbo za jando na unyago (vijana waliopitia jando na unyago)

(iii) Wazazi wa vijana waliopitia jando na unyago.

(iv) Wazee wanaozifahamu nyimbo za jando na unyago.

(v) Ngariba, mashowari na makungwi wa jando na manyakanga, mafundi na makungwi wa Unyago.

**Jedwali Na. 5.1: Orodha ya Wahojiwa**

| JINA | UMRI |
|---|---|
| Makungwi | 60 – 70 |
| Mangariba | 70 – 80 |
| Vijana waliopitia jando na unyago | 18 – 35 |
| Wazazi wa kike | 40 – 50 |
| Wazazi wa kiume | 40 – 50 |

**Chanzo: Mtafiti, (2011)**

Mtafiti amefanikiwa kuwahoji vijana 50 wa kiume na 50 wa kike sawa na asilimia 100%. Maswali ya hojaji ndiyo yaliyotumika kukusanya data hizi. Majibu yao yameonyeshwa katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 5.2: Mafunzo Wanayoyapata Vijana Kupitia Nyimbo za Jando na Unyago**

| Vijana wa kiume | Vijana wa kike |
|---|---|
| Kutokubali kushindwa katika jambo katika jamii<br>Ushujaa<br>Kuoa na kutunza mke na watoto<br>Kujali kazi za uzalishaji mali<br>Kujitambua kuwa yeye ni mwanaume na kiongozi wa familia yake.<br>Uvumilivu katika majukumu mazito | Malezi ya familia<br>Kuheshimu ndoa<br>Kutunza ndoa kwa kumpa mume mahitaji yake kama kumpa chakula cha ndoa ili asiende kula kwingine<br>Kuwa msafi na kujipamba kwa ajili ya mume.<br>Kukubali makosa na kuomba msamaha kwa mume hata kama hajafanya kosa.<br>Kuwa na lugha ya upole mbele ya mume. |

**Chanzo: Mtafiti, (2011)**

**Jedwali Na. 5.3: Vijana Wanaoona Nyimbo za Jando na Unyago Zina Manufaa**

| | **Zina Mafunzo Lakini Yanatumika Vibaya** | **Asilimia** | **Hazina Mafunzo** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|
| Wanawake | 46 | 46% | 4 | 4% |
| Wanaume | 49 | 49% | 1 | 1% |
| **Jumla** | **95** | **95%** | **5** | **5%** |

**Chanzo: Mtafiti, (2011)**




**Kielelezo Na. 5. 1: Mchanganuo kwa Asilimia Kuonyesha Manufaa ya Nyimbo za Jando na Unyago**

**Chanzo: Mtafiti, (2011)**

Data hizi zinatupa picha halisi kuwa jamii ya Wahiyao wanaikubali mila hii ya jando na unyago. Na hii imetokana na mazingira yaliyojengwa na jamii hii kuwa ni lazima vijana wapitie jando na nyago. Kutopitia jando na unyago ni kumnyima kijana haki yake ya kupata maadili mema. Vijana 4 wa kiume waliosema hakuna faida ni sawa 4% wamesema kwamba wao wanaona yanayofundishwa ni ya kiutu uzima zaidi.

Kwa nafasi yao yanawapotosha na kuwafanya watamani utu uzima kabla ya umri wao.

**Jedwali Na. 5.4: Manufaa ya Nyimbo za Jando na Unyago**

| | Zina Fasihi | % | Zinakubalika | % | Hazikubaliki | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanawake | 50 | 100% | 50 | 00% | 00 | 00% |
| Wanaume | 49 | 98% | 49 | 98% | 01 | 2% |
| Jumla | 99 | % | 99 | 98% | 01 | 2% |

**Chanzo: Mtafiti, (2011)**




**Kielelezo Na. 5.2: Manufaa ya Nyimbo za Jando na Unyago Kwa Asilimia**

**Chanzo: Mtafiti, (2011)**

Data zinaonyesha kuwa nyimbo za jando na unyago zina fasihi simulizi ya kutosha kwa jamii. Nyimbo hizo zinakubalika na jamii nzima. Kwa vile fasihi ni chombo cha jamii, kinachosaidia kwa kiasi kikubwa katika kutoa maadili kwa jamii husika, inaonyesha wazi kuwa jamii ya Wahiyao wa Lulindi wameikubali fasihi hii. Na hivyo wanaitumia kama chombo chao cha kuwakuzia vijana wao kwa kurithisha

vizazi vyao. Kila mwanajamii wa jamii ya wahiyao wa Lulindi ni lazima wapiti mafunzo ya jando na unyago katika kutimiza jadi yao.

(i) Uchunguzi unaonyesha kuwa vijana wanaopelekwa jandoni na unyagoni ni wadogo ukilinganisha na vijana waliokuwa wanapelekwa hapo awali. Mafunzo yaliyokuwa yanatolewa hapo awali yaliendana na umri wa vijana, kiasi cha kufanya mafunzo hayo kuonekena kuwa ni bora kwa vile walengwa walipata elimu iliyowastahili. Miaka ya sasa vijana wanapelekwa wakiwa wadogo. Kinyume na malengo ya hapo awali ya mafunzo ya jando na unyago. Wazee wa jamii ya wahiyao wameeleza sababu zinazowafanya wazazi kuwapeleka vijana wadogo jandoni na unyagoni ni kama zifuatazo:

(ii) Msukumo wa kundi rika. Utafiti umebaini kuwa rika linashawishi watoto kuwalazimisha wazazi kuwapeleka jandoni. Hii ni kwa sababu, kama kundi rika wapo waliopitia jando na unyago, basi wanalazimika kuwatenga wale wasiopitia jando na unyago kwa kuwaona ni watoto hawafai kucheza pamoja nao.

(iii) Hofu ya wazazi kuwa mtoto akifikia umri wa miaka saba ya kwenda shuleni, hatapata nafasi ya kumpeleka kijana wake jando au unyagoni kutokana na kupishana kwa ratiba za shule na zile za jando na unyago.

(iv) Tamaa ya wazazi ya kupata pesa. Imekuwa ni kama mradi wa kupatia pesa (upatu) hasa kwa akina mama. Hivyo kwa kuhofu muda utakuwa mrefu atakosa pesa zake basi humpeleka kijana wake jandoni au unyagoni hata kama umri wake bado haujafikia.

(v) Kuiga kutoka mataifa ya nje hasa ya Asia (ya Kiaarabu) ambayo mtoto wa kiume anapelekwa kutahiriwa mara tu anapozaliwa ili kumpunguzia maumivu awapo mkubwa.

**Jedwali Na. 5.5: Takwimu Zifuatazo Zinaonyesha Umri wa Vijana Walioingizwa Mafunzo ya Jando na Unyago Mwaka 2010**

| | **Umri** | | | | | | | | | | **Jumla** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jinsia | **1** | **2** | **3** | **4** | **5** | **6** | **7** | **8** | **9** | **10** | | % |
| Vijana wa kiume | 0 | 0 | 5 | 12 | 27 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 44 | 44% |
| Vijana wa kike | 0 | 0 | 2 | 18 | 30 | 5 | 0 | 0 | 0 | 1 | 56 | 56% |
| Jumla | 0 | 0 | 7 | 30 | 57 | 11 | 0 | 0 | 0 | | 100 | 100% |

**Chanzo: Ofisi ya Serikali ya Tarafa ya Lulindi, (2010)**

**Jedwali Na. 5.6: Takwimu Zifuatazo Zinaonyesha Umri wa Vijana Walioingizwa Mafunzo ya Jando Naunyago Mwaka 2011**

| | **Umri** | | | | | | | | | | **Jumla** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jinsia | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 55 | % |
| Vijana wa kiume | 0 | 0 | 0 | 0 | 12 | 34 | 33 | 0 | 0 | 0 | 79 | |
| Vijana wa kike | 0 | 0 | 0 | 0 | 55 | 20 | 46 | 0 | 0 | 0 | 121 | |
| Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 67 | 54 | 79 | 0 | 0 | | 200 | |

**Chanzo: Ofisi ya Serikali ya Tarafa ya Lulindi, 2011)**

Takwimu hizi zinaonyesha jamii ya watu wa Lulindi wengi wao wanawapeleka vijana kwenye mafunzo ya jando na unyago wakiwa na umri wa miaka kuanzia 3 hadi miaka 7. Huu ni umri mdogo sana kwa mafunzo ya jando na unyago.

Ni vijana wadogo ambao hawawezi kufundishwa maisha ya kiutu uzima. Elimu inayotolewa ni ile ya kiutu uzima. Utafit umebaini kuwa mafanikio ya elimu hiyo kwa sasa ni madogo. Vijana wanajaribu kutenda yale waliyofundishwa wakiwa jandoni na unyagoni kama wanajaribu kujamiiana kwa vile amefundishwa mfano binti anafundishwa namna ya kumpa chakula cha ndoa mume wake pindi atakapoolewa kwa ustadi ili mume asitoke nje kutafuta starehe ya chakula hicho. Kutokana na utoto wao mara tu watokapo chuo hicho vijana wanajaribu yale waliyofundishwa. Hatima ya hayo ni kupata mimba za utotoni ambazo sasa vijana wengi wa jamii ya Wahiyo wa Lulindi wameacha watoto wao na kukimbilia mijini kutafuta maisha bora ambayo yamekuwa bora maisha.

Mafunzo ya jando na unyago ni mafunzo yanayomuandaa kijana na maisha ya kiutu uzima ambayo yatamsaidia kijana kuishi na jamii kisawasawa. Kutokana umri mdogo wa vijana wanaopelekwa jandoni na unyagoni kuwa mdogo, ni wazi mafunzo hayo hayafundishwi kikamilifu. Utafiti ulifanya mahojiano na baadhi ya makungwi ni mambo gani wanafundisha vijana hao wadogo. Walieleza kuwa mafunzo yanayotolewa ni yale tu yanayomsaidia kijana kuishi vema na jamii kama heshima, kupokea wakubwa, utii pamoja na uwajibikaji. Walieleza kuwa kwa kiasi kidogo kwa kutumia mafumbo wanawafundisha vijana baadhi ya miiko katika jamii. Walieleza pia ni vigumu kuwafundisha mengi ya undani ya jando na unyago.

**Jedwali Na. 5.7: Mchango wa Wazazi Kuhusu Mafunzo Ya Jando Na Unyago**

| | Wanaosema Nyinbo Za Jando Na Unyago Zina Mafunzo Lakini Yanatumika Vibaya | Asilimia | Wanaosema Nyinbo Za Jando Na Unyago Hazina Mafunzo | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Wazazi Wa Kike | 18 | 18% | 2 | 2% |
| Wazazi Wa Kiume | 20 | 20% | 0 | 0% |
| Jumla | 38 | 95% | 2 | 5% |

**Chanzo: Mtafiti, (2012)**

Mafunzo hayo zaidi wanayapata pindi wanapobalehe na kuvunja ungo kwa sababu tayari wanakuwa wamekua kiasi cha kuweza kuelewa nini wanafundishwa. Hata hivyo wanakuwa tayari wamekosa misingi ya awali ya mafunzo hayo yakilinganishwa na mafunzo yaliyokuwa yanatolewa hapo awali.




**Kielelezo Na. 5.3: Mchango wa Wazazi Kuhusu Mafunzo ya Jando na Unyago kwa Asilimia**

Wazazi wanaosema hazina mafunzo ambao ni asilima 2% wamesema kuwa kwa vile wanaopewa mafunzo ni watoto wa umri mdogo, ni wazi wanachofundishwa siyo mafunzo kamilifu ya kiutu uzima, bali ni kutimiza mila tu. Kulingana na data zinavyojieleza inaonyesha wazi kuwa jando na unyago katika jamii ya Wahiyao wa Lulindi ni jambo la lazima kupitiwa na kila mwanajamii. Ni sehemu ya maisha ya

kila siku ya jamii hiyo. Ni elimu inayorithishwa kizazi hadi kizazi kwa jamii hiyo. Kila mmoja katika jamii anawajibu wa kurithisha kwa mwenzake ili mradi mila, desturi na utamaduni huu uwe endelevu kwa kila kizazi cha jamii hii.

**Jedwali Na. 5.8: Sababu za Wazazi Wanaosema Hakuna Faida ya Nyimbo za Jando na Unyago**

| Sababu za Wazazi wa Kiume Wanaoona Nyimbo za Jando Na Unyago Hazina Faida | Sababu za Wazazi wa Kike Nyimbo za Jando na Unyago Hazina Faida |
|---|---|
| i) Vijana wanaopelekwa chuo hicho ni wadogo hivyo hakuna wanachofundishwa.<br>ii) Ukakamavu na uvumilivu kwa vijana umepotea<br>iii) Vijana hawana heshima ukilinganisha hapo zamani.<br>iv) Maadili yamepungua kwa vijana. | i) Hakuna siri ya mafunzo ya chuo hicho<br>ii) Mabinti wanafanya majaribio ya kile wanachofundishwa unyagoni hasa chakula cha ndoa matokeo yake ni kupata mimba za utotoni.<br>iii) Wanashindwa kutunza familia zao kwa vile mafunzo ya kutunza familia waliyapata wakiwa wadogo hayakuwaandaa kwa maisha ya kiutu uzima. Na hivyo hawapikiki kisawasawa. |

**Chanzo: Mtafiti, (2012)**

Wazazi 5% wameona hakuna faida ya vijana kupelekwa jandoni na unyagoni. Malengo ya chuo hicho ni kutoa elimu ya maisha ya ki-utu uzima yatakayomfanya kijana aisha kulingana na matakwa ya jamii. Elimu hiyo anaikosa kutokana na vijana kupelekwa wakiwa na umri mdogo na hivyo kuikosa elimu hiyo basi wanaona hakuna haja ya kutoa elimu hiyo. Ila kwa kujali afya ya kijana wanawapeleka vijana wao hospitali kwa madaktari na kuwafanyia upasuaji mdogo kuwasafisha.

Wazazi hao wanaona kuwa Warombo wanashindwa kutoa elimu hiyo kwa kina wakiwa jandoni au unyagoni kutokana na umri mdogo wa vijana. Walitolea mfano vijana wa umri wa miaka 3 hadi 5 wanapelekwa jandoni na unyagoni hakuna

wanachoelewa zaidi ya michezo ya kitoto waliyokuwa nayo. Wanapolazimishwa kufundishwa mambo ya kiutu uzima, madhara yake ni mmomonyoko wa maadili kwa jamii ya kihiyao. Vijana wanakuwa na uhuru wa kuamua mambo wanayoyataka. Mtafiti amekusanya data kutoka kwa vijana wa kike (50) na wa kiume (50) waliopitia nyimbo za jandoni na unyago. Mafunzo yaliyokusanywa yameoneshwa piya katika jedwali la matokeo kama ifuwatavyo:

**Jedwali Na. 5.9: Mafunzo ya Jando na Unyago**

| Vijana | Mafunzo ya jando | Mafunzo ya unyago |
|---|---|---|
| Wa kiume | i)ukakamavu na uvumilivu<br>ii)kuheshimu watu wazima<br>iii)utii na unyenyekevu<br>iv)usafi<br>v)bidii katika kazi<br>vi)uadilifu<br>vii) Kuishi na jamii yake vizuri. | i) wanajifunza malezi ya familia kama kutunza watoto kwa kuwanyonyesha<br>ii) uvumilivu katika ndoa<br>iii)heshima kwa mume,wazazi wa mume na watu wazima<br>iv) Kuogopa na kuwaheshimu waume za watu. |

**Chanzo: Mtafiti, (2012)**

Mafunzo haya yanafundishwa kwa njia ya nyimbo. Nyimbo zinazoambatana na vitendo vya wari katika kusisitiza yale yanayofundishwa.

**Wimbo**

Abanuele Abanuela

Pa n’tepo mbalambala

Kuseka va’ngali umbo mun’twe

Kuleva nkukusosa

**Tarjama**

Banuela wewe

Umekaa chini ya mti

Kuwacheka wenye vipara kichwani

Makosa unayatafuta.

Wimbo huu unawakataza vijana wa kiume wakiwa jandoni kuwa na tabia ya kuwachungulia akina mama wawapo kisimani wakioga. Kuwachungulia akina mama ni kuwavunjia heshima. Kwa hiyo jamii ya wahiyao inawajali akina mama, kwani wao wanashiriki kwa kiasi kikubwa kwa malezi ya vijana tangu wakiwa wadogo. Kwa hiyo ni watu wa kuheshimiwa.

**Wimbo**

Van'kwenu ngava alumbo,

Kwa komasya, kwa jongola masengo genu

Kwimuka ni kuteleka

Kupyajila ni kutandika

Malove ga mtemela ni kukunguluka

**Tarjima**

Mumeo siyo kaka yako

Kumsalimia, kumnyoosha ni kazi yako

Kuamka na kupika

Kufagia na kutandika kitanda

Maneno ya siri kuongea

Wimbo huu unawafundisha vijana wa kike wakiwa unyagoni namna ya kumtunza mume asitoke nnje kutafuta vyakula. Wanaelekeza kuwa mume ni mtu anayehitaji kuheshimiwa, anahitaji kutukuzwa. Heshima na matunzo kwa mume yanakuweka kwenye ndoa kwa kipindi kirefu bila kuachana.

Msokile (1992) amesema, nyimbo za jando na unyago, huchukua sehemu kubwa ya baadhi ya maisha ya jamii. Nyimbo zote zinazoimbwa na wasanii wakati huo ni za mafunzo na huimbwa kwa mafumbo. Kwa vile vijana waliotarajiwa kupata mafundisho hayo ni wale waliofikia utu uzima, ni rahisi kufumbua mafumbo hayo. Lengo ni kumfanya kijana awe ni mtu wa kufikiri wakati wote na kuchambua kipi kizuri cha kukifuata na kipi kibaya cha kuweza kukiepuka katika maisha yake. Pamoja kuwa nyimbo hizo huimbwa kimafumbo,lakini vitendo vinavyoambatana navyo ni vya wazi. Kila tendo lina nia na mafundisho yake yaliyo muhimu kwake kijana na jamii yake. Hii inasaidia kumjenga kijana kisawasawa kile anachofundishwa.

Mabadiliko ya kisiasa na ya kiuchumi nchini na duniani kote, yamesababisha mabadiliko ya utoaji wa elimu ya jando na unyago kwa jamii zetu za kiafrika. Katika, jamii ya Wahiyao wa Lulindi Masasi katika miaka ya sitini hadi themanini nyimbo za jando na unyago zilipewa nafasi kubwa katika kuelimisha vijana juu ya maisha bora.

Elimu ilitolewa porini kwa muda mrefu usiopungua miezi miwili kwa lengo la kuwapa elimu ya kutosha. Lakini kufikia miaka ya tisini hadi miaka ya elfu mbili. Wanasiasa wamebadilisha mfumo wa utoaji elimu ya nyimbo za jando na unyago. Wanasisitiza vijana kupewa elimu hiyo kwa muda mfupi wa wiki mbili au mwezi mmoja. Hii imetokana  na kuonekana kwa gharama za kuwaweka vijana porini kwa muda mrefu kuwa ni kubwa, wazazi hawazimudu kutokana na hali zao kuwa za chini kiuchumi.vilevile wanasiasa wamesisitiza zaidi elimu ya darasani au shuleni inayohimiza kijana kujua kusoma na kuandika. Hali hiyo imesababisha elimu ya nyimbo za jando na unyago kushuka, kudharaulika, na kuonekana si muhimu. Elimu ya nyimbo za jando jando na unyago ni muhimu kwani inahifadhi na kuthamini utamaduni wa jamii. Shuleni kuna kisomo. Jandoni na Unyagoni kulikuwa na elimu ya maisha ya nadharia na ya vitendo.

Sengo (2009) katika nadharia ya utambulishi ameeleza kuwa fasihi inatambulisha Sanaajadiiya na Sanaa za jadi za utamaduni wa jamii. Amewataja wasungo wa sanaajadia wasiopitia jando na unyago kuwa wanathamini utamaduni wa ulaya zaidi na kuacha utamaduni wa jadi zao. Amesisitiza kuwa nadharia ya utambulishi isipelekwe Ulaya wala Marikani. Uhalisia usomwe viamboni, vijijini na nadharia zitumike kwa upana wake. Kwa hiyo nadharia inahimiza jamii kutukuza utamaduni wake kwa sababu ndiyo silaha ya maisha ya jamii hiyo.

Utamaduni wa jamii ya Wahiyao wa Lulindi ni kudumisha nyimbo za jando na unyago. Jamii nyingi za kiafrika, uimbaji ni mambo yanayohusika na maisha ya kila siku. Kwa hiyo nyimbo hizo huimbwa kwa madhumuni maalumu. Kwa mfano mtoto alipozaliwa ishara ya kuzaliwa kwake ni kuimbwa nyimbo.

Kwa jamii ya Wahiyao wa Lulindi wana wimbo wao

Ajombweche kasulo kana maganga

Agulwiche ni mwana apatile

Mwana jwa nnume/jwa nkongwe

Lelo ukulu aupatile, eeee

**Tarjima**

Amevuka kijito chenye mawe,

Ameruka na mtoto amepata,

Mtoto wa kiume/wa kike,

Leo ukubwa ameupat.

Wimbo huu unaimbwa mara tu watokapo hospitli au kwa Mkunga wa jadi baada ya binti kujifungua mtoto wakielekea nyumbani kwa mzazi aliyejifungua. Lengo la wimbo ni kutoa taarifa kuzaliwa kwa mtoto salama na kutambulisha aina ya mtoto aliyezaliwa. Waimbaji wa wimbo huu tumetambulishwa kuwa ni wanawake watu wazima waliompeleka binti kujifungua. Bi Zainabu Mkumbila ametueleza kuwa wanapofika nyumbani kwa binti wanapokelewa na wanawake wenzao watu wazima na kuimba na kucheza ngoma iitwayo “Likwata” ambayo wimbo huu ndiyo unaimbwa.

Pia wana nyimbo waimbazo wakati mtoto wa kiume anapopelekwa jandoni kutahiriwa akiwa Ngariba yuko tayari kwa kuwatahiri vijana. Wimbo ufuatao unatumika kuibwa kwa lengo la kuwatambulisha wazazi wa kike kuwa watoto wao ni muda wa kutahiliwa.

**Wimbo**

Mwatuona, mwatuona, eee

Mwatuona eee mwatuona

Liyaya, ndeleule

Liyaya, ndeleule mwalole vandu kogoya

**Tarjima**

Hamtaona

Jando letu hatari

Muwaone watu hatari

Wakati wimbo huu unaibwa wazazi wa kike wako nyumbani wakiwa wameporomosha kanga kiunoni matiti wazi wakiomba miungu wanaume wamalize salama kazi yao. Na huko jandoni wanaume wanapiga ngoma na kuimba wimbo huu kwa lengo la kuzuia kelele za vilio vya watoto kutokana na maumivu ya kutahiliwa. Bwana Nayari ni Ngariba. Yeye ametueleza kuwa vilio vya watoto vinatokana na maumivu ya kutahiriwa bila kutumia sindano ya ganzi. Ametueleza kuwa kisu kimoja kilitumika kutahiri vijana wote kwa kipindi cha nyuma. Amesema hivi sasa amezuiliwa na serikali kutumia kisu kimoja kutokana na ugonjwa hatari wa UKIMWI. Na badala yake kila mzazi anawajibika kuleta kisu chake ambacho kinashikiliwa na Mlombo.

Nyimbo za jando na unyago ni elimu inayojenga misingi ya kuonyesha vijana wafanye mambo mema ambayo baadaye ndiyo yanayojenga jamii baada ya fikra na mazoea kujengeka udogoni.

**Faida ya nyimbo za jando na unyago**

(i) Vijana wanakuwa wanyenyekevu na wenye heshima.

(ii) Wanajali mila na desturi za jadi yao.

(iii) Inakuza utamaduni wa jamii ya wahiyao

(iv) Inajenga jamii iliyosawa.

Utafiti unatueleza kuwa Wahiyao wanajali Sanaajadia yao ya jando na unyago. Ni Chuo kinachotoa elimu bora ya maisha ya ki-utu uzima. Likini mila hiyo inapungua hadhi yake kutokana na kukiuka malengo ya elimu hiyo. Kama malengo ni kumuandaa kijana aliyefikia utu uzima aishi maisha ya ki-utu uzima, kumpeleka kijana wa umri mdogo ni kutimiza tu mila hiyo na ambayo haitamjenga katika maisha yake ya ki-utu uzima. Badala yake yamekuwa mashindano ya matumizi mabaya ya raslimali na kusababisha kushuka kwa uchumi wa jamii hiyo kutokana na mashindano ya nani anapesa ya kufanya anasa wakati wa shughuli za jando na unyago.

Kutokana na kupata elimu ya jando na unyago katika umri mdogo vijana hawajui miiko ya mila hiyo, na hivyo kunajitokeza mmomonyoko wa maadili. Vijana hawana woga wala wasiwasi wa jambo lolote wanalofanya hawajui miiko ya maisha ya jamii yao. Utafiti umebaini kuwa vijana wa Kihiyao wa Lulindi wamekuwa walevi wa pombe hasa pombe iitwayo "**Nyipa**" ni pombe inayotengenezwa kwa mabibo ya korosho. Kama mila na desturi yao ilivyotueleza hapo awali pombe ilitumika wakati wa matambiko pale wanapoandaa jando na unyago. Lakini hivi sasa ni kinyume. Pombe inatumika wakati wowote na hivyo vijana wengi ni wavivu na hawana

heshima na hivyo jamii hiyo inakosa nguvu kazi, ambapo wazee ndiyo wanategemewa kuwa wazalishaji. Vijana hawana ukakamavu, wanawategemea zaidi wazazi wao kwa shughuli za kiuchumi.

**Muundo wa lugha**

Katika utafiti wetu tulichunguza lugha wanayotumia Wahiyao katika kutoa elimu ya jando na unyago. Lugha rasmi inayotumika ni ya Kihiyao ingawa kwa kiasi kidogo Kiswahili kinatumika kutokana na mchanganyika wa vijana kuishi mazingira tofauti ya kihiyao na hivyo kufanya vijana hao kutoelewa.

Lugha ya kifasihi ina maana nyingi na mzuri katika kuelimisha jamii. Neno moja linafundisha mambo mengi ya kimsingi kwa jamii. Lugha ya fasihi simulizi inaambatana na ishara mbalimbali. Ishara ambazo zinamjengea kumbukumbu ya kudumu kwa anayefundishwa. Na kila ishara inategemeana maana yake ya utoaji (Holt na wenzake 2001).

Lugha ya Kihiyao katika jando na unyago ina maana nzito sana kuliko lugha ya kiswahili. Lugha ya Kihiyao ina falsafa kubwa inayoambana na mila na desturi zake. Ni Lugha rafiki ambayo inamaana kihistoria, kiutamaduni, ina falsafa na inabembeleza. Lugha ya kihiyao ni nzuri kutumika katika mafunzo ya jando na unyago kwa jamii ya wahiyao. Inamkuza kijana katika maadili ya Kihiyao.lengo ni kumfanya kijana aijue lugha yake, utamaduni wake pamoja na mila na desturi za Kihiyao. Lugha ya Kihiyao ina ishara mbalimbali zinazotumika katika mafunzo ya jando na unyago.

Baadhi ya ishara zinazotumika katika mafundo yao ya unyago kama, kumkata kiwembe binti pajani na kutoka damu nyingi, kunamfundisha binti kuwa ipo siku atakuja kuona damu ikitoka sehemu zake za siri, hiyo binti anaelekezwa kuwa atakapoona hali hivyo akimbie haraka kwa shangazi au bibi aelezwe tatizo lake. Bibi na shangazi watamfundisha jambo. Na kwamba asipofanya hiyo miiko itamfuata katika maisha yake. Ishara nyingine walieleza kuwa, binti anafundishwa namna ya kumpa mume wake chakula cha ndoa pindi atakapokuwa mkubwa na kuolewa. Binti anatengenezewa mfano wa uume na kumfundisha namna atakavyompa chakula hicho mume wake huku akifundishwa vionjo mbalimbali vya mume kufurahia chakula hicho hadi ashibe na asitamani kwenda kutafuta chakula kingine kwingine.

Pia tulifanya usaili na Makungwi wa jando 5, hawa walitueleza ishara zinazotumiwa na kufundisha wanaume katika mafundisho yao. Kijana anaelezwa kuwa ishara mojawapo ya kujitambua kuwa amekuwa ni pale atakapoona kuwa amepita mbele yake binti wa kike na akampenda ataona uume wake umesimama, basi ajue kuwa amekuwa na hivyo awe mwangalifu wa kuchagua binti mzuri wa tabia na matendo yake wa kuweza kumuoa. Asipofanya hivyo anaweza kuambukizwa magonjwa au kuoa mke mvivu ambaye hatapendwa na familia yake.

Ishara pia inajitokeza katika kupeana taarifa ya matukio ya kifo kinachotokea jandoni. Kama kijana amefariki jandoni (kwa kihiyao wanaita “Awilile kumalembe” inatolewa ishara nyumbani kwa wazazi wa kijana kwa kuvunja chungu mlangoni asubuhi mapema na mrombo wa kijana, ili watakapoamka ujumbe uwafikie. Wazazi wanapoona hivyo, hawaruhusiwi kulia wala kukaa matanga hadi shughuli za jando

zimalizike. Walisema sababu ya kufanya hivyo ni siri iliyopo jandoni, na kwa kwamba inasaidia kuzuia hofu ya wazazi wengine kupotelewa na vijana wao. Wazazi waliofiwa wanashauriwa kuwa wasiri na wavumilivu wasiweze kuwaathiri wazazi wengine.

Tamathali za semi zimetumika katika nyimbo hizo. Haya ni maneno, methali, nahau, au misemo, ambayo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana au kufanya kazi ivutie. Tamathali za semi huipamba kazi ya fasihi na kuongeza athari za maana iliyokusudiwa. Kwa maneno mengine, tamathali za semi ni jumla ya lugha inayojenga taswira mbalimbali kwa msomaji au msikilizaji.

**Sitiari**

Hii ni tamathali ya semi ambayo sifa ya kitu fulani hufananishwa au hulinganishwa na kitu kingine kama kitu hicho ni sawa na kabisa. Sitiari imetumika katika nyimbo za Kihiyao za jando na unyago. Kwa kufanya hivyo kijana anaweza kufananisha jambo fulani na tendo linalofanyika na kumfanya atafakari matokeo ya jambo hili.

**Tanakali**

Hii ni tamathali ya semi ambayo maneno yanayofanana na aina fulani za sauti za vitu vinavyowakilishwa kurudiwarudiwa. Kwa mfano katika wimbo wa unyagoni wa kumfunda binti aweze kumtunza mume wake asije akaoa mume mwingine. Sauti ya jogoo anapowika alfajiri imeingwa. "*checheleche"*

Wimbo huo unamsihi binti wa kike kumjali mume wake kipindi chote cha ndoa yao. Kwa kutofanya hivyo mume wa kihiyao ana tabia ya kumuacha mke wake na kutafuta anay**e**mfaa. *Tambala checheliche Litongo lyekulupuche* ina maana kuwa,

jogoo anapowika alfajili mume anaondoka nyumbani. *Checheliche* ni sauti ya jogoo anapowika. Hivyo sauti hiyo imefananishwa na tabia za wanaume wa Kihiyao.

**Takiriri**

Hii ni tamathali ambayo ina marudio ya maneno katika sentensi kwa lengo la kusisitiza jambo. Wahiyao katika nyimbo zao za jando na unyago, wanatumia takiriri katika kusisitiza mafunzo wanayoyatoa. Katika utafiti wetu tulizipata takiriri katika nyimbo za kuomboleza.

**Taswira**

Matumizi ya taswira pia yamejitokeza katika nyimbo za kihiyao. Lengo ni kuibua hisia kuhusu jambo linalofundishwa kwa vijana. Hali inayomfanya kijana asikilize kwa makini na kuyashika yale yanayozungumzwa.

Katika nyimbo za Kihiyao kuna matumizi makubwa ya lugha ya Kihiyao na Kiswahili.hii inatokana na kwamba kila lugha inakua kimsamiati.

# SURA YA SITA

# 6.0 HITIMISHO, MAPENDEKEZO MAREJELEO

## 6.1 Hitimisho

Utafiti wetu ulilenga kukusanya na kuchanganua data, kuhakiki na kuelezea mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao wa Lulindi Wilayani Masasi. Utafiti wetu uliweka msisitizo zaidi juu ya mafunzo yapatikanayo kwenye nyimbo za jando na unyago kama sehemu ya fasihi simulizi. Nyimbo za jando na unyago zimekuwa na mjadala mkubwa kwa jamii ya Wahiyao. Hii imetokana na mwelekeo hasi wa vijana wa kihiyao. Hali hiyo ilichochea kufanyika kwa utafiti huu ili kupata ukweli wa yale yanayosemwa na wasemaji wa tatizo hilo.

Utafiti pia ulizingatia lugha inayutumika katika kutoa mafunzo ya nyimbo za jando na unyago, ambapo kipengele hiki kimetumika katika uchanganuzi wa data zilizokusanywa kuhusu mafunzo ya jando na unyago. Matokeo ya uchanganuzi wa data katika tasnifu hii yamedhihirisha kwamba mafunzo ya nyimbo za jando na unyago yana kasoro ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho kwa jamii ya Wahiyao wa Lulindi Masasi na wilaya ya Masasi kwa ujumla wake.

Kazi hii ya utafiti imetudhihirishia kuwa mafunzo ya nyimbo za jando na unyago lengo lake ni kumuandaa kijana aliyefikia utu uzima kuishi maisha ya kiutu uzima. Kwa mfano, kijana wa umri wa miaka 9-12, ni kipindi cha balehe kwake. Hivyo akifundishwa mambo ya ki-utu uzima ataelewa na ataweza kutumia mafunzo hao katika maisha yake yote.

Kinyume na matarajio hayo, jamii ya wahiyao wanatumia elimu hiyo kama sehemu ya kuonyeshana utajiri na ufukara wao. Vijana wanaopelekwa jandoni na unyagoni ni wa umri mdogo kuanzia miaka 2-5. Ukweli ni kwamba kwa umri wao ni wadogo hawawezi kutunza siri ya mafunzo ya nyimbo za jando na unyago. Wanapewa mafunzo ya kiutu uzima katika umri mdogo na hatima yake vijana hao kukosa maadili kwa vile waliyofundishwa ya msingi ni machache na machache hayo wanajaribu kuyafanyia majaribio. Hatima ya majaribio hayo kama namna ya kumtunza mume kwa kumpa chakula cha ndoa na ashibe asije akatafuta chakula hicho kwingine, matokeo ya majaribio hayo ni vijana hao kupata ujauzito na kuzaa kabla ya umri wao wa utu uzima na kujitokeza kwa mmomonyoko wa maadili.

Utafiti umebaini kuwa vijana wengi wa Kihiyao wa Lulindi ni walevi wa pombe, na wavivu. Hawajali kazi wala malezi ya familia zao. Wanategemea zaidi wazazi wao, yaani bibi na babu, kuwalelea watoto wao na wao wenyewe kunywa pombe au kukimbilia mijini.

## 6.2 Mapendekezo

Kama fasihi simulizi inatendeza mambo kwa jamii yake, basi jamii haina budi kuitazama fasihi simulizi yake kwa kila jamii kwa mtazamo chanya kwa lengo la kuwa ni chombo cha ukombozi kwa jamii. Fasihi simulizi itumike kuelimisha jamii na kutoa mwelekeo mwema kwa jamii yake. Fasihi pia ikosoe na kuirekebisha jamii pale inapokosea. Jamii itumie fasihi simulizi katika kuyarekebisha maovu yao. Hatuna budi kufahamu kuwa fasihi simulizi ikitumiwa vema na jamii, jamii itapata maendeleo bora.

Ili kurekebisha tatizo linalojitokeza kwa jamii ya Wahiyao wa Lulindi Masasi la kutoa mafunzo ya jando na unyago kwa vijana wadogo, yapasa jamii ijitambue, ijitathimini, ijichambue na kujikosoa mapungufu yake ili iweze kurudisha maudhui ya awali ya mafunzo ya nyimbo za jando na unyago kama ilivyokusudiwa hapo awali.

Mafunzo hayo yalilenga kuwaandaa vijana na kuwakuza katika maisha ya kiutu uzima. Mafunzo hayo yaliwasidia sana vijana na vijana wengi waliweza kumudu kuishi maisha yao kwa kuyaendesha wenyewe bila kutegemea wazazi. Kinyume na matarajio hayo, mafunzo hayo sasa yamekuwa ni sehemu tu ya kutimiza jadi hiyo pasipo kuwa na manufaa yoyote.

Jando na unyago sasa imekuwa ni sehemu ya makusanyo ya pesa na mali kwa jamii. Ni sehemu ya kuonyeshana utajiri na umasikini wa miongoni mwa wanajamii. Mfumo wa maisha tulionao hivi sasa ndiyo unaotulazimisha kuibadili fasihi yetu simulizi ambayo ni kongwe kwa jamii zetu. Fasihi simulizi ni mkombozi wa maisha ya jamii. Inasaidia kumkomboa na kumnyoosha mwanajamii na kumuweka sawa

aweze kuishi vema na jamii yake. Kila jamii ina fasihi yake inanyoongoza jamii hiyo.

Kama jamii ya Wahiyao wa Lulindi watarekebisha utaratibu wa utoaji wa elimu ya jando na unyago na kutoa mafunzo hayo kama awali hasa kwa kuzingatia wanaopewa elimu hiyo ni wale waliokaribia au kufikia utu uzima, basi elimu hiyo itakuwa bora na itasaidia kurekebisha kasoro zinazojitokeza.Ni elimu inayofaa kwa jamii na inapaswa ipitiwe na kila mmoja katika jamii

Jamii ikisaidiana na serikali ihakikishe kuwa elimu ya jando na unyago ina rudishiwa hadhi yake ili kupunguza wimbi la vijana waliokosa maadili. Umri wa vijana wa kupata elimu hiyo uwe ni ule wa utu uzima ili waweze kuyakabili maisha ya kiutu uzima. Masuala ya kisiasa yasiingilie uendeshaji na utoaji wa mafunzo hayo kwa jamii.

Mipango ya pamoja miongoni mwa wanajamii inatakiwa iwekwe imara ili kudhibiti utoaji wa elimu ya nyimbo za jando na unyago kwa umri unaofaa. Hii iende sambamba na ushirikiano na idara za utamaduni za Wilaya, Mkoa na hadi Taifa kwa kuzingatia haki za kimataifa za uendelezaji wa utamaduni kwa jamii. Kuwa kila jamii ikuze utamaduni weke na kuutumia ili kuenenda kulingana na matakwa ya jamii hiyo. Kila jamii ina njia yake ya kutoa wa elimu ya maisha kama ilivyo jamii ya Kihiyao kwa kutumia nyimbo za jando na unyago. Ziko jamii nyingi Tanzania na Afrika zinazotoa elimu ya jando na unyago kwa njia tofauti. Utafiti wetu umeangalia tu jamiii moja ya wahiyao waishio Lulindi Wilaya ya Masasi.

## MAREJELEO

Abdallah.Y B (1993) *The Yaos-Chikala cha wayao*, Second Edition printed in Great Britain by Clarke, Doble and Brendon ltd.plymouth and Ltd London

Abdilatif. A (1971) *Utenzi wa Maisha ya Adamu na Hawa*, Oxford University Press.

Ahmed.E.N (1994) *Marudio na Mazoezi kwa Vyuo vya Ualimu*. East African Educational Nairobi.

Ali, A.A.EL-Maawy (2011) *Jawabu la mwanakupona* (Mausiyo ya mke wa kisasa na wasiya wa Mwanakupona.TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Allen. J.W.T (1971) *Tendi*, Heinemann Educational Books Ltd. Graet Britain, Richard Clay (The Chaucer press Ltd) Bungay, Suffolk.New Delhi

Ameir.I.H (1983) *Misingi ya Nadharia ya Uhakiki*. TUKI, Dar es Salaam

Austin. J. S (Mhariri) (1968) *The African Assertion.A Critical Anthology of African Literature*. State University College. New Paltz.New York.

Bernth .L na Ulla S. (Wahariri) (1976) *Neo.African Literature and Culture.Essay in Memory of Janheinz Jahn*.B, Heymann Verlag GmbH, Weisbaden, Germany.

BEST, W.J na Khan (1992) *Research in Education*. New Delhi Prentice

Bukenya. A na wenzake (wahariri)(1994) *Understanding oral literature,* Nairobi University Press, University of Nairobi Library cataloguing in publication Data.

Cohen. L.L.M na Keitle. M (2001) *Research Methodology Education*, London, Routlege farmer. Dar es Salaam

Denscombe, M (1998) *The Good Research for Small Social Reseach Projects*, Buckihari: Open University Press, India.

Enon, J.C (1998) *Educational Research Statistics and Measurements*. Kampala Makerere University.

Fennegan. R (1970) Oral Literature in Africa.Oxford: University Press.

Gerard. A .S (1971) *Four African Literatures.Xhosa, Sotto, Zulu, Amharic, University* of Colifonia Press Ltd, London, England.

H.Bin Ismail. H na Lienhardt.P (Editors and Transilated) (1968) The *Medicine Man, Swifa ya Nguvumali*.Oxford University Press.Great Britain, Ely House, London W.

Hoopes.J (1979) *Oral History: An introducation for Students*, The University of North Carolina, Chapel Hill.

Howard.J na wenzake (1982) *Sociology: Traditional and Radical Perspectives*, British Library cataloguing, publication, The Pitiman Press Ltd, Bath.

I.Olpewho.I(1992) *Africa Oral Literature. Backgrounds, Character and Continuity. Indiana* University Press, 60/North Morton Street, Bloomington, IN 47404-3797 U.S.A.

Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es salaam, (1995) *Kioo cha Lugha*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Jan .V (1985). *Oral Traditional as History*.Nairobi, Heinemann, Kenya.

Jopo la Utafiti kuhusu Liyongo (Wahariri) (2006), *Nyimbo za Liyongo, Liyongo Songs*, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Keya S.O. na wenzake (1989) Guideline *for the proposal*, Nairobi, Oxford University Press.

Kiango, S.K na Sengo.T.S.Y (1973*) Hisi Zetu*, Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Kisanji. J (2011) *Miiko ya jamii ya wabungu*. Dar salaam Huda Publishers

Kothari, C.R (1993) *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delhi – India, Wiley Eastern Ltd.

Kuappert.J na Brill.E (1967) *Traditional Swahili Peetry*. An investigation into the concepts of East Africa Islam as Reflected in the Utenzi Literature. Netherlands.

Lucas.S.A (Mhariri) (1975) *Utani Relationships: The Yao*,

Lyndon. H. (Editor) (1965) *Swahili Prose Text. A selection from the material*. Collected by Carl Velten from 1893 to 1896. Oxford University Press, Nairobi. (Assoc-Professor of Swahili Language and Literature University of Wisconsin, U.S.A.)

Lyndon. H. (Editor) (1966) Poems from Kenya. The University of Wisconsin Press, Madison, Milwaukee and Londan.

Makumbusho ya Taifa (1998) *Historian ya baadhi ya Mila za Masaai*. Dar es salaam, Makumbusho ya Taifa.

Mapunda .H. (1979). *Historia ya mapambano ya Mtanzania*. Tanzania Publishing House. Dar es Salaam.

Mayala (2009) *Basukuma Jokes FASS OLT 325* Dar es Salaam. The Open University of Tanzania

Mayoka.J.M (1993). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*, Benedictine publication Ndanda-Peramiho Tanzania.

Minduva .H.M (M.A 2004). *The Impact of grade B/C-A Teachers upgrading Programme in enhancing Teaching and learning Process in Primary school*. University of Dar es Salaam.

Mbogo .E (2008) *Ngoma ya Ng'wana Malundi*. Nyambali Nyangwine Publishers, Dar es Salaam.

Mkinya. B (1991) *Historia, Mila na Desturi za Wazanaki,* Benedictine publications Ndanda-Peramiho Tanzania.

Mlacha A.C. A. V (1989) *Lugha na Fasihi,* Oxford University Nairobi.

Muller. H.N (1970) *Statistical Reasoning in Sociology Boston*. Hongton Mufflin Company.

Mulokozi. M. M. (1999) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

Mulokozi. M. M. (Mhariri) (1999) Tenzi Tatu za Kale (Fumo Liyongo, Al-Inkishafi na Mwana Kupona) TUKI, Dar es salaam.

Mwenda. N (Ph, D. 2004) *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Augustana College. Rock Island. IL 61201.

Ndungo, W, (1991) *Misingi ya Nadharia ya Fasihi ya Kiswahili*. Nairobi University.

Ngugi .T (1990) This Time Tomorrow.Kenya Literature Bureau,Nairobi .

Njiru. E (1981) *Indigenous Education as practiced. By Ameru: with special reference to circumcision ceremonies.* M.A, Thesis, University of Nairobi.

Nkwera. F. M. V (1978) *Sarufi na Fasihi-Sekondari na Vyuo*,Dar saalam Tanzania, Publishing house.

Okpewho.I (1992) *African Oral Literature. Backgrounds, character and continuity*.Indiana University Press, 601 North Morton street.Blooming, IN474043797 U.S.A.

Omari.C.K na Mvungi. M (1981) *Mitaala ya Lugha na Fasihi Na.9, Urithi wa Utamaduni Wetu*; TPH, Dar es salaam Tanzania

Othuman.S.Y na Yahya.A (Wahariri) 2004, Howan Mwana wa Howani, TUKI, Chuo Kikuu cha Dar-salaam.

Richard M.Dorison (Editor) (1968) *Peasant Customs and Savage Myths, selection from the British folklorists,* Volume one.London Routledg and Kegan Paul.Great Britain by Butler and Tanner ltd.

Rinehart.H na Winsion (2001) *World Literature*, Printed in the United States of America.

S, A, Mazingwe.S.A (1991) *Fasihi ya Kiswahili*, Ndanda Misheni Press Benedictine, Pubilication, Tanzania

Sengo T, S, Y, M (2008) *Tafakuri ya Utu na Uhai*, Dar salaam Huda Publishers

Sengo T, S, Y, M (2008) *Tungizi ya Mnyangatwa*, Dar salaam Huda Publishers

Sengo T.S.Y. (1992) *Shaaban Robert, uhakiki wa Maandishi Yake*. KAD Associates,

Sengo T.S.Y.M. (1988) *Fasihi Simulizi Sekondari na Vyuo*, Nyanza Dar es salaam

Sengo T.S.Y.M. (2009) *Utafiti wa Utani: Ukwereni.*Dar es Salaam AERA Kiswahili Researched Products

Senkoro.F.E. M. K (1982) *Fasihi*, Dar es Salaam Press and Publicity Centre.

Senkoro.F.E.M.K (1987*) Fasihi na Jamii*, Press and Publicity Centre Dar es salaam.

Senkoro.F.E.M.K (2011) *Fasihi*, KAUTT Limited, Dar es Salaam.

Senkoro.F.E.M.K na Kahigi.K.K (Wahariri) 2007, Kioo cha Lugha,Idara ya Kiswahili,Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Somjee.S. (1987) Material culture and Teaching of Art, Paper presented at the International Conference on Art, McGill University, Canada

Soyinka. W (1975) *Poems of Black Africa*. Great Britain by Richard Clay(The Chaucer press) Ltd, Bungay, Suffolk.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Tanzania (1987) *Mulika Na 19*, Dar-salaam.

Taban L. L (1972*) Popular Culture of East Africa: Oral Literature*, Longman Kenya Ltd Harambee Avenue, Nairobi.

TATAKI, (Mahariri. Mulokozi.M.M) 92011) *Nyimbo za Kumbi*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (1978) *Kiswahili, (Journal of Institute of Kiswahili Research*) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (1981) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Oxford University Press, Nairobi

TUKI (1985) *MULIKA Na 18* Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

TUKI (1986) *MULIKA Na 17* Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

TUKI (1992) *Kiswahili Vyuoni* .KIUTA –NPC-Dar es salaam.

TUKI (2000) *MULIKA Na 26* Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

TUKI (2001) *Kiswahili Juzuu 64*, Jarida la TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (2002) *Kiswahili, Jarida la TUKI*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

TUKI (2004) Kamusi ya Kiswahili Sanifu.University of Dar es salaam.

TUMI (1992) Kiswahili Vyuoni, KIUTA-NPC Dar es salaam

Vedasto. A. K (2010) *Chopikwa Kikapikika*, IDEA Publishers, Dar es Salaam. Tanzania.

Wembah.J.A.R (1975) *The Ethno –History of the Matrilineal Peoples of Southeast Tanzania.* Anna Hohenwart-Gerlachstein Wien Austri der universitat Wien.

WWW.Answers.com/topic/economic-growth-2

## NYONGEZA

**KIAMBATANISHI Na 1 maswali ya viongozi wa jando na unyago.**

1. Unaelewa nini kuhusu nyimbo za jando na unyago katika kabili la Wahiyao?
2. Tangu lini unaifanya kazi hii ya kufundisha nyimbo za jando na unyago?
3. Ni watu wa umri gani wanaostahiki kupata elimu ya nyimbo za jando na unyago katika kabila hili la Wahiyao.
4. Ni vifaa gani muhimu vinavyotumika kwa shughuli za nyimbo za jando na unyago?
5. Jee, nyimbo za jando na unyago zinawafundisha nini vijana wa Kihiyao?
6. Nyimbo za Jando na unyago hufanyika katika mazingira yapi?na kwa sababu zipi.?
7. Ni lugha ipi hutumika wakati wa kutoa elimu ya nyimbo za jando na unyago?
8. Kuna matatizo yoyote unayokumbananayo wakati wa shughuli za nyimbo za jando na unyago?

9. Ni watu gani wanaohusishwa kuingia sehemu inapotolewa elimu ya nyimbo za jando na unyago?
10. Una maoni gani kuhusu nyimbo za jando na unyago?

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**MASWALI YA VIJANA WALIOPITIA JANDO NA UNYAGO**

1. Umepitia nyimbo za jando na unyago ukiwa na umri gani?
2. Kuna manufaa yoyote uliyoyapata?
3. Jee, mafunzo ya nyimbo za jando na unyago yanakusaidiaje katika maisha yako hivi sasa?
4. Shughuli gani mnazozifanya mkiwa jandoni au unyagoni?
5. Nyimbo zinazoimbwa jandoni au unyagoni zinatungwa na nani? Kwa nini?
6. Kuna siri zipi zinazozuia nyimbo za jandoni na unyagoni zisiimbwe hadharani?
7. Nini chanzo cha nyimbo za jando na unyago kwa jamii ya Wahiyao?
8. Una jibu gani kwa watu wanaoitukana na kuikashifu mila hii ya nyimbo za jando na unyago?
9. Jee?, unafikiri “kitchen parties” (khafla za kukusanya pesa na kufundwa na wasiyofundwa ) JKT,Madrasa,shule,Misikiti na Makanisa,zimeweza kuchukua nafasi ya nyimbo za jando na Unyago katika kufanikisha elimu ya maisha ya kiutuuzima, nidhamu na utu wa jamii?

10. Una maoni gani ya jumla kuhusu nyimbo za jando na unyago?

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**MASWALI KWA WAZAZI**

1. Wewe ukiwa mzazi, unajisikiaje kama mwanao hajapitia nyimbo za Jandoni na Unyagoni?
2. Kuna manufaa gani ya kuwepo kwa shughuli za nyimbo za jando na Unyago katika kabila lenu la Wahiyao?
3. Kuna mabadiliko yoyote kwa kijana wako baada ya kutoka jandoni? Yataje…
4. Jee, mototo anapokuwa jandoni au unyagoni,mzazi unahusishwa vipi? Unauhusiano upi na walimu wanaoishi na vijana Jandoni?
5. Ni nani ana wajibu wa kumlea kijana awapo jandoni?..... Kwa gharama gani?.....
6. Kwanini vijana wanaopelekwa jandoni na unyagoni ni wadogo ukilinganisha na hapo awali?.....
7. Kwanini jamii inalalamikia utovu wa adabu, utovu wa maadili, utovu hadi wa utu nchini mwetu?

8. Jee, Jando na Unyago, vyuo hivi vina nafasi ipi kuendeleza mambo mama katika jamii ambazo zinaviyahamini na kuvienzi?
9. Maoni ya jumla?

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**MASWALI KWA NGARIBA**

1. Ulianza lini kazi hii ya ungariba?.....
2. Kuna vikwazo gani unavyokutana navyo wakati wakati wa kutahiri?
3. Ni mambo gani unayofanya wakati wa shughuli za nyimbo za jando na unyago?
4. Ni vifaa gani unavitumia kwa kutahiri vijana.
5. Kuna madhara yoyote yanayoweza kuzuka kutokana na vifaa vya kutahili?
6. Sayansi na teknolojia za kigeni zinaathiri vipi kwa shughuli za nyimbo za jando na unyago?.....
7. Una maoni gani ya kuendelezea elimu hii ya nyimbo za jando na unyago?
8. Uganga wa jandoni ni tofauti na uganga wa kutibu nje ya jando?.....
9. Maoni ya jumla……

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**MASWALI KWA MWENYEKITI, DIWANI, MTENDAJI WA KIJIJI**

1. Una muda gani katika uongozi wa kijiji?
2. Shughuli za nyimbo za jando na unyago zinaendeshwa na nani? Kwa namna gani? Taarifa unazipataje?
3. Kuna utaratibu wowote uliowekwa juu ya shughuli za nyimbo za jando na unyago hapa kijijini kwenu?
4. Una maoni gani juu ya uendeshaji wa shughuli hii ya nyimbo za jando na unyago hapa kijijini kwenu?
5. Matatizo yakitokea, unahusika vipi?
6. Matusi ya wasungo dhidi ya urombo wa nyimbo za jando na unyago, wewe, ukiwa kiongozi na mwenyeji wa mila hii, una majibu yepi?
7. Unatoa maoni na ushauri gani kwa (a) Serikali?
8. Jamii juu ya nyimbo za jando na unyago.

**ASANTE KWA USHIRIKIANO WAKO**

**Fomu ya uchunguzi jandoni na unyagoni**

| Muda | Vitendo vya makugwi,nyakanga | Vitendo vya vijana | Vifaa vinavyotumika | Kiwango cha utendaji |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

Maoni ya mtafiti……

**PICHA ZA VIJANA WA KIUME WAKIWA JANDONI**

Vijana wakiume wa kabila la wayao siku chache kabla ya kutoka jandoni

Sherehe ya ngoma ya asili ya chingenge, kusherehekea kurudi kwa vijana kutoka jandoni.

**RAMANI YA TARAFA YA LULINDI WILAYA YA MASASI**

QuickTime™ and a
decompressor
are needed to see this picture.